

# **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE**

**IMEANDIKWA NA: SHEIKH MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYA**

**IMETAFSIRIWA NA: SHEIKH HASAN MWALUPA**

**IMEHARIRIWA NA: USTADH ABDALLAH MOHAMED**

**IMEPANGWA KATIKA KOMPYUTA NA: UKHT PILI RAJABU**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu

## **UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI**

Kitabu hiki kilichoko mikononi mwako hivi sasa ni juhudi ya miaka mingi sana ya watu waliojitolea kuona kazi hii imefanikiwa bila ya kumsahau Marhum Abu Muhammad wa London.

Kama lilivyo jina la Tafsiri yenyewe ndivyo ilivyo Tafsiri yenyewe ambayo mwanachuoni huyu mahiri kabisa aliyeifafanua ni mtu aliyebobea katika fani zote ambazo mfasiri (Mfafanuzi) anatakiwa awe nazo. Sheikh Muhammad Jawad Mughniyya ameonesha cheche zake katika vitabu vingi alivyoviandika katika maudhui mbali mbalimbali na hivyo kujipatia wasomaji wengi sana.

Msomi huyu, mwenye fikra huru na anayetetea kile anachokiamini, ni mtu mwenye mawazo mapana na kuyaangalia mambo kwa undani sana, kipaumbele chake ni katika maslahi ya umma huu na amejaribu sana kwenda na wakati.

Sifa kubwa pekee ya mwanachuoni huyu ni kuwa yeye hakujihusisha sana na kung'ang'ania madhehebu fulani tu, labda hii yatokana na wadhifa wake wa ukadhi aliokuwa nao katika nchi ya Lebanon ambayo ina madhehebu mengi, ambapo sula la madhehebu ni nyeti nchini humo, hata hivyo yeye aliweza kuamua matatizo ya watu kwenye ofisi yake kulingana na madhehebu yao pale walipomwendea, hiyo ilimsaidia sana hata kuweza kutoa kitabu kitwacho 'Al-Fiqh a'laa madhaahabil-khamsah' (Fikhi ya madhehebu matano) yaani ya Hanafi, Maaliki, Shafi, Hambali na Shia (ambacho twataraji kitatoka hivi karibuni Inshaallah).

Jambo lililotupa msukumo wa kukifasiri kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili ni zile faida nyingi atakazozipata msomaji na kujua mambo mengi na ya ajabu yaliyo mapya kwake ambayo si rahisi kuyapata kwa wafasiri wengine.

Msomaji atapata faida katika fani za Sayansi, Siasa, Historia, Mashairi, visa vizuri, na Saikolojia miongoni mwa mengine; ndiyo maana msomaji atashangaa kidogo anapoisoma Tafsiri hii atakapoona mwandishi amewataja na kuwanukuu watu kama kina Mfalme Edward, wanasyansi kama kina Einstein, Charlie Champlin (Mchekeshaji maarufu), na wengineo, hali inayoifanya tafsiri hii kuwa ni ya kipekee kabisa.

Mtindo alioutumia mwandishi ni sahali uliokusudiwa watu wa tabaka mbalimbali, wanavyuoni na watu wa kawaida.

Nia yetu ni kukigawanya kitabu hiki bure lakini tumelazimika kukiua kwa bei nafuu ili kurudisha gharama za uchapishaji.

**Mwisho:** Shukrani kubwa iwaendee bila ya kuwataja watu waliojitolea usiku na mchana, jopo la wafasiri, wahariri, wachapaji, waliotupa moyo na kutoa maoni yao na walioisimamia ili kuhakikisha kwamba kitabu kimemfikia msomaji.

### **MAKOSA YA CHAPA**

Sikumbuki kama nimewahi kusoma kitabu kilichotoka kupigwa chapa, cha zamani au cha sasa, bila ya kukuta makosa ya chapa, Nafikiri sitasoma kitabu kisichokuwa hivyo. Nimejaribu sana kuliepuka hilo katika tungo zangu, lakini sikufanikiwa.

Nilikuwa sifikirii kama ninaweza kuona makosa haya katika maandishi ya msahafu mtukufu, kama yale yaliyo katika baadhi ya chapa; kwa mfano neno yabswutu kwa swad, badala ya yabsutu kwa sin, na katika chapa ya Tafsir Arrazi ya Misr ya mwaka 1935, Sura ya (2:146). Imeandikwa La Ya'alamuun, (hawajui) badala ya Ya'alamuun (wanajua), Mfano wa makosa haya hausameheki.

Katika Tafsir Al-Manar, chapa ya Pili, sura (5:212), imeandikwa "Fawqahum ila yawmil qiyama" badala ya "Fawqahum yawamal qiyama", Hatuwezi kusema kosa hili ni kubwa zaidi kuliko lile.

Lakini mkosaji atatuletea udhuru kwa msemu mashuhuri huko kwetu jabal amail 'Makosa ya chapa.'

Katika Tafsiri Majmau chapa ya Urfan, Sura (46:15), imeandikwa: "Hatta idha balagha arbai' na sanah badala ya: Hattaidha balagha ashuddahu arbai ' na sanah"

Kusema hivi sio kama ninajitetea kutokana na makosa ya chapa atakayoyakuta msomaji katika kitabu hiki, ijapokuwa naomba msamaha kama litatokea hili, lakini makusudio yangu hasa ni kumwambia yule atakayefungua macho yake kwenye makosa ya matamko na kuufungua macho uzuri wa maana.

Vilevile ninamwambia yule ambaye siku moja aliniambia: "Vitabu vyako vimejaa makosa ya chapa, kama kwamba hakuna kitu chochote katika vitabu hivyo isipokuwa makosa ya chapa tu. Wote hao ninawaambia: Mungu awasamehe na aniongoze mimi na nyinyi.

Vyovyote iwavyo, mimi ninaomba msamaha kutokana na makosa ya kifikra na ya chapa. Anasema Amirul Muminiin <sup>(a.s)</sup>: **"Watu wote ni wapungufu wenye kuchanganyikiwa, isipokuwa yule aliyehifadhiwa na Mwenyezi Mungu."**

Na Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye mwenye jukumu la kunikubali- ayale niliyoyapatia na kunisamehe niliyakosea, kwa jaha ya Mtume na kizazi chake, ziwashukie rehema na amani (Amin).

**MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYAH**

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

Muendelezo Wa Sura Ya Sita: Al-An'am

وَلَوْ أَنَّا نَزَّلْنَا إِلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةَ وَكَلَّمَهُمُ الْمَوْتَى وَحَشَرْنَا عَلَيْهِمْ كُلَّ شَيْءٍ فُبَلَا مَّا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا  
إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ يَجْهَلُونَ ﴿١١١﴾

111. Na lau kama tungewateremshia Malaika, na wafu wakazungumza nao, na tukawakusanyia kila kitu ana kwa ana, wasingeliamini ila atake Mwenyezi Mungu, Lakini wengi wao wamo ujingani.

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيَاطِينَ الْإِنسِ وَالْحَيِّ يُوْجِي بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ زُخْرَفَ الْقَوْلِ  
غُرُورًا وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوهُ فَذَرَّهُمْ وَمَا يُفْتَرُونَ ﴿١١٢﴾

112. Na kama hivyo tukamfanyia kila Nabii adui, mashetani watu na majini. Baadhi yao wanawapa wenzao maneno ya kupambapamba kuwahadaa. Na kama Mola wako angelitaka wasingeliyafanya. Basi waache na wanayoyatunga.

وَلِتَصْغَىٰ إِلَيْهِ أَفئِدَةُ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ وَلِيَرْضَوْهُ وَلِيَقْتَرِفُوا مَا هُمْ مُّقْتَرِفُونَ ﴿١١٣﴾

113. Na ili zielekee hayo nyoyo za wale wasioamini akhera, nao wayaridhie na ili wayachume wanayoyachuma.

### AINA YA WATU AYA

Aya 111 – 113

#### MAANA

Na lau kama tungewateremshia Malaika, na wafu wakazungumza nao, na tukawakusanyia kila kitu ana kwa ana, wasingeliamini ila atake Mwenyezi Mungu.

Tumesema katika Tafsir ya Aya iliyotangulia kuwa jamaa katika washirikina walimtaka Mtume (s.a.w.w) awalettee muujiza maalum; na kwamba waumini walitamani lau Mwenyezi Mungu angeliitikia maombi yao; na Mwenyezi Mungu akawajibu waumini kwa kauli yake: “Na ni kitu gani kitakachowatambulisha ya kuwa zitakapowafikia hawataamini?”

Baada ya kuishiria yote hayo, Mwenyezi Mungu Mtukufu amemfananulia Mtume wake mtukufu, kwamba hawa washirikina ambao wamekutaka waliyoyataka katika miujiza, hawatakuamini kwa hali yoyote; hata kama tutawateremshia Malaika kutoka mbinguni, na tukawafufulia wafu wakashuhudia kwa lugha fasaha ya Kiarabu kuwa wewe ni Mtume, bali hata kama utakushuhudia ulimwengu ardhi yake na mbingu yake, wasingelikusadiki wala kukufuata ‘ila atake Mwenyezi Mungu;’ yaani Mwenyezi Mungu awalazimishe wakuamini wewe kwa nguvu.

**Unaweza kuuliza:** Je, kukadiria huku ni sawa?. Na je aina hii ya watu inaweza kupatikana, katika hali ya kawaida?. Itakuwaje kikundi kidogo kiukadhibishe ulimwengu na vilivyomo? Je, inawezekana mtu asiamini masikio yake na macho yake, kwa kuwaona wafu wanafufuka kutoka katika makaburi yaliyochakaa maelefu ya miaka na waseme. ‘Hapana mola

isipokuwa Mwenyezi Mungu (na) Muhammad ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu;’ wasikie wanyama na ndege na samaki na miti na nyota zote, zikinadi shahada mbili; inawezekana kweli aweko mtu atakayekadhibisha miujiza yote hii? Si ajabu hiyo?

**Jibu:** Kukadiria hivi si sawa, bali ni muhali kwa wale wanaoathirika na haki na dalili yake, na wanaokwenda pamoja na wahyi wa mantiki ya kiakili na umbile la Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu. Kwa sababu miujiza hii ni dalili mkato isiyokuwa na shaka yoyote.

Ama kukadiria huku kwa watu ambao hisia zao zote zinatawaliwa na masilahi mahususi na kuyaona kuwa ndio akili, ndio umbile na ndiyo haki na uadilifu, basi ni sahihi. Kwa sababu aina hii ya watu ipo, nao ni wakoloni na walanguzi na wengineo mfano wao, ambao wanaishi kwa unyang’anyi na ufisadi.

Wale wanaoona ajabu kukadiria huku hawaitambui hali halisi ya kundi hili, na wamechanganya baina ya mantiki ya kiakili na ya yule mwenye kuongozwa na manufaa.

Akili kwa maana ya akili ni ile tu iliyo mwongozi, anayeamrisha na kukataza; wala haimsikilizi isipokua anayetafuta haki kwa njia ya haki. Ama chenye kuongoza na kuelekeza kwenye manufaa basi hicho ni manufaa ya kibinafsi.

Hicho peke yake ndicho kinachowaongoza katika mambo yao na silika zao. Ndiyo dini yao, ndiyo akili yao, bali ndiyo utu wao na uhai wao. Kwa sababu hiyo, hakuna mantiki yoyote yanayowafaa isipokuwa nguvu aliyoiashiria Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa kauli yake: ‘Ila atake Mwenyezi Mungu.’

**Lakini wengi wao wamo ujingani**

Hawajui kuwa wao ni kikundi kiovu ambacho hakifaliwi na mantiki ya kiakili na maumbile wala na mantiki ya dini na utu; wala kitu chochote ila nguvu na kushindwa. Ni makosa na ni kupoteza wakati kuzungumza na watu hawa kwa lugha ya elimu na ubinadamu.

**Na kama hivyo tukamfanyia kila Nabii adui, mashetani watu na majini.**

Shetani mtu ni maarufu, ni kila anayehadaa watu kwa kuwaingiza kwenye batili na kuwavisha nguo ya haki. Ama jinni yeye ni katika mambo ya ghaibu ya Mwenyezi Mungu. Nasi tunaamini kijumla na kimsingi; wala hautuhusu ufafanuzi; kwani hatutaulizwa kuhusu yeye; sawa na ilivyo katika Malaika. Wala si ajabu kwa Manabii kuwa na maadui. Kwa sababu, ni kawaida kuwe na uadui kati ya kheri na shari, na baina ya haki na batili.

**Unaweza kuuliza:** Ikiwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye aliyewajaalia Manabii wawe na maadui, kama inavyoonyesha katika Aya, kwa nini basi awaadhibu kwa kuwafanyia uadui Mitume? Vilevile vipi ameamrisha kuwafuata Mitume kisha akawafanyia maadui watakaowapinga na kuwahadaa watu kuwapinga na kuupinga Utume wao?

**Jibu:** Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewatuma Mitume na akafanya kazi yao ni kulingania Tawhid na uadilifu na kuondoa dhuluma na ushirikina.

Kazi hii, kwa tabia yake, huleta mgongano na vita baina ya Manabii na wale waabudu masanamu na wanyonyaji. Hivyo basi, Mwenyezi Mungu (s.w.t) ni sababu ya kutumwa Manabii, na Manabii ni sababu ya uadui. Kwa

kuzingatia haya umenasibishwa uadui kwake kimajazi, Anasema Mwenyezi Mungu akimsimulia Nuh <sup>(a.s)</sup>:

﴿قَالَ رَبِّ إِنِّي دَعَوْتُ قَوْمِي لَيْلًا وَنَهَارًا ﴿٥﴾ فَلَمْ يَزِدْهُمْ دُعَائِي إِلَّا فِرَارًا﴾

“Ewe Mola wangu! Kwa hakika nimewalingania watu wangu usiku na mchana, lakini mwito wangu haukuwazidishia ila kukimbia” (71: 5 – 6)

Kwa hiyo kukimbia kumenasibishwa mwito wa Nuh <sup>(a.s)</sup>, na mwito wa Nuh <sup>(a.s)</sup> ni amri ya Mwenyezi Mungu. Kwa ufasaha zaidi tupige mfano huu: Mtu amemwachia mwanawe utajiri, na ule utajiri ukamsababishia uadui na husda. Basi kimajazi: “Mzazi wake ndiye aliyempa husda ile mwanawe!”

**Baadhi yao wanawapa wenzao maneno ya kupambapamba kuwahadaa.**

Maneno ya kupambapamba ni maneno yaliyochanganywa na uwongo. Dhahiri yake ni rehema na ndani yake ni adhabu. Maana ni kuwa waovu wanawatia wasiwasi wenzao kwa mambo ya batili yaliyochanganywa haki, kwa makusudio ya kuhadaa na kuipinga haki na watu wake.

**Na kama Mola wako angelitaka wasingeliyafanya.**

Dhamir ya wasingeliyafanya inarudia kwenye amali zao mbaya; yaani uadui kwa Mitume na kuambiana wao kwa wao maneno ya kupamba. Maana ni kuwa lau Mola wako angelitaka kuwazuia kwa nguvu kufanya ubaya wasingelikuwa na uadui huo wala kuambiana. Lakini hekima yake imepitisha kuwaacha kama walivyo, wawe na hiyari bila ya kuendeshwa, wapate kuhisabiwa waliyoyafanya na kuadhibiwa wanayostahiki.

**Basi waache na wanayoyatunga katika uwongo.**

Wajibu wako ni kufikisha na ni juu yetu kuhisabu na malipo.

**Na ili zielekee hayo nyoyo za wale wasioamini akhera.**

Yaani waovu wanaambiana kauli za kupambapamba ili wazisikilize makafiri na waridhie baada ya kuzisikiliza na wazitumie bila ya kufanya utafiti. Na ili wayachume wanayoyachuma katika maasi na madhambi; na apambanuke mumin na kafir na mwenye ikhlasi na mnaifi.

Kwa ufupi ni kuwa maiblis waovu wanapambapamba kauli ili wawahadae wenye nafsi dhaifu na wapondokee kwao na wachume dhambi.

Amesema Abu Hayani Al-andalusi: “Maneno haya yako katika upeo wa fasihi, kwani mwanzo inakuwa ni hadaa, inayofuatiwa na kupondokea, kisha kuridhia na kuchuma (dhambi); kama kwamba kila moja linasababishwa na lililo kabla yake.

فَعَيَّرَ اللَّهُ أَبْتَعِي حَكَمًا وَهُوَ الَّذِي أَنْزَلَ إِلَيْكُمُ الْكِتَابَ مُفَصَّلًا وَالَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ

يَعْلَمُونَ أَنَّهُ مُنَزَّلٌ مِّن رَّبِّكَ بِالْحَقِّ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿١١٤﴾

114. Je, nimtafute hakimumu asiyekuwa Mwenyezi Mungu na hali yeye ndiye aliyewateremshia Kitab kinachofafanua. Na wale tuliowapa Kitab wanajua kwamba imeteremshwa na Mola wako kwa haki, Basi usiwe miongoni mwa wanaotia shaka.

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا ۗ لَا مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِهِ ۗ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١١٥﴾

115. Na limetimia neno la Mola wako kwa ukweli na uadilifu. Hakuna wa kubadilisha neno lake. Na Yeye ni msikizi, mjuzi.

وَإِنْ تُطِغْ أَكْثَرُ مَنْ فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۗ إِنْ يَتَّبِعُونَ إِلَّا لَآ الظَّنَّ وَإِنْ هُمْ إِلَّا

يَخْرُصُونَ ﴿١١٦﴾

116. Na kama ukiwatii wengi katika waliomo ardhini watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Hawafuati ila dhana na hawakuwa ila wenye kuzua tu.

إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ مَنْ يَضِلُّ عَنْ سَبِيلِهِ ۗ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَبِينَ ﴿١١٧﴾

117. Hakika Mola wako anawajua vyema wanaopotea njia yake na anawajua sana wanaoongoka.

## NIMTAFUTE HAKIMU ASIYEKUWA MWENYEZI MUNGU

**Aya 114 – 117**

### MAANA

Je, nimtafute hakimu asiyekuwa Mwenyezi Mungu na hali yeye ndiye aliyewateremshia Kitab kinachofafanua?

Aya hii inaambatana na ile Aya ya ugomvi na uadui baina ya Mtume na washirikina ambao walimtaka awaonyeshe muujiza. Maana ni kuwa Mtume (s.a.w.w) aliwaambia washirikina kwamba nyinyi mnatoa hukumu katika kutaka miujiza na mnanipangia mambo, na mimi siwezi kuikiuka hukumu ya Mwenyezi Mungu.

Qur'an imekwisha washukia, inatosha na kutekeleza mnayoyahitajia kujua haki, halali na haramu. Haina mfano wake katika misingi yake na mafunzo yake. Ni yenye kuthibitisha ukweli wake kwa kutumia ufasaha wake ushindao, ina sharia zenye kudumu milele na kutoa habari nyingi za ghaibu. Kwa hiyo, huku kutaka kwenu mambo mengi si lolote ispokuwa ni inadi tu.

Na wale tuliowapa Kitab wanajua kwamba imeteremshwa na Mola wako kwa haki.

Yaani wale wenye insafu katika maulama wa kiyahudi na kinaswara, wana- jua kwa yakini ukweli wa Qur'an na Utume wa Muhammad (s.a.w.w). Tazama Aya yenye maneno kama haya katika Juz. 2 (2:146).

**Basi usiwe miongoni mwa wanaotia shaka.**

Wafasiri wengi wamesema kuwa msemo huu (usitie shaka) anaambiwa Mtume na makusudio ni asiyekuwa yeye kwa njia ya fumbo.

Ama sisi tunaona kuwa msemo unaelekezwa kwa Mtume, na yeye ndiye makusudio, pamoja na kujua kuwa Mtume hatii shaka Qur'an, bali ni muhali kwake kutia shaka. Imesihi kuelekezwa msemo kwake pamoja na isma yake, kwa vile unatoka kwa aliye juu (Mwenyezi Mungu) kwenda kwa aliye chini, Hayo tumeyaeleza mara nyingi.

**Na limetimia neno la Mola wako kwa ukweli na uadilifu.**

Makusudio ya neno la Mola wako hapa ni Qur'an au Uislam ambao umeshinda juu ya dini zote wajapochukia washirikina. Haya ndiyo makusudio kwa ukamilifu. Ama maana ya kwa ukweli na uadilifu ni kuwa Qur'an ni kweli katika kila inayoyasema, na ni uadilifu katika kila inayohukumu na kuwekea sharia.

**Hakuna wa kubadilisha neno lake.**

Kwa sababu ni ukweli na uadilifu na kila ambalo ni ukweli na uadilifu basi ni hali halisi, wala haiwezi kusemwa jambo ni ukweli na uadilifu ikiwa

halina msingi halisi. Na msingi huu haubadiliki wala haugauki; yaani haupukani na athari na natija iliyopangiwa.

Na yeye msikizi wa wanayoyasema mjuzi wa wanayoyafanya na wanayoyadhamiria.

Na kama ukiwatii wengi katika waliomo ardhini watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Hawafuati ila dhana na hawakuwa ila wenye kuzua tu.

Kila mwenye kushikamana na dini basi huamini kwa imani ya moja kwa moja, na hushikamana nayo kwa upofu, na kila rai anayoiona huona ni kweli, na kwamba mengineyo ni njozi na dhana tu. Kwa hiyo tukizikusanya rai zote na itikadi zote na tukazipima kwa vipimo vya Mwenyezi Mungu, natija ni kuwa watu wengi hufuata dhana za makosa na za uongo.

Kwa ajili hiyo ndipo Mwenyezi Mungu akamwamrisha Mtume wake asiwasikilize watu na kutowaheshimu na ada zao na itikadi zao; na kwamba ni juu yake kufuata yale aliyopewa Wahyi na Mwenyezi Mungu kwa sababu ndiyo njia ya haki na uwongofu.

Ikiwa watu wengi wako kwenye makosa katika rai na dini, basi hakuna kipimo cha kauli zao na hukumu zao kwa uwongofu wa hili na upotofu wa lile. Isipokuwa hukumu katika hilo ni ya Mwenyezi Mungu peke yake; yaani yale aliyoyabainisha katika misingi na uthabiti uliomo katika Kitabu chake chenye hekima.

Haya ndiyo makusudio ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

Hakika Mola wako anawajua vyema wanaopotea njia yake na anawajua sana wanaoongoka.

Katika msingi hiyo ya Mwenyezi Mungu inayowapambanua wenye haki na wenye batili ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ وَمَنْ أَحْسَنُ قَوْلًا مِّمَّنْ دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ صَالِحًا وَقَالَ إِنَّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴾

“Na ni nani mbora wa kusema kuliko alinganiaye kwa Mwenyezi Mungu, na akafanya amali njema na akasema: Mimi ni miongoni mwa waislamu.” (41:33).

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

﴿فَكُلُوا مِمَّا ذُكِرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ إِنْ كُنْتُمْ بِآيَاتِهِ مُؤْمِنِينَ﴾ ﴿١١٨﴾

118. Basi kuleni katika wale waliosomewa jina la Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi mnaziamini ishara zake.

﴿وَمَا لَكُمْ أَلَّا تُكُلُوا مِمَّا ذُكِرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ وَقَدْ فَصَّلَ لَكُمْ مَا حَرَّمَ عَلَيْكُمْ إِلَّا مَا

اضْطُررْتُمْ إِلَيْهِ ۗ وَإِنَّ لَثِيْرًا لَّيُضِلُّونَ بِأَهْوَائِهِمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِالْمُعْتَدِينَ﴾ ﴿١١٩﴾

119. Mna nini hamli katika wale waliosomewa jina la Mwenyezi Mungu? Na amewafanulia aliyowaharamishia isipokuwa vile mnavyolazimika, Na hakika wengi wanapoteza kwa matamano yao bila ya ilimu, Hakika Mola wako anawajua vyema wanaoru- ka mipaka.

﴿وَدَرُوا ظَاهِرَ الْإِثْمِ وَبَاطِنَهُ ۗ إِنَّ الَّذِينَ يَكْسِبُونَ الْإِثْمَ سَيُجْزَوْنَ بِمَا كَانُوا يَقْتَرِفُونَ﴾ ﴿١٢٠﴾

120. Na acheni dhambi zilizo dhahiri na zilizofichikana. Hakika wale wanaochuma dhambi watalipwa yale waliyokuwa wakiyachuma.

﴿وَلَا تَأْكُلُوا مِمَّا لَمْ يُذْكَرِ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ وَإِنَّهُ لَفِْسُقٌ ۗ وَإِنَّ الشَّيَاطِينَ لَيُوحُونَ إِلَىٰ أَوْلِيَآئِهِمْ

لِيُجَادِلُوكُمْ ۗ وَإِنْ أَطَعْتُمُوهُمْ إِنَّكُمْ لَمُشْرِكُونَ﴾ ﴿١٢١﴾

121. Wala msile wale wasiosomewa jina la Mwenyezi Mungu kwani huko ni ufasiki, Na hakika mashetani wanawafunza marafiki zao kubishana nanyi. Na kama mkiwatii, hakika mtakuwa washirikina.

### BISMILLAH KWA KINACHOCHINJWA

Aya 118 – 121

#### MAANA

Basi kuleni katika wale waliosomewa jina la Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi mnaziamini ishara zake.

Waarabu wakati wa ujahiliya walikuwa wakila mfu, na wakitaja majina ya masanamu wanayoyaabudu wakati wa kuchinja. Mwenyezi Mungu akaharamisha hilo kwa Wailsamu; akahalalishia kula wanaochinjwa kwa sharti ya kutaja jina Lake na sio jina la mwengine.

**Unaweza kuuliza:** kuwa kujuzu kula aliyechinjwa, aliyesomewa jina la Mwenyezi Mungu, hakuambatani na kumwamini Mwenyezi Mungu na ishara zake. Ambapo inajuzu kwa kafiri kumla huyo; kama ambavyo kumwamini Mwenyezi Mungu hakuambatani na kula aliyesomewa Jina la Mwenyezi Mungu. Ambapo Mumin anakuwa Mumin hata kama hakumla. Lakini dhahiri ya Aya inafahamisha kuwa kuamini ni sharti la uhalali wa kula chinjo hilo. Kwa sababu maana yake ni, kuleni ikiwa nyinyi ni waumini.

**Jibu:** Kauli yake Mwenyezi Mungu, ‘Ikiwa nyinyi mnaziamini ishara zake,’ sio sharti la uhalali wa kula chinjo lililosomewa jina la Mwenyezi Mungu, isipokuwa hii ni kuonyesha kuwa anayemtaja asiyekuwa Mwenyezi Mungu kwa chinjo, basi amemfanyia Mwenyezi Mungu mshirika.

Kwa sababu, ameelekeza tendo lake hili kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, kama walivyokuwa wakifanya washirikina wa Kiarabu; na kwamba



mwenye kutaja jina la Mwenyezi Mungu kwa chinjo basi atakuwa amemwamini Mwenyezi Mungu na amemkanushia mshirika, Kwa vile atakuwa amemwelekea yeye tu peke yake.

**Mna nini hamli katika wale waliosomewa jina la Mwenyezi Mungu?**

Inaonyesha, kutokana na Aya hii, kwamba baadhi ya Waislamu walijizuilia kula chinjo ambalo limesomewa jina la Mwenyezi Mungu kwa kujitatiza; kwamba inakuwaje mtu achinje mnyama kwa mkono wake na ataje jina la Mwenyezi Mungu kisha ale na isijuzu kula mnyama aliyeuliwa na Mwenyezi Mungu ambaye amekufa mwenyewe!

Ndipo Mwenyezi Mungu akalipingia hilo kwa kusema: Mna nini hamli katika wale waliosomewa jina la Mwenyezi Mungu

**Na amewafanulia aliyowaharamishia isipokuwa vile mnavyolazimika.**

Kuhusu aliyowafanulia anakusudia wale aliowaishiria katika Aya 145, katika Sura hii, ambayo itakuja tafsir yake Inshaalah. Pia anaashiria wale waliotajwa katika Juz.2 (2:173).

Tumezungumzia kwa ufafanuzi kuhusu walioharamishwa na hukumu ya aliyelazimika katika Juz.2 (2:173).

**Na hakika wengi wanapoteza kwa matamano yao bila ya ilimu.**

Yaani wanahalalisha na kuharamisha kulingana na matamano yao bila ya dalili. Miongoni mwa hayo ni kuwa washirikina wa Kiarabu walihalalisha kula nyamafu na kuharamisha kula bahira, saiba, wasila na hami. Umetangulia ufafanuzi wa hayo katika Juz.6 (5:3).

**Hakika Mola wako anawajua vyema wanaoruka mipaka.**

Ambao wanahalalisha na kuharamisha kwa hawaa zao na matamano yao, Na kwamba atawaadhibu inavyostahiki.

**Na acheni dhambi zilizo dhahiri na zilizofichikana.**

Makusudio ya dhambi ni kitendo cha haramu kinacholeta dhambi; na dhahiri yake ni kufanya maasi dhahiri; na kufichikana ni kuyafanya kisiri. Mwenyezi Mungu amekataza kufanya maasi yote ya dhahiri na ya batini.

**Hakika wale wanaochuma dhambi watalipwa yale waliyokuwa wakiyachuma,** katika kufuata matamano bila ya elimu; wala hawataachwa bure bure bila ya hisabu na adhabu.

**Wala msile wale wasiosemea jina la Mwenyezi Mungu kwani huko ni ufasiki.**

Dhamiri ya huko inarudia kula, Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuhalalishia waliochinjwa kwa jina lake, anaharamisha ambao hawakutajiwa.

Kwa kutegemea hilo, ndipo mafakihi wote, isipokuwa Shafii, wamekonga- mana kuwa mchinjaji akiacha kutaja jina la Mwenyezi Mungu kwa makusudi, basi ni haramu; sawa na nyamafu. Inatosha jina la Mwenyezi Mungu tu, mfano: Allah, Allahu Akbar, Al-Hamdulillah, Bismillah, Lailaha illa Ilah na mfano wake.

Wametofautiana kuacha kusoma jina la Mwenyezi Mungu kwa kusahau. Hanafi, Jaafariya (Shia) na Hanbal wamesema si haramu nyama hiyo. Malik akasema ni haramu na Shafii amesema kuwa akiwacha kusoma jina la Mwenyezi Mungu kwa makusudi pia si haramu, sikwambii tena kusahau.

**Na hakika mashetani wanawafunza marafiki zao kubishana nanyi.**

Makusudio ya mashetani hapa ni maiblis-watu ambao wanauviringa ukweli na kutunga maneno wanayowahadalia wale wenye akili za juu juu. Kwa mafano, baadhi ya washirikana na maiblis wao walikuwa wakiwaambia wafuasi wao.

Waulizeni Masahaba wa Muhammad, vipi mnakula mnyama mliyemuua nyinyi wenyewe, kumchinja kwa mikono yenu; na wala hamli mnyama aliyeuawa na Mwenyezi Mungu, aliyekufa mwenyewe ambapo aliyeuawa na Mwenyezi Mungu ni bora kuliko mliyemuua nyinyi?

Huo ndio mjadala wao ambao mashetani waliwashauri marafiki zao kwa makusudio ya kuingiza shaka katika nyoyo dhaifu za baadhi ya Waislamu na kuwafitini na dini yao.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) akasema kuwaambia hawa wadhaifu:

**Na kama mkiwatii, hakika mtakuwa washirikina.**

Yaani mwenye kuwasikiliza washirikina na akahalalisha kula nyamafu, kama walivyohalalisha, basi yeye ni mshirikina kama wao, na hukumu hii haihusiki na kula nyamafu peke yake, bali kila anayepinga hukumu ya sharia akijua kuwa imethibiti, basi huyo ni kafiri.

أَوْ مَن كَانَ مَيِّتًا فَأَحْيَيْنَاهُ وَجَعَلْنَا لَهُ نُورًا يَمْشِي بِهِ فِي النَّاسِ كَمَن مَّثَلُهُ فِي الظُّلُمَاتِ لِي سَ  
بِخَارِجٍ مِّنْهَا ۚ كَذَلِكَ زُيِّنَ لِلْكَافِرِينَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢٢﴾

122. Je, aliyekuwa maiti kisha tukamhuisha na tukamjaalia nuru, hutembea mbele za watu kwayo, mfano wake ni kama yule aliyegizani asiyeweza kutoka humo? Namna hiyo wamepambiwa makafiri waliyokuwa wakiyafanya.

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا فِي كُلِّ قَرْيَةٍ أَكْبَرًا مَّجْرِمِيهَا لِيَمْكُرُوا فِيهَا ۗ وَمَا يَمْكُرُونَ إِلَّا بِأَنفُسِهِمْ وَمَا  
يَشْعُرُونَ ﴿١٢٣﴾

123. Na kama hivyo tumejaalia katika kila mji wakubwa wa wakosefu wake ili wafanye vitimbi humo; wala hawafanyii vitimbi isipokuwa wanajifanyia wenyewe, lakini hawatambui.

وَإِذَا جَاءَتْهُمْ آيَةٌ قَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ حَتَّى نُؤْتَىٰ مِثْلَ مَا أُوتِيَ رُسُلَ اللَّهِ ۗ اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ  
رِسَالَتَهُ ۗ سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللَّهِ وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا يَمْكُرُونَ ﴿١٢٤﴾

124. Na zinapowafikia ishara husema: Hatutaaamini mpaka tupewe sawa na yale waliyopewa Mitume wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi wa kujua mahali anapoweka ujumbe wake. Itawafika wale waliokosea dhila inayotoka kwa Mwenyezi Mungu na adhabu kali kwa sababu ya vitimbi walivyokuwa wakivifanya.

## **KUMHUISHA MAITI**

**Aya 122 – 124**

### **MAANA**

Je, aliyekuwa maiti kisha tukamhuisha na tukamjaalia nuru, hutembea mbele za watu kwayo, mfano wake ni kama yule gizani asiyeweza kutoka humo?

Huu ni mfano alioupiga Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kulinganisha baina ya mumin na kafiri. Ufafanuzi wake ni kuwa, kuwalinganisha wawili hao ni sawa na kulinganisha mauti na uhai. Na mwanga na giza. Kafiri ni

maiti akiamini hufufuliwa upya na kurudiwa na uhai na imani yake ni nuru anayokwenda nayo katika uhai wake.

Anayebakia kwenye ukafiri na shirki ni kama anajikokota gizani, anakwenda bila ya uongozi na haimfikii kheri yoyote katika maisha yake yote.

### **MWENYE KUULIZWA NA MUULIZAJI MKUU**

**Mtu anaweza kusema kuwa:** Aya imefananisha imani na uhai; na ukafiri na mauti; ingawaje makafiri na walahidi, katika zama hizi, wanaishi maisha ya anasa na wenye utajiri zaidi kuliko waumini na wenye kuabudu?

**Jibu:** Makusudio ya uhai katika Aya hii sio kuishi mtu katika neema na anasa, akawa anakula vizuri, kuvaa nguo za thamani na kunywa vinywaji vitamu. Hakika anasa hazihusiani na ukafiri wala imani. Kama ni hivyo waumini wa Mashariki na Magharibi wangelikuwa sawa katika maendeleo na uchumi mzuri, vilevile walahidi na makafiri.

Hali nzuri ya maisha ina sababu na mambo yanayoambatana nayo ambayo hayafungamani na chochote katika imani au ukafiri. Isipokuwa makusudio ya uhai, katika Aya hii, ni imani na hisia za kidini zinazompa mtu msukumo wa kutekeleza wajibu, akiwa ni mtu atakayeulizwa kuhusu mwenendo wake, atahisabiwa na kulipwa thawabu kwa wema wake, na adhabu kwa uovu wake.

Lau mtu angelikuwa si mwenye kuulizwa chochote, ingelikuwa sharia na kanuni ni maneno tu, yasiyokuwa na maana yoyote. Na tukipitisha kuwa mtu ataulizwa wala hataachwa bure bure, basi itatulazimu tupitische kwamba yeye ataulizwa mbele ya yule ambaye

﴿ لَا يُسْأَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْأَلُونَ ﴾

“Haulizwi anayoyafanya, na wao ndio wanaoulizwa” (21:23)

Lau muulizaji huyu anaulizwa, basi ingelipaswa kupatikana atakayemuuliza, na kuendelea hivyo hivyo bila mwisho.

Mwenye kukanusha kuweco muulizaji mkuu kabisa ambaye huuliza na haulizwi, basi atakuwa amekanusha maulizo; Kwa sababu hakuna maulizo bila ya muulizaji, Na mwenye kukanusha maulizo amekanusha maisha ya kijamii.

**Unaweza kusema:** Ndio mtu ataulizwa, lakini si lazima muulizaji awe Mwenyezi Mungu; watu wanaweza kuchagua kundi (kamati) ambalo litauliza watu.

Nasi tutauliza je kundi hilo likikosea, liulizwe na lihukumiwe na nani? Ikijibwa ni dhamir.

**Tutasema: Kwanza,** dhamir ni jambo la kimaana si la kidhati.

**Pili,** dhamiri anayo kila mtu, kwanini huyu aache dhamiri yake afuate ya mwingine?

Kwa hiyo, basi hakuna muulizaji asiyeulizwa ila Mwenyezi Mungu peke yake. Mwenye kumwamini Mwenyezi Mungu akailazimisha nafsi yake kufuata sharia za Mwenyezi Mungu na hukumu zake, basi atakuwa na busara ya mambo yake, itikadi yake na tabia zake. Vinginevyo atakuwa kama aliye gizani asiyeweza kutoka.

**Namna hiyo wamepambiwa makafiri waliyokuwa wakiyafanya.**

Yaani kama waliyovopambiwa waumini amali zao, vilevile washirikina wamepambiwa amali zao. Tofauti ni kuwa wao wamepambiwa kinyume na hali halisi, wamepambiwa, kimawazo na kinjozi tu.

**Na kama hivyo tumeajaalia katika kila mji wakubwa wa wakosefu wake.**

Makusudio ya mji ni kila jamii (mkusanyiko) wa watu, wachache au wengi. Maana ni kuwa: Ewe Muhammad kama ambavyo wanapatikana katika jamii yako viongozi wa waovu wanaofanya vitimbi na kuifanyia uadui dini ya Mwenyezi Mungu, vilevile katika jamii zilizotangulia walikuwapo; na hivi sasa pia wako viongozi wanaowafanyia vitimbi watu wao na kuwa katika msimamo wa kuifanyia uadui haki na wenye haki.

**Unaweza kuuliza:** Dhahiri ya Aya hii inafahamisha kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye aliyewafanya wakubwa kuwa waovu kwa watu wa haki, na tunajua kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu hukataza vitimbi na uovu; je, kuna taawili gani hapa?

**Jibu:** Makusudio ya kunasibishwa kwake huku Mwenyezi Mungu Mtukufu, ni kuashiria kwamba matakwa ya Mwenyezi Mungu yamepitisha kuwa desturi ya jamii iwe kwenye misingi ya kupingana baina ya wenye haki na wenye batili, baina ya viongozi wenye kufanya uadui na wenye kufanyiwa uadui.

Hakuna kimbilio la kuepuka mgongano huu ila kumalizwa waovu; na hapana budi kutimia hilo na kutukuka neno la haki mikononi mwa wanaolingania uadilifu na utengenevu; hata kama batili itakuwa kubwa kiasi gani. Hilo amelisajili Mwenyezi Mungu (s.w.t) katika Kitabu chake, aliposema:

﴿اَسْتِكْبَارًا فِي الْأَرْضِ وَمَكْرَ السَّيِّئِ وَلَا يَحِيقُ الْمَكْرُ السَّيِّئِ إِلَّا بِأَهْلِهِ فَهَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا سُنَّتِ الْأَوَّلِينَ فَلَنْ نَحْدِلَّ إِلَّا تَبْدِيلًا وَلَنْ نَجِدَ لِسُنَّتِ اللَّهِ تَبْدِيلًا﴾

“Na vitimbi vibaya havimpati ila yule aliyevifanya, Basi hawangoji ila desturi iliyokuwa kwa watu wa zamani, wala hutakuta mabadiiko katika desturi ya Mwenyezi Mungu, wala hutakuta mageuko katika desturi ya Mwenyezi Mungu.” (35:43)

Kukaririka huku ni kutilia mkazo kwamba mwisho ni wa wanaomcha Mwenyezi Mungu; kadiri zitakavyorefuka zama. Hivi ndivyo tunapata tafsiri ya kauli yake Mwenyezi Mungu:

Ili wafanye vitimbi humo; wala hawafanyii vitimbi isipokuwa wanajifanyia wenyewe, lakini hawatambui.

**Na zinapowafikia ishara husema: Hatutaaamini mpaka tupewe sawa na yale waliyopewa Mitume wa Mwenyezi Mungu.**

Wametofautiana wafasiri katika maana ya Aya hii kwa kauli mbili: Kwanza, kwamba wakubwa waovu katika Waarabu walimtaka Muhammad (s.a.w.w) awalettee muujiza kama aliopewa Musa, wa kupasua bahari; na wa Isa, wa kufufua wafu.

Kauli ya pili, ni kuwa wao walimwambia hatutakuamini mpaka utushushie wahyi kama ulivyowashukia Mitume. Razi akasema: “Hii ndio kauli mashuhuri baina ya wafasiri.”

Nasi tunaipa uzito kuliko ya kwanza; Kwa sababu mfumo wa Aya unafahamisha hivyo, ambapo Mwenyezi Mungu anawajibu wakubwa waovu kwa kauli yake:

Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi wa kujua mahali anapoweka ujumbe wake.

Kuongezea kuwa kutaka kwao Mwenyezi Mungu awateremshie Wahyi kunaafikiana na hasadi yao kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu amesema:

﴿ أَمْ يَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَىٰ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ ﴾

“Au wanawahusudu watu kwa alichowapa Mwenyezi Mungu katika fadhila yake?.” Juz.5 (4:54)

Katika Majmaul-bayan na kwengine, imeelezwa kuwa Walid bin Mughira alimwambia Mtume (s.a.w.w): **“Lau Utume ungelikuwa ni kweli mimi ningelistahiki zaidi kuliko wewe, kwa sababu mimi ni mkubwa kuliko wewe, na nina mali nyingi kushinda wewe.”**

Maana ya kauli yake Mwenyezi Mungu: ‘Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi wa kujua mahali anapoweka ujumbe wake’, ni kuwa yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu anauchagulia ujumbe wake mtu atakayefaa katika viumbe vyake, na Muhammad ni Mtukufu zaidi wa viumbe vya Mwenyezi Mungu na aheshimiwaye zaidi kwao.

**Itawafika wale waliokosea dhila inayotoka kwa Mwenyezi Mungu.**

Kwa sababu walijifanya wakubwa wakajiadhimisha, Ndipo wakastahiki malipo ya udhalilifu na fedheha. Kuna Hadith isemayo kuwa wenye kutakabari watafufuliwa katika Sura ya chembe (kama sisimizi) watakanyagwa na watu kwa nyayo zao, ikiwa ni malipo ya kujifanya kwao wakubwa katika dunia.

**Na adhabu kali kwa sababu ya vitimbi walivyokuwa wakivifanya.**

Udhalili ni malipo ya kiburi, na adhabu ni malipo ya vitimbi na hadaa. Kwa maneno mengine ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) anawafanyia wale wenye nia mbaya na malengo ya ufisadi kinyume cha wanavyokusudia na wanavyolenga.

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

فَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ أَنْ يَهْدِيَهُ يَشْرَحْ صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ ۗ وَمَنْ يُرِدْ أَنْ يُضِلَّهُ يَجْعَلْ صَدْرَهُ ضَيِّقًا حَرَجًا  
كَأَنَّمَا يَصَّعَّدُ فِي السَّمَاءِ ۗ كَذَلِكَ يَجْعَلُ اللَّهُ الرِّجْسَ عَلَى الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٢٥﴾

125. Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumwongoza humfungulia kifua chake Uislam; na yule anayetaka apotee hufanya kifua chake kina dhiki kimebana, Kama kwamba anapanda mbinguni. Namna hii anajaalia Mwenyezi Mungu adhabu juu ya wale wasioamini.

وَهَذَا صِرَاطٌ رَبِّكَ مُسْتَقِيمًا ۗ قَدْ فَصَّلْنَا الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَذَّكَّرُونَ ﴿١٢٦﴾

126. Na huu (Uislamu) ndio njia ya Mola wako iliyonyooka. Hakika tumezipambanua ishara kwa watu wenye kukumbuka.

لَهُمْ دَارُ السَّلَامِ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۗ وَهُوَ وَلِيُّهُمْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢٧﴾

127. Watapata nyumba ya salama kwa Mola wao naye ndiye walii wao, kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyatenda.

### HUMFUNGULIA KIFUA CHAKE UISLAM

Aya 125 – 127

#### MAANA

Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumwongoza humfungulia kifua chake Uislam; na yule anayetaka apotee hufanya kifua chake kinadhiki kimebana.

Anasema Razi: “Wameshikilia masahibu zetu -yaani Sunni Ashaira - Aya hii katika kubainisha kuwa upotevu na uongofu unatoka kwa Mwenyezi Mungu.” Ama masahibu zetu sisi- Shia - wanasema lau ingelikuwa upotevu na uongofu unatoka kwa Mwenyezi Mungu, basi kusingelikuwa na taklifu zozote na ingebatilika hisabu na malipo. Kwa sababu yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mwadilifu, hawezi kufanya jambo na kisha amhisabu mwingine kwalo. Itakuwaje hivyo na hali yeye ndiye aliyesema:

﴿ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ﴾

“Wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine” (6:164)

Ama Aya hii tuliyonayo haifahamishi madai ya Razi na masahibu zake; wa haikuja kubainisha chimbuko la upotevu na uongofu, au kwamba unatoka kwa Mwenyezi Mungu au mwinginewe; isipokuwa imekuja kubainisha kuwa watu ni makundi mawili:

Kundi la kwanza, ni wale ambao vifua vyao vitakunjukia haki, wataitumia na kuitegemea, kwa sababu ya mwamko wao, kujiepusha kwao na malengo ya kiutu na kujikomboa na kuiga na hawaa. Hao ndio wanaokusudiwa na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ الَّذِينَ يَسْتَمِعُونَ الْقَوْلَ فَيَتَّبِعُونَ أَحْسَنَهُ أُولَئِكَ الَّذِينَ هَدَاهُمُ اللَّهُ وَأُولَئِكَ هُمْ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴾

“Ambao husikia maneno wakafuata yaliyo mazuri yao, Hao ndio aliowaongowa Mwenyezi Mungu na hao ndio wenye akili” (39: 18)

Alipojua Mwenyezi Mungu (s.w.t) kheri kutoka katika kundi hili aliwazidishia uongofu na akawasaidia kwa tawfiki yake, akasema:

﴿ وَيَزِيدُ اللَّهُ الَّذِينَ اهْتَدَوْا هُدًى ﴾

“Na Mwenyezi Mungu huwazidishia uowongofu wale walioongoka...” (19:76).

Akasema tena:

﴿ وَالَّذِينَ اهْتَدَوْا زَادَهُمْ هُدًى وَآتَاهُمْ تَقْوَاهُمْ ﴾

“Na wale wanaofuata uongofu anawazidishia uongofu na huwapa takua yao.” (47:17).

Vilevile mwalimu humshughulikia na kumshujaisha mwanafunzi wake atakapojua kuwa ni mwerevu na mchangamfu.

Kundi la pili: Ni wale ambao vifua vyao haviikunjukii haki kwa ujinga wao na kuwa finyu fikra zao, au kwa kuwa haki inapingana na manufaa yao na faida zao au desturi zao na takilidi zao. Hawa ndio waliokusudiwa na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ فَوَيْلٌ لِلْقَاسِيَةِ قُلُوبُهُمْ مِّنْ ذِكْرِ اللَّهِ ﴾

“Basi ole wao wale wenye nyoyo ngumu kumkumbuka Mwenyezi Mungu ...” (39:22)

Na kauli yake:

﴿ مَا يَأْتِيهِمْ مِّنْ ذِكْرٍ مِّن رَّبِّهِمْ مُّحَدَّثٍ إِلَّا اسْتَمَعُوهُ وَهُمْ يَلْعَبُونَ ﴾

“Hayawafikii mawaidha mapya kutoka kwa Mola wao ila huyasikiza, na hali wanafanya mchezo” (21:2)

Na pia kauli yake:

﴿ وَلَوْ عَلِمَ اللَّهُ فِيهِمْ خَيْرًا لَّأَسْمَعَهُمْ وَلَوْ أَسْمَعَهُمْ لَتَوَلَّوْا وَهُمْ مُّعْرِضُونَ ﴾

“Na Mwenyezi Mungu angelijaalia wema wowote kwao angeliwasikilizisha, na lau angeliwasikilizisha wangelikengeuka wakapuuza” (8:23)

Kwa hiyo Mwenyezi Mungu (s.w.t) anaachana na mja na kumwacha ajitegemee mwenyewe, ikiwa haoni kheri yoyote kwake; kama ambavyo mwalimu anampuuza mwanafunzi wake baada ya kukata tamaa na kufaulu kwake. Angalia Juz.5 (4:88).

**Kama kwamba anapanda mbinguni.**

Zamani watu walikuwa wakipigia mfano wa mtu aliyelemewa kwa kupanda mbinguni, ambapo hakuna wasila wa kufika huko kwa hali yoyote. Mfananisho katika Aya unaafikiana na wakati ilipoteremka. Makusudio yake ni kwamba kundi la watu, ambalo ni kundi la pili tulilolielezea, linapata dhiki na uzito wakikalifishwa kufuata haki, sawa na kuamrisha kupanda mbinguni.

**Namna hii anajaalia Mwenyezi Mungu adhabu juu ya wale wasioamini.**

Neno Rijsi hapa lina maana ya adhabu. Maana ni kuwa wale wanaoona dhiki na tabu kufuata haki katika dunia, vilevile kesho wataingia katika adhabu ambayo ni kali na kubwa kuliko kufuata haki.

﴿ وَقَالُوا لَا تَنْفِرُوا فِي الْحَرِّ قُلْ نَارُ جَهَنَّمَ أَشَدُّ حَرًّا ﴾

“.... Wakasema msiende katika joto hili. Sema: Moto wa Jahanamu una joto zaidi ...” (9:81)

Na huu (Uislamu) ndio njia ya Mola wako iliyonyooka.

Huu, ni ishara ya Uislam ambao hukunjua nyoyo za wale wanaosikiliza kauli wakafuata mazuri yake. Na Uislamu ndio njia isiyo kombo.

Hakika tumezipambanua ishara kwa watu wenye kukumbuka.

Yaani, tumesimamisha dalili na hoja zilizo wazi zenye kutosheleza, juu ya kuswihi Uislamu na ukweli wake katika Qur'an na Aya zake. Kwa hoja hizo watanufaika wale ambao wanajua dalili za haki na kuzitumia.

Watapata nyumba ya salama kwa Mola wao.

Watakaokaa katika nyumba hii ya Mwenyezi Mungu hawatapatwa na uovu wowote wala hawatahuzunika, kwa sababu Mwenyezi Mungu ndiye anayewatunza naye ndiye walii wao kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyatenda miongoni mwa mambo ya kheri na twaa.

وَيَوْمَ يُحْشَرُهُمْ جَمِيعًا يَا مَعْشَرَ الْجِنِّ قَدِ اسْتَكْبَرْتُمْ مِنَ الْإِنسِ ۗ وَقَالَ أَوْلِيَاؤُهُمْ مِنَ الْإِنسِ رَبَّنَا اسْتَمْتَعَ بَعْضُنَا بِبَعْضٍ وَبَلَّغْنَا أَجَلَنَا الَّذِي أَجَلْتَ لَنَا ۗ قَالَ النَّارُ مَثْوَاكُمْ خَالِدِينَ فِيهَا إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ ۗ إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿١٢٨﴾

128. Na siku atakapowakusanya wote, (awaambie): Enyi makundi ya majini! Hakika nyinyi mmechukua wafuasi wengi katika watu, Na marafiki wao katika watu waseme: Mola wetu tulinufaishana sisi na wao, na tumefikia muda wetu uliotuwekea. Atasema: Moto ndio makazi yenu, mtadumu humo, ila apende Mwenyezi Mungu, Hakika Mola wako ndiye mwenye hekima, Mjuzi.

وَكَذَلِكَ نُؤَلِّي بَعْضَ الظَّالِمِينَ بَعْضًا بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٢٩﴾

129. Na kama hivi tunawatia mapenzi baadhi, wao kwa wao, kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

يَا مَعْشَرَ الْجِنِّ وَالْإِنسِ أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ يَقُصُّونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِي وَيُنذِرُونَكُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَذَا ۗ قَالُوا شَهِدْنَا عَلَىٰ أَنْفُسِنَا ۗ وَغَرَّتْهُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَشَهِدُوا عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ أَنَّهُمْ كَانُوا كَافِرِينَ ﴿١٣٠﴾

130. Enyi makundi ya majini na watu! Je, hawakuwafikia Mitume miongoni mwenu kuwasomea Aya zangu na kuwaonya kukutana na siku yenu hii? Watasema: Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu, Na yaliwadanganya maisha ya dunia, Nao watajishuhudia wenyewe kwamba wao walikuwa Makafiri.

ذَلِكَ أَنْ لَمْ يَكُنْ رَبُّكَ مُهْلِكَ الْفَرَىٰ بَطْلَمٍ وَأَهْلُهَا غَافِلُونَ ﴿١٣١﴾

131. Hayo ni kwa sababu ya kuwa Mola wako hakuwa ni mwenye kuiangamiza miji kwa dhulma na hali wenyewe wameghafilika.

وَلِكُلِّ دَرَجَاتٍ مِّمَّا عَمِلُوا ۗ وَمَا رَبُّكَ بِغَافِلٍ عَمَّا يَعْمَلُونَ ﴿١٣٢﴾

132. Na wote wana daraja mbali mbali kutokana na yale waliyoyatenda. Na Mola wako si mwenye kughafilika na yale wanayoyatenda.

## SIKU ATAKAPOWAKUSANYA WOTE

Aya 128 – 132



## MAANA

Na siku atakapowakusanya wote, yaani majini na watu, na awaambie: Enyi makundi ya majini! Hakika nyinyi mmechukua wafuasi wengi katika watu. Yaani kuwapoteza na kuwahadaa.

Na marafiki wao katika watu waseme; yaani wanadamu ambao wamemtawalisha shetani na kumtii, watasema kumwambia Mwenyezi Mungu: Mola wetu! Tulinufaishana sisi na wao. Yaani walinufaisha watu na watu wao wakawanufaisha majini. Razi amebainisha wajahi wa kunufaishana huko kwa kusema: “Watu walikuwa wakiwatii majini, kwa hiyo majini wakawa kama viongozi, Huku ndiko kunufaika majini. Ama kunufaika watu, ni kuwa majini walikuwa wakiwafahamisha watu aina za matamania na kuwafanyia sahali”

Na tumefikia muda wetu uliotuwekea.

Bado maneno yanaendelea ya watu waliowatii majini, Maana ni kuwa kunufaishana kwetu sisi kwa sisi kulikuwa kwa muda maalum na wakati uliopangwa – nao ni siku ile tulipouacha uhai wa dunia, Sasa tuko mbele yako tukikiri dhambi zetu, basi tuhukumu unavyotaka.

Atasema: Moto ndio makazi yenu, mtadumu humo, ila apende Mwenyezi Mungu.

Hii ndiyo hukumu ya sawa na malipo yenye kulingana.

Hakika Mola wako ndiye mwenye hekima, Mjuzi.

Hupitisha hukumu yake kwenye misingi ya hekima na ujuzi.

Na kama hivi tunawatia mapenzi baadhi wao kwa wao, kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) alipotaja katika Aya iliyotangulia (127) kuwa Yeye ndiye walii wa waumini, hapa anataja kuwa makafiri katika majini na watu baadhi yao ni marafiki wa wengine kwa sababu wao wanashirikiana katika kufuru na dhuluma, na siku ya Kiyama watakuwa washirika katika adhabu vilevile.

Enyi makundi ya majini na watu! Je, hawakuwafikia Mitume miongoni mweni kuwasomea Aya zangu na kuwaonya kukutana na siku yenu hii?

**Swali hili:** atalielekeza kesho Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa waovu katika majini na watu; nalo ni kulaumu na kukemea; sio kuwa Mwenyezi Mungu anataka kujua. Kwa sababu Mwenyezi Mungu anajua na wao wanajua kuwa Mwenyezi Mungu amewatumia Mitume watoaji bishara na waonyaji.

﴿ وَإِنْ مِنْ أُمَّةٍ إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ ﴾

“Na hakuna umma wowote ila alipita humo muonyaji” (35:24)

Watasema: Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu.

Kwa vile hakuna nafasi ya kukanusha hapa, Na mahali pengine aliwapa nafasi wakakadhibisha, Wakasema: “Wallahi, Mola wetu! Hatukuwa washirikina” kama ilivyoelezwa katika Aya 23 ya Sura hii.

Na yaliwadanganya maisha ya dunia.

Kwa sababu dunia haikuficha chochote katika mawaidha yake na mageuzi yake.

Nao watajishuhudia wenyewe kwamba wao walikuwa makafiri.

Kwanza Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja kuwa wao watasema: Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu, kisha akafuatishia kwa kusema kuwa wao watajishuhudia wenyewe.

Makusudio ya msisitizo huu ni makaripio ya ukafiri na maasia. Kwa sababu mwenye kujaribu kufanya dhambi akiwa na yakini kwamba yeye atalazimika kukiri, basi ataacha, ikiwa ana akili.

Hayo ni kwa sababu ya kuwa Mola wako hakuwa ni mwenye kuiangamiza miji kwa dhulma na hali wenyewe wameghafilika.

Hayo, ni hayo ya kupeleka Mitume. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu ni mwadilifu, hamdhulumu yeyote wala hamwadhibu ila baada ya kutuma Mitume watakaoamrisha mema na kukataza maovu. Kama mja hakuamrika na akakoma, basi ataambiwa na Mtume yatakayompata ikiwa hatatubu na kuacha. Akiendelea ataadhibiwa na Mwenyezi Mungu yale anayostahiki.

**Na wote wana daraja mbalimbali kutokana na yale waliyoyatenda.**

Waovu wana daraja kulingana na dhara zao, kunyonya jasho la wananchi na kutupa mabomu ya Atomic kwa maelfu ya watu. Na wema nao wana daraja kulingana na matendo yao, kuanzia mamkuzi mpaka kufa shahid katika njia ya haki na maslahi ya umma.

**Na Mola wako si mwenye kughafilika na yale wanayoyatenda.**

Kila kitu kimesajiliwa, kiwe kikubwa au kidogo, kizuri au kibaya. Si vibaya kurudia yale tuliyoyaeleza mara kwa mara, kwamba sisi tunaamini kiujumla kuweko majini, kwa sababu wahyi umethibtisha hilo na akili hailikanushi; sawa na kuhusu Malaika. Ama kuhusu ufafanuzi wao bado uko kwa Mwenyezi Mungu Mjuzi wa ghaibu.

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

وَرَبُّكَ الْغَنِيُّ ذُو الرَّحْمَةِ ۚ إِنَّ يَسْأَلُ بَعْضَكُمْ مِنْ بَعْضِكُمْ مَآ يَشَاءُ كَمَا أَنْشَأَكُمْ مِنْ

ذُرِّيَّةٍ قَوْمٍ آخَرِينَ ﴿١٣٣﴾

133. Na Mola wako ndiye Mkwasi, mwenye rehema, Akipenda atawaaondoa, na kuweka wengine awapendao baada yenu. Kama alivyowaanzisha kutokana na uzao wa watu wengine.

﴿١٣٤﴾ إِنَّ مَا تُوْعَدُونَ لَآتٍ ۖ وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ ﴿١٣٤﴾

134. Hakika mnayoahidiwa yatafika tu. Wala hamtaweza (kuepuka)

قُلْ يَا قَوْمِ اعْمَلُوا عَلَىٰ مَكَانَتِكُمْ إِنِّي عَامِلٌ ۖ فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ مَنْ تَكُونُ لَهُ عَاقِبَةُ الدَّارِ ۗ إِنَّهُ

لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿١٣٥﴾

135. Sema: Enyi watu wangu! Fanyeni vile muwezavyo; na mimi nafanya. Mtakujajua ni nani atakuwa na makazi mema mwishoni, Hakika madhalimu hawafaulu.

### NA MOLA WAKO NDIYE MKWASI

Aya 133 – 135

#### MAANA

Na Mola wako ndiye mkwasi, mwenye rehema.

Baada ya Mwenyezi Mungu kutaja kwamba atawahisabu watu kulingana na matendo yao. Ameashiria kuwa yeye ni mkwasi (mwenye kujitosheleza), hawahitajii viumbe.

Haimnufaishi twaa ya mwenye kumtii, wala hayamduru maasi ya mwenye kuasi; na kwamba ulimwengu wote una haja ya rehema yake; Kwa sababu, yeye ndiye sababu ya kwanza ya kupatikana huo ulimwengu.

Akipenda atawaaondoa kwa sababu ni Mkwasi, hawahitajii, na kuweka wengine awapendao baada yenu awabadili wengine wawe watiifu zaidi kuliko nyinyi. Lakini amewaacha na kuwapa muda kutokana na fadhila na ukarimu kutoka kwake.

**Kama alivyowaanzisha kutokana na uzao wa watu wengine.**

Yaani kama ambavyo imekuwa wepesi kwake kuwaleta nyinyi kutokana na kizazi kilichopita, vilevile ni wepesi kwake kuleta kizazi kipya kutokana na nyinyi na wengineo.

Makusudio ya Aya hii ni kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaonya makafiri, wenye inadi, na maangamivu, kama ilivyokuwa kwa kaumu ya Nuh <sup>(a.s)</sup>, A'd na Thamud.

**Hakika mnayoahidiwa yatafika tu.**

Baada ya Mwenyezi Mungu kuwahofisha na adhabu ya dunia, sasa anawahofisha na Kiyama na adhabu yake; kwamba Kiyama kitakuja bila ya shaka yoyote, wala hapana pa kukikimbia ila kwake yeye tu, peke yake.

Sema: Enyi watu wangu! Fanyeni vile muwezavyo; na mimi nafanya. Mtakujajua ni nani atakuwa na makazi mema mwishoni.

Baada ya Mtume (s.a.w.w) kuwalingania kwenye Uislamu waarabu wa ujahiliya na wakaitikia mwito wake walioitikia na kupinga waliopinga, Mwenyezi Mungu Mtukufu alimwamrisha kuwaambia wenye inadi: Kuweni kama mlivyo na mimi ninafanya kulingana na uongozi wa Mola wangu.

Baada ya muda mtajua mwisho mwema utakuwa wa nani; sawa na kumwambia yule anayepinga nasaha zako: Haya endelea tu utaona!

**Hakika madhalimu hawafaulu.**

Wale wanaojidhulumu wenyewe au wengineo kwa uadui. Lau angefaulu dhalimu, basi mwadilifu angelikuwa na hali mbaya kuliko dhalimu. Na maneno ya msimamo wa usawa yangelikuwa ni misamiati ya unafiki na ria.

وَجَعَلُوا لِلَّهِ مِمَّا ذَرَأَ مِنَ الْحَرْثِ وَالْأَنْعَامِ نَصِيبًا فَقَالُوا هَذَا لِلَّهِ بِرِعْمِهِمْ وَهَذَا لِشُرَكَائِنَا ۗ  
فَمَا كَانَ لِشُرَكَائِهِمْ فَلَا يَصِلُ إِلَى اللَّهِ ۗ وَمَا كَانَ لِلَّهِ فَهُوَ يَصِلُ إِلَى شُرَكَائِهِمْ ۗ سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ

﴿١٣٦﴾

136. Na wamemfanyia sehemu Mwenyezi Mungu katika mimea aliyoiumba na katika wanyama na kusema: hii ni ya Mwenyezi Mungu, kwa madai yao, na hii ni ya wale tunaowashirikisha. Basi vile walivyokusudia wale wanaowashirikisha, havifiki kwa Mwenyezi Mungu, na vilivyokuwa vya Mwenyezi Mungu huwafikia wanaowashirikisha, Ni mabaya kabisa wanayoyahukumu.

وَكَذَلِكَ زَيْنَ لِكَثِيرٍ مِنَ الْمُشْرِكِينَ قَتَلَ أَوْلَادَهُمْ شُرَكَائُهُمْ لِيُرِدُّوهُمْ وَلْيَلْبِسُوا عَلَيْهِمْ دِينَهُمْ ۗ  
وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا فَعَلُوهُ ۗ فَذَرْهُمْ وَمَا يَفْتَرُونَ ﴿١٣٧﴾

137. Namna hivi wanaowashirikisha wamewapambia wengi katika makafiri kuwaua watoto wao. Ili kuwaangamiza na kuwavu- rugia dini yao. Na kama Mwenyezi Mungu angependa wasingalifanya hayo. Basi waache na haya wanayoyazua.

وَقَالُوا هَذِهِ أَنْعَامٌ وَحَرْثٌ حِجْرٌ لَا يَطْعَمُهَا إِلَّا مَنْ نَشَاءُ بِرِعْمِهِمْ وَأَنْعَامٌ حُرِّمَتْ ظُهُورُهُمْ وَأَنْعَامٌ  
لَا يَذْكُرُونَ اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهَا افْتِرَاءً عَلَيْهِ ۗ سَيَجْزِيهِمْ بِمَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿١٣٨﴾

138. Na husema: Wanyama hawa na mimea hii ni mwiko, hawatokula ila wale tuwapendao - kwa madai yao (tu). Na wanyama wengine imeharamishwa migongo yao, Na wanyama wengine hawalitaji jina la Mwenyezi Mungu juu yao. Wanamzulia tu. Atawapa kwa hayo wanayomzulia.

وَقَالُوا مَا فِي بُطُونِ هَذِهِ الْأَنْعَامِ خَالِصَةٌ لِّذُكُورِنَا وَمُحَرَّمٌ عَلَىٰ أَرْوَاجِنَا ۗ وَإِن يَكُن مَّيْتَةً فَهُمْ  
فِيهِ شُرَكَاءُ ۗ سَيَجْزِيهِمْ وَصَفَهُمْ ۗ إِنَّهُ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿١٣٩﴾

139. Na husema: waliomo matumboni mwa wanyama hawa ni kwa ajili ya wanaume wetu tu, na wameharamishwa kwa wake zetu. Lakini ikiwa ni nyamafu hushirikiana. Atawalipa kwa maelezo yao. Hakika Yeye ni mwenye hekima, Mjuzi

قَدْ خَسِرَ الَّذِينَ قَتَلُوا أَوْلَادَهُمْ سَفَهًا بِغَيْرِ عِلْمٍ وَحَرَّمُوا مَا رَزَقَهُمُ اللَّهُ افْتِرَاءً عَلَى اللَّهِ ۗ قَدْ  
صَلُّوا وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿١٤٠﴾

140. Hakika wamehasirika wale waliowaua watoto wao kwa upumbavu bila ya elimu, Na wakaharamisha alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu Kwa

kumzulia Mwenyezi Mungu, Hakika wamepotea wala hawakuwa wenye kuongoka.

## **HUSEMA: HII NI SEHEMU YA MWENYEZI MUNGU**

**Aya 136 – 140**

### **MAANA**

Na wamemfanyia sehemu Mwenyezi Mungu katika mimea aliyoiumba na katika wanyama na kusema: hii ni ya Mwenyezi Mungu, kwa madai yao, na hii ni ya wale tunaowashirikisha. Basi vile walivyokusudia wale wanaowashirikisha, havifiki kwa Mwenyezi Mungu, na vilivyokuwa vya Mwenyezi Mungu huwafikia wanaowashirikisha, Ni mabaya kabisa wanayoyahukumu.

Dhamiri katika ‘wamemfanyia’ inawarudia washirikina wa kiarabu.

Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) baada ya kubatilisha itikadi ya washirikina, katika Aya zilizotangulia, kwa mantiki ya kiakili na kimaumbile, katika Aya hizi anaonyesha baadhi ya vile ambavyo washirikina walikuwa wakivitenga katika mali zao na watoto wao.

Aya hii tuliyonayo inaonyesha hali zao katika utajiri wao wa mali ambao ni kilimo na mifugo. Walikuwa, kama inavyoelezwa katika vitabu vya tafsiri, wakitenga sehemu katika mimea yao na mifugo kwa ajili ya Mungu na kuitoa kwa watoto na maskini. Na hutenga sehemu kwa ajili ya masanamu yao, na kuitoa kwa watunzaji na walinzi wa masanamu.

Walikuwa wakijitahidi kuzidisha fungu la masanamu, kuliko la Mwenyezi Mungu, ili litosheleze. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ni tajiri na masanamu ni mafakiri. Ikiwa kitu walichokifanya ni cha Mwenyezi Mungu kinachanganyika na kile walichokifanya cha masanamu, basi hukiachia masanamu. Na ikiwa kile walichokifanya ni cha masanamu kinachanganyika na kile walichokifanya ni cha Mwenyezi Mungu, hukirudisha kwa masanamu. Vilevile wakikumbwa na ukame walikuwa wakila fungu la Mwenyezi Mungu na kuacha fungu la masanamu. Huu ni ufafanuzi wazi wa “Ni mabaya kabisa wanayoyahukumu” katika kuyatanguliza masanamu yao kuliko Mwenyezi Mungu Mtukufu.

**Namna hivi wanaowashirikisha wamewapambia wengi katika makafiri kuwaua watoto wao.**

Yametangulia maelezo kuwa maana ya wanaowashirikisha katika Aya iliyopita kuwa ni masanamu. Ama katika Aya hii inakusudia makuhani na walinzi wa masanamu kulingana na hali ilivyo. Kwa sababu masanamu hayatambui wala hayasemi, basi yatawezeje kuwapambia na kuwahadaa. Maana ni kuwa washirikina kama waliyopiga mafungu mali zao kwa Mwenyezi Mungu na masanamu, vilevile makuhani na watunzaji wamewapambia kuwaua watoto wao.

**Unaweza kuuliza:** Matumizi ya washirikina katika mali zao na watoto wao, kwa namna iliyotangulia, yalikuwa ni kwa kutokana na desturi ya wakati wa ujahiliya. Inajulikana kuwa desturi huwekwa na watu. Mmoja wao alikuwa anaweza kuua mwanawe kwa kuogopa ufukara, au akimzika binti yake kwa kuogopa aibu; kama ilivyonasibishwa kwa Qais bin Asim aliyeigwa kwa ujinga. Sasa kuna wajihi gani katika kulinasibisha hilo kwa masanamu au wanaosimamia masanamu?

**Jibu:** Ni kweli kuwa matumizi ya washirikina yalitokana na desturi, lakini Makuhani na viongozi wao walipendekeza na kuipamba desturi hii, nao ndio wasemaji rasmi wa masanamu, kwa hiyo ikafaa kunasibishwa kwenye masanamu.

**Ili kuwaangamiza na kuwavurugia dini yao.**

Yaani Makuhani waliwapambia washirikina amali zao, ikawa natija ya kupambia huku ni kuangamia washirikina na kupotea kwao na haki na dini iliyonyooka.

**Na kama Mwenyezi Mungu angependa wasingalifanya hayo.**

Yaani kama Mwenyezi Mungu angelitaka kuwazuia hilo kwa nguvu wasingalifanya ubaya huo kwa mali zao na watoto wao, lakini amewaacha kama walivoyo baada ya kuwabainishia njia ya kheri na shari.

**Basi waache na haya wanayoyazua** ya kutegemeza kwa Mwenyezi Mungu yale wanayoyahalalisha na kuyaharamisha.

Amri ya kuwaacha na uzushi wao, imekuja kwa kuwakemea na kuwapa kiaga washirikina na sio kwa njia yake na uhakika wake; kama vile ilivyo amri katika kauli yake Mwenyezi Mungu:

﴿اعْمَلُوا مَا شِئْتُمْ إِنَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ﴾

**“Fanyeni mpendavyo, hakika yeye anayaona myafanyayo.”** (41:40)

Baada ya hapo Mwenyezi Mungu anataja katika Aya inayofuatia kwamba washirikina waligawanya mavuno yao na mifugo yao mafungu matatu:

1. Fungu la kwanza: **Na husema: Wanyama hawa na mimea hii ni mwiko, hawatokula ila wale tuwapendao - kwa madai yao (tu).** Yaani washirikina walikuwa wakigawa sehemu ya mazao na mifugo na kukataza kutumiwa ila kwa wanaowachagua. Mwenyezi Mungu (s.w.t.) hakubainisha hao waliochaguliwa na washirikina. Lakini baadhi ya wafasiri wamesema, ni makuhani na watumishi wa masanamu. Wengine wakasema ni wanaume tu, sio wanawake.

2. Fungu la pili: **Na wanyama wengine imeharamishwa migongo yao, hawapandwi wala kubebeshwa mizigo.** Rejea maelezo katika Juz.7 (5:103).

3. Fungu la tatu: **Na wanyama wengine hawalitaji jina la Mwenyezi Mungu juu yao** wakati wa kuchinja, bali wanataja majina ya waungu wao.

Umetangulia ufafanuzi katika kusafiri Sura hii, Aya ya 121, kuwa wao wamemnasibishia Mwenyezi Mungu kugawanya huku kwa uwongo na uzushi na Mwenyezi Mungu atawaadhibu.

**Na husema: waliomo matumboni mwa wanyama hawa ni kwa ajili ya wanaume wetu tu, na wameharamishwa kwa wake zetu. Lakini ikiwa ni nyamafu hushirikiana. Atawalipa kwa maelezo yao. Hakika yeye ni mwenye hekima, Mjuzi.**

Razi amesema: “Hii ni aina ya nne katika mambo yao maovu. Walikuwa wakisema katika mimba za Bahira na Saiba: “atakayezaliwa hai basi atahusu wanaume tu, hawali wanawake, na atakayezaliwa maiti basi watashirikiana kumla wanaume na wanawake.” **Watalipwa maelezo yao.**

Na makusudio ya kiaga cha kuwa. **Hakika yeye ni mwenye hekima, Mjuzi, ni makemeo yawe kwenye hekima na kwa mujibu wa inavyostahiki.”**

**Hakika wamehasirika wale waliowaua watoto wao kwa upumbavu bila ya elimu.**

Kuna upumbavu gani zaidi ya mzazi kumchinja mwanawe kwa mkono wake au kumzika mzima. Kauli yake Mwenyezi Mungu bila ya elimu ni kusisitiza upumbavu wao. Ama hasara yao katika dunia ni kule kuua watoto wao na uufisadi wa maisha yao ya kijamii. Na hasara yao katika akhera ndiyo nzito na chungu.

Na wakaharamisha alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu katika wanyama na mazao ambayo wamedai kuwa ni mwiko.

Kwa kumzulia Mwenyezi Mungu.

Kwa sababu kuharamisha kunatokana na wao na wala sio kutoka kwake Mwenyezi Mungu.

Hakika wamepotea wala hawakuwa wenye kuongoka kwenye kheri yoyote na uwongofu.

Razi anasema: “Mwenyezi Mungu ametaja mambo saba na kila moja kati hayo ni sababu tosha ya kupatikana shutuma. Nayo ni: Kupata hasara, upumbavu, ujinga, kuharamisha aliyoyahalalisha Mwenyezi Mungu, kumzulia Mungu, upotevu na kuacha kuongoka.”

Kisha akaendelea kusema Razi: “Imethibiti kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu amewashutumu wanaowaua watoto na kuharamisha aliyohalalisha Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa sifa hizi saba zenye kuwajibisha aina kubwa na ya mwisho ya shutuma, na huo ni ufasaha wa hali ya juu.”

Nasi tunamwambia Razi: Ikiwa Mwenyezi Mungu amewashutumu kwa upotevu kuwa ndiyo aina kubwa na ya mwisho ya shutuma, sasa vipi wewe unadai kuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyewapoteza? Ni mantiki gani yanayosema kuwa inafaa asiye na hatia kuadhibiwa na kushutumiwa kwa kitendo ambacho amekifanya yule anayeshutumu na kuadhibu?

Hayo Razi ameyasema mara kadhaa katika tafsir yake Al-Kabir, miongoni mwayo ni yale aliyoyasema karibuni katika kufasiri Aya 125 ya Sura hii.

وَهُوَ الَّذِي أَنْشَأَ جَنَّاتٍ مَّعْرُوشَاتٍ وَغَيْرِ مَعْرُوشَاتٍ وَالنَّخْلَ وَالزَّرْعَ مُخْتَلِفًا أُكُلُهُ وَالزَّيْتُونَ  
 وَالرَّمَانَ مُمْتَشَابِهًا وَغَيْرِ مُتَشَابِهٍ ۗ كُلُوا مِنْ ثَمَرِهِ إِذَا أَثْمَرَ وَآتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ ۗ وَلَا تَسْرِفُوا ۗ  
 إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ ﴿١٤١﴾

141. Naye ndiye aliyeyumba bustani zenye kutambaa na zisizotambaa na mitende na mimea yenye kutofautiana uliwaji wake. Na mizaituni na mikomamanga. Inayofanana na isiyofanana, Kuleni matunda yake inapozaa, Na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake, Wala msifanye ufujaji, hakika Yeye hawapendi wafujaji.

وَمِنَ الْأَنْعَامِ حَمُولَةً وَفَرْشًا ۗ كُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُواتِ الشَّيْطَانِ ۗ إِنَّهُ  
 لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿١٤٢﴾

142. Na katika wanyama wale wabebao na wa kutoa matandiko. Kuleni katika alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu, wala msifuate nyayo za Shetani; hakika yeye ni adui yenu dhahiri.

ثَمَانِيَةَ أَزْوَاجٍ ۗ مِنَ الضَّأْنِ اثْنَيْنِ وَمِنَ الْمَعْزِ اثْنَيْنِ ۗ قُلْ آلذَّكَرَيْنِ حَرَّمَ أَمِ الْأُنثَيَيْنِ أ ۗ مَا  
 اشْتَمَلَتْ عَلَيْهِ أَرْحَامُ الْأُنثَيَيْنِ ۗ نَبِّئُونِي بِعِلْمٍ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٤٣﴾

143. Namna nane za madume na majike: wawili katika kondoo dume na jike na wawili katika mbuzi dume na jike. Sema je, ameharamisha madume mawili au majike mawili, au waliomo matumboni mwa majike mawili, niambieni kwa ilimu ikiwa nyinyi mnasema kweli.

وَمِنَ الْإِبِلِ اثْنَيْنِ وَمِنَ الْبَقَرِ اثْنَيْنِ ۗ قُلْ آلذَّكَرَيْنِ حَرَّمَ أَمَ الْأُنثَيَيْنِ أَمَّا اشْتَمَلَتْ عَلَيْهِ أَرْحَامٌ الْأُنثَيَيْنِ ۗ أَمْ كُنْتُمْ شُهَدَاءَ إِذْ وَصَّاكُمُ اللَّهُ بِهَذَا ۗ فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا لِيُضِلَّ النَّاسَ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٤٤﴾

144. Na wawili katika ngamia na wawili katika ng'ombe, Sema je, ameharamisha madume mawili au majike mawili, au waliomo matumboni mwa majike mawili? Au nyinyi mlikuweko Mwenyezi Mungu alipowausieni haya? Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo ili kuwapoteza watu bila ya ilimu? Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu.

## KULENI MATUNDA YAKE

Aya 141 – 144

### MAANA

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kubainisha katika Aya zilizotangulia, waliyoharamisha katika kilimo na mifugo kwa uzushi, amebainisha katika Aya hizi kwamba yeye ameumba mimea na wanyama binadmau anufaike nayo.

Anasema Mtukufu wa Wasemaji:

Naye ndiye aliyeumba bustani zenye kutambaa inayowekwa matawi yake katika chanja na zisizotambaa na mitende na mimea inaungana na Bustani katika upande wa kuunganisha mahsus kutoka ujumla.

Yenye kutofautiana uliwaji wake.

Nafaka ziko aina nyingi na kila moja ina aina yake, na kila aina ina ladha yake. Matunda nayo yako aina kwa aina; yenye rangi tofauti, ladha na hata harufu, vilevile mboga.

Na mizaituni na mikomamanga.

Hiyo pia inaungana na bustani.

Inayofanana na isiyofanana.

Matunda ya mikomamanga yanafanana, lakini kuna yaliyo tamu na yaliyo ugwadu. Vilevile matunda ya jamii ya malimau na mizaituni; kuna mazuri na mabaya.

Kuleni matunda yake inapozaa.

Kwa sababu imeumbwa kwa ajili yenu.

Na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake.

Imesemekana kuwa makusudio ya haki yake ni Zaka. Wengine wakasema kuwa ni sadaka ya Sunna. Lakini, kauli zote mbili ni kinyume na dhahiri.

Linalokuja haraka kwenye akili ni kukusanywa na wala yasiachwe yakaharibika na kupotea.

Wala msifanye ufujaji, hakika Yeye hawapendi wafujaji.

Ufujaji (Israf) ni kupetuka kiwango, na Mwenyezi Mungu amelikataza hilo: ni sawa iwe ni kutumia mtu mwenyewe, au kumpa mwingine.



Na katika wanyama wale wabebao na wa kutoa matandiko.

Yaani ameumba katika wanyama wanaowabeba nyinyi na kubeba mizigo yenu; kama vile ngamia. Na wale mnaowachinja na kunufaika kwa nyama yake manyoya na sufi zake.

Kuleni katika alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu,

kama vile wanyama hawa na wengineo na mshukuru neema zake.

Wala msifuate nyayo za Shetani, kwa kuhalalisha aliyoyaharamisha Mwenyezi Mungu, na kuharamisha aliyoyahalalisha, na pia kufanya ubadhirifu.

Hakika yeye ni adui yenu dhahiri.

Anawaamrisha uovu na kusema kwa Mwenyezi Mungu msiyoyajua.

Namna nane za madume na majike: wawili katika kondoo dume na jike na wawili katika mbuzi dume na jike. Sema je, ameharamisha madume mawili ya kondoo na mbuzi au majike mawili, ya kondoo na mbuzi? Au waliomo matumboni mwa majike mawili ya kondoo na mbuzi?

Niambieni kwa ilimu ikiwa nyinyi mnasema kweli sio kwa hawa za nafsi na kufuata mnavyoambiwa tu, kwa sababu kuharamisha kunahitajia dalili mkato; sasa je, iko wapi?

Na wawili katika ngamia na wawili katika ng'ombe, Sema je, ameharamisha madume mawili au majike mawili, au waliomo matumboni mwa majike mawili? Au nyinyi mlikuweko Mwenyezi Mungu alipowausieni haya?

Walidai kwamba Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaharamishia waliowaharamisha katika wanyama na mimea. Ndipo akawaambia kuwa jambo halithibitiki ila kwa mojawapo ya hali mbili. Ama kwa kuona au kwa kushuhudia shahidi mkweli. Na nyinyi hamkupata hukumu ya uharamu kutoka kwa Mwenyezi Mungu moja kwa moja au kupitia kwa Mtume wake; basi mmezitoa wapi hukumu hizi?

Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo?

Ikiwa hamkuona, wala hakuna ushahidi wowote, basi nyinyi mtakuwa wazushi. Na mzushi ni dhalimu mwenye dhambi. Bali nyinyi ni madhalimu kuliko dhalimu yeyote, kwa sababu mnamzulia Mwenyezi Mungu uwongo.

Ili kuwapoteza watu bila ya ilimu.

Akiwazuia kufuata njia ya Mwenyezi Mungu na wakati huo huo anadai kuwa yeye ni kiongozi wa dini ya Mwenyezi Mungu; kama walivyo masheikh wengi siku hizi.

Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu.

Kwa sababu wao wamekata uhusiano na Mwenyezi Mungu. Isitoshe wameharamisha aliyoyahalalisha na kuhalalisha aliyoyaharamisha.

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

قُلْ لَا أَجِدُ فِي مَا أُوحِيَ إِلَيَّ مُحَرَّمًا عَلَى طَاعِمٍ يَطْعَمُهُ إِلَّا أَنْ يَكُونَ مَيْتَةً أَوْ دَمًا مَسْفُوحًا أَوْ لَحْمَ  
خِنزِيرٍ فَإِنَّهُ رِجْسٌ أَوْ فِسْقًا أُهْلًا لِغَيْرِ اللَّهِ بِهِ ۚ فَمَنِ اضْطُرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَلَا عَادٍ فَإِنَّ رَبَّكَ غَفُورٌ  
رَّحِيمٌ ﴿١٤٥﴾

145. Sema: Sioni katika niliyopewa wahyi kilichoharamishiwa mlaji kukila isipokuwa kiwe ni mzoga au damu inayomwagika au nyama ya nguruwe, kwani hivyo ni uchafu; au kwa uharamu, kimetajiwa jina la asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Lakini aliyefikwa na dharura bila ya kutamani wala kupita kiasi, basi Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghufira, mweye kurehemu.

وَعَلَى الَّذِينَ هَادُوا حَرَّمْنَا كُلَّ ذِي ظُفْرٍ ۖ وَمِنَ الْبَقَرِ وَالْغَنَمِ حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ شُحُومَهُمَا إِلَّا مِمَّا  
حَمَلَتْ ظُهُورُهُمَا أَوْ الْحَوَايَا أَوْ مَا اخْتَلَطَ بِعَظْمٍ ۚ ذَلِكَ جَزَيْنَاهُمْ بِبَعْضِهِمْ ۗ وَإِنَّا لَصَادِقُونَ ﴿١٤٦﴾

146. Na kwa wale walio mayahudi tuliharamisha kila mwenye kucha. Na katika ng'ombe na mbuzi na kondoo tukawaharamishia mafuta yao; isipokuwa yale iliyobeba migongo yao, au matumbo, au iliyochanganyika na mifupa. Tuliwalipa hivyo kwa sababu ya uasi wao, Na hakika sisi ndio wakweli.

فَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقُلْ رَبُّكُمْ ذُو رَحْمَةٍ وَاسِعَةٍ وَلَا يُرَدُّ بَأْسُهُ عَنِ الْقَوْمِ الْمُجْرِمِينَ ﴿١٤٧﴾

147. Wakikukadhibisha, basi sema: Mola wenu ana rehema nyingi; wala adhabu yake haizuliwi kwa watu waovu.

### SIONI KATIKA NILIYOPEWA WAHYI

**Aya 145 – 147**

#### MAANA

Sema: Sioni katika niliyopewa wahyi kilichoharamishiwa mlaji kukila isipokuwa kiwe ni mzoga au damu inayomwagika au nyama ya nguruwe, kwani hivyo ni uchafu; au kwa uharamu, kimetajiwa jina la asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Lakini aliyefikwa na dharura bila ya kutamani wala kupita kiasi, basi Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghufira, mwenye kurehemu.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kubainisha uzushi wa washirikina kwa Mwenyezi Mungu, katika vyakula walivyoharamisha na kuhalalisha, kati- ka Aya hii anabainisha vilivyoharamishwa na Mwenyezi Mungu kuliwa.

Navyo ni vinne: Mfu, damu yenye kutirizika, nyama ya nguruwe na kilichotajiwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu; yaani aliyechinjwa kwa jina la asiyekuwa Mwenyezi Mungu.

Haifai kwa yeyote kula chochote katika hivyo ila akiwa amelazimika; katika hali hiyo anaruhusiwa kula kiasi kile kitakachoweza kuzuia madhara ya nafsi yake tu. Umetangulia ufafanuzi wa hayo katika kufasiri Juz.2 (2:173) Huko tumejibu swali la mwenye kuuliza, kuwa inaonyesha vilivyo

haramu ni hivi vinne tu, lakini tunaalezewa vingi, Vilevile umetangulia ufafanuzi zaidi katika Juz.6 (5:3).

**Na kwa wale walio Mayahudi tuliharamisha kila mwenye kucha.**

Katika Aya iliyotangulia, Mwenyezi Mungu ameharamisha aina zilizotajwa kwa watu wote, Mayahudi na wasiokuwa Mayahudi. Ama vilivyoharamishwa, katika Aya hii, vinawahusu Mayahudi tu, kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu: “Na kwa wale walio Mayahudi tuliharamisha:

**Kwanza:** ni, kila mwenye kucha; yaani wote wenye kucha bila ya kuacha wengine. Tabari katika Tafsir yake anasema: “Mwenye kucha katika wanyama na ndege ni ambaye vidole vyake havikuachana; kama vile ngamia, mbuni na bata.”

**Pili:** Na katika ng’ombe na mbuzi na kondoo tukawaharmishia mafuta yao.

Mwenyezi Mungu hakuwaharamishia sehemu yote ya nyama ya ng’ombe na mbuzi na kondoo,ispokuwa nyama nyeupe tu sio nyekundu. Na pia katika hiyo amevua kwa kusema:

**Isipokuwa yale iliyobeba migongo yao.**

Yaani mafuta yaliyogandana na mgongo.

**Au matumbo** yaani mafuta yanayogandamana na utumbo.

**Au iliyochanganyika na mifupa** nayo ni mafuta ya mkia kulingana na wafasiri wote waliokuwako wakati wa Razi. Na mfupa uliochanganyika na na mafuta ya mkia ni kifandugu.

**Tuliwalipa hivyo kwa sababu ya uasi wao, Na hakika sisi ndio wakweli.**

Hii ni kubainisha sababu ya kuharamishiwa mayahudi vitu hivi vizuri, na kwamba hivyo ni malipo ya makosa yao yasiyo na idadi, yakiwemo kuua mitume, kula mali za watu kwa batili, kusema kwao mikono ya Mwenyezi Mungu imefumba na mengineyo. Tazama Juz.4 (3:93).

**Wakikukadhibisha, basi sema: Mola wenu ana rehema nyingi; na adhabu yake haizuiliwi (kuwafikia) watu waovu.**

Yaani wakikukadhibisha Ewe Muhammad, basi usiwakatishe tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu na uwaambie kuwa mkitubia, basi Mwenyezi Mungu atawakubali na atawasamehe; kama ambavyo atawaadhibu mkiendelea na mliyo nayo.

Katika Aya hii kuna ahadi na kiaga kikali. vilevile radhi ya Mwenyezi Mungu na ghadhabu yake: Radhi yake ni kwa atakayekimbilia kwake akitaka msamaha na ghadhabu yake ni kwa atakayeendelea na uasi. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿لَئِنْ شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ وَلَئِنْ كَفَرْتُمْ إِنَّ عَذَابِي لَشَدِيدٌ﴾

“Mkishukuru, nitawazidishia; na mkikufuru (jueni) kuwa adhabu yangu ni kali” (14:7)

سَيَقُولُ الَّذِينَ أَشْرَكُوا لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَشْرَكْنَا وَلَا آبَاؤُنَا وَلَا حَرَمْنَا مِنْ شَيْءٍ ۚ كَذَلِكَ كَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ حَتَّىٰ ذَاقُوا بَأْسَنَا ۗ قُلْ هَلْ عِنْدَكُمْ مِنْ عِلْمٍ فَتُخْرِجُوهُ لَنَا ۗ إِن تَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ أَنْتُمْ إِلَّا تَخْرُصُونَ ﴿١٤٨﴾

148. Watasema walioshirikisha: Lau angelitaka Mwenyezi Mungu tusingelimshirikisha sisi wala baba zetu; wala tusingeliharamisha chochote. Kama hivi walikadhibisha waliokuwa kabla yao mpaka wakaonja adhabu

yetu, Je, mnayo elimu mtutolee? Nyinyi hamfuati ila dhana tu, na hamsemi ila uwongo tu.

قُلْ فَلِلَّهِ الْحُجَّةُ الْبَالِغَةُ ۗ فَلَوْ شَاءَ لَهَدَاكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٤٩﴾

149. Sema: Basi Mwenyezi Mungu ndiye mwenye hoja ikomeshayo, Na kama angelitaka angeliwaongoza nyote.

قُلْ هَلْ مَسَّ شُهَدَاءَكُمْ الَّذِينَ يَشْهَدُونَ أَنَّ اللَّهَ حَرَّمَ هَذَا ۗ فَإِنْ شَهِدُوا فَلَا تَشْهَدُ مَعَهُمْ ۗ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ وَهُمْ يَرِبُّهُمْ يُعَدِّلُونَ ﴿١٥٠﴾

150. Sema: Leteni mashahidi wenu wanaoweza kushuhudia kuwa Mwenyezi Mungu ameharamisha haya, Basi wakitoa ushahidi, wewe usishuhudie pamoja nao. Wala usifuate matamanio ya wale waliozikadhibisha ishara zetu na wale wasioamini Akhera, na ambao humlinganisha Mola wao.

## ANGELITAKA MWENYEZI MUNGU TUSINGELISHIRIKISHA

Aya 148 – 150

### MAANA

Watasema walioshirikisha: Lau angelitaka Mwenyezi Mungu tusingelimshirikisha sisi wala baba zetu; wala tusingeliharamisha chochote.

Wanaokubali nasaha na kufuata kauli nzuri ni wachache sana; na wanaokubali makosa yao ni wachache zaidi. Kwani wengi wanaona makosa yao ndiyo mambo bora na maovu yao kuwa ni mema.

﴿كَذَلِكَ زَيْنٌ لِّلْمُسْرِفِينَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾

“... Namna hii wamepambiwa wale wapitao mipaka yale waliyokuwa wakiyatenda,” (10:12).

Wanaposhindwa kuboresha uovu wao wanajivua na kusema kuwa ni matakwa ya Mwenyezi Mungu au sababu yoyote nyingine.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametakata na hayo wanayomsifu nayo. Yeye anawaamrisha na kuwakataza, na kuwafanya wawe na hiyari katika wanayoyafanya na kuyaacha. Ili aangamie mwenye kuangamia kwa dalili zilizo dhahiri na apone yule atakayepona kwa dalili zilizo dhahiri. Wala hakuna yeyote mwenye mamlaka kwa mwingine; hata shetani atasema siku itakapokatwa hukumu:

﴿إِنَّ اللَّهَ وَعَدَكُمْ وَعَدَ الْحَقِّ وَوَعَدْتَكُمْ فَأَخْلَفْتُمْ وَمَا كَانَ لِي عَلَيْكُمْ مِّنْ سُلْطَانٍ إِلَّا أَن دَعَوْتُكُمْ فَاسْتَجَبْتُمْ لِي فَلَا تَلُومُونِي وَلُومُوا أَنفُسَكُمْ﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu aliwaahidi ahadi ya kweli, nami nikawaahidi, lakini sikuwatimizia, Wala sikuwa na mamlaka juu yenu isipokuwa niliwaita tu, nanyi mkaniitikia. Basi msinilaumu, bali jilaumuni wenyewe ... (14:22).

Katika Aya hii tuliyonayo, Mwenyezi Mungu anasimulia madai ya washirikina kuwa shirki yao na shirk ya mababa zao na kuharamisha kwao mimea na wanyama, ilitokana na matakwa ya Mwenyezi Mungu na amri yake. Lau angelitaka wasishirikishe angeliwazuia na shirk.

**Kama hivi walikadhibisha waliokuwa kabla yao mpaka wakaonja adhabu yetu.**

Yaani washirikina wa Kiarabu walimkadhibisha Muhammad (s.a.w.w), aliyewakataza ushirikina na kumzulia Mwenyezi Mungu uwongo; sawa na walivyokadhabisha Mitume wale waliokuwa kabla yao; na hawakuwasadiki mpaka baada ya kuteremshiwa adhabu ya malipo ya kukadhibisha kwao.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kusimulia madai ya washirikina, na mababu zao, alimwamrisha Mtume wake kuwajibu kwa swali litakalowazima na kubatilisha madai yao nalo ni:

**Je, mnayo elimu mtutolee?**

Makusudio ya elimu hapa ni dalili. Hiyo ni katika kutumia chenye kusababisha kuwa ndio sababu; Kwa sababu dalili ndiyo sababu ya kupatikana elimu.

Makusudio ya swali hili ni kudhihirisha uwongo wao na kushindwa kwao.

Kwa sababu maana yake ni kuwa nyinyi washirikina! Mmedai shirk ilikuwa ni kwa kuridhia kwake Mwenyezi Mungu; sasa ni nani basi aliyewaambia haya?

Kutoka wapi mmejua matakwa yake Mwenyezi Mungu Mtukufu? Hiyo ni katika siri zake Mwenyezi Mungu wala hamdihirishii siri yake ila Mtume wake aliyemridhia, Na Mtume hakuwaambia haya nyinyi wala wengineo, Kwa hiyo vipi mnafanyia hila Mwenyezi Mungu?

**Nyinyi hamfuati ila dhana tu, na hamsemi ila uwongo tu.**

Sisi hatuna shaka kwamba wakubwa wa waasi wanajua kuwa wao ni waongo katika wanayoyasema; isipokuwa wanaysema kwa kuifanyia inadi haki ambayo inaipomosha batili yao na kumaliza malengo yao na matendo yao ya uadui.

**Sema: Basi Mwenyezi Mungu ndiye mwenye hoja ikomeshayo.**

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amebainisha katika Aya iliyotangulia kuwa washirikina hawana hoja ya madai yao isipokuwa dhana na uwongo. Katika Aya hii amebainisha kuwa hoja inayokomesha ni ya Mwenyezi Mungu pekee yake, juu yao na juu ya wengine. Maana ya kuwa inakomesha ni kwamba ina nguvu ya kukomesha nyudhuru zote.

**Na kama angelitaka angeliwaongoza nyote.**

Katika kufasiri Juz.1 (2: 26), tumetaja kuwa Mwenyezi Mungu ana matakwa mawili: Matakwa ya kuumba ambayo yanakuwa katika ibara yake “Kuwa na ikawa” (kun fayakun) na Matakwa ya kuweka sharia, ambayo ni amri zake na makatazo yake.

Na Yeye Mwenyezi Mungu (s.w.t) anaumba ulimwengu kwa matakwa yake ya kuumba na hajiingizikama sikosei - katika matakwa haya kwenye mambo ya watu ya kijamii; bali huweka sharia na mwongozo.

Maelezo haya ndiyo yanatufafanulia maana ya kauli yake: **‘Na kama angelitaka angeliwaongoza nyote;** Yaani lau angelitaka kujiingiza katika mambo yenu ya kijamii kwa matakwa ya neno “Kuwa ikawa” (ya kuumba), basi mngeliamini nyote, Lakini yeye hafanyi hivyo. Kwa sababu lau angelifanya hivyo ingelibatilika taklifu na kusingekuwapo thawabu na adhabu.

Tunarudia kusema tena kuwa washirikina walidai kuwa shirki yao ilikuwa kwa matakwa ya Mwenyezi Mungu, ndipo Mwenyezi Mungu (s.w.t) aka- batilisha madai yao haya kuwa ni madai yasiyo na dalili. Kwa sababu Mwenyezi Mungu hajiingizi katika mambo ya watu kwa matakwa ya kuumba.

Lau tukichukulia kuwa Mwenyezi Mungu anajiingiza katika mambo hayo, basi kwa hali ilivyo angeliwaelekeza kwenye imani ya umoja wake na sio kwenye uasi, ukafiri na ushirikina.

**Sema: Leteni mashahidi wenu wanaoweza kushuhudia kuwa Mwenyezi Mungu ameharamisha haya.**

Washirikina walimzulia Mwenyezi Mungu uwongo katika kuharamisha waliyoyaharamisha katika mimea na wanyama; vilevile walimzulia katika kunasibisha shirki yao kwake. Ndipo Mwenyezi Mungu akamwamrisha Mtume wake Muhammad, katika Aya ya kwanza, kuwambia kuwa kama wanayo dalili waitoe.

Katika Aya ya pili akamwamrisha kuuwambia kuwa dalili mkataa ni ya Mwenyezi Mungu tu, si yenu. Kisha katika Aya hii amemwamrisha kuwambia nionyeshe ni anayeshuhudia kuwa Mwenyezi Mungu amewapa wahyi moja kwa moja au kupitia kwa Mtume miongoni mwa Mitume yake kuwa yeye ameharamisha mliyoyaharamisha. Kwa sababu kushuhudia haki kuna sharti la kuweko elimu yenye kuondoa shaka na dhana. Wala hakuna nyenzo ya kujua yaliyoharamishwa na yaliyohalalishwa ila Wahyi tu; basi mleteni atakeylishuhudia hilo.

**Basi wakitoa ushahidi, wewe ushishuhudie pamoja nao.**

Katazo hili ni fumbo la uwongo wao katika ushahidi wao. Kwa sababu ni muhali mtume kushuhudia pamoja na washirikina. Na fumbo ni fasaha zaidi kuliko ufafanuzi.

**Wala usifuate matamaniao ya wale waliozikadhibisha ishara zetu na wale wasioamini Akhera, na ambao humlinganisha Mola wao.**

Baada ya Mwenyezi Mungu kuwahukumia uwongo na uzushi, anabainisha sababu ya hukumu yake hiyo kwa mambo matatu:

**Kwanza:** kuwa wao wanafuata hawaa na matamaniao. Hilo ameliletea ibara ya:

Wala usifuate matamaniao ya wale waliokadhibisha ishara zetu, kwa sababu ni muhali kwa Mtume kumfuata anayekadhibisha utume wake.

**Pili:** kwamba wao ni wale wasioamini Akhera; na asiyeamini Akhera hao- gopi mwisho wa uwongo.

**Tatu:** kwamba wao Humlinganisha Mola wao. Yaani wanamfanya kuwa ana wa kulingana naye katika kuumba. Na yeyote anayemshirikisha Mwenyezi Mungu haukubaliwi ushahidi wake, sababu yeye amefanya madhambi mabaya zaidi.

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

قُلْ تَعَالَوْا أَنُؤَلِّمُكُم مَّا كَرِهَ رَبُّكُمْ عَلَىٰكُمْ ۖ أَلَّا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۚ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۚ وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ مِمَّنْ إِمْلَاقٍ ۚ نَحْنُ نَرْزُقُكُمْ وَإِيَّاهُمْ ۚ وَلَا تَقْرَبُوا الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَّنَ ۚ وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ۚ ذَٰلِكُمْ وَصَّاكُم بِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ

﴿١٥١﴾

151. Sema: Njoooni niwasomee aliyowaharamishia Mola wenu: Kwamba msimshirikishe na chohote, Na kuwafanyia wema wazazi wawili. Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa kuishiwa sisi tutawaruzuku nyinyi na wao. Wala msikurubie mambo machafu, yaliyodhihirika na yaliyofichika; wala msiue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharamisha (kuiua), ila kwa haki. Hayo amewausia Mwenyezi Mungu ili mpate kutia akili.

وَلَا تَوَدُّوْا مَالَ الْيَتِيْمِ اِلَّا بِالَّتِي هِيَ اَحْسَنُ حَتَّىٰ يَبْلُغَ اَشُدَّهُ ۚ وَاَوْفُوا الْكَيْ لَ وَالْمِيْرَانَ بِالْفَيْسِطِ ۚ لَا نُكَلِّفُ نَفْسًا اِلَّا وُسْعَهَا ۚ وَاِذَا قُلْتُمْ فَاعْدِلُوْا وَلَوْ كَانَ دَا قُرْبَىٰ ۚ وَبِعَهْدِ اللّٰهِ اَوْفُوا ۚ ذَٰلِكُمْ وَصَّاكُم بِهِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُوْنَ ﴿١٥٢﴾

152. Wala msiukurubie mali ya yatima isipokuwa kwa njia bora zaidi, Mpaka afikie kukomaa kwake. Na kamilisheni vipimo vya ujazo na uzani kwa uadilifu. Hatuikalifishi nafsi ila kwa uweza wake Na msemapo semeni kwa uadilifu hata kama ni jamaa, Na tekelezenim ahadi ya Mwenyezi Mungu. Haya ameusiwa ili mpate kukumbuka.

وَأَنَّ هٰذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيْمًا فَاتَّبِعُوْهُ ۚ وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيْلِهِ ۚ ذَٰلِكُمْ وَصَّاكُم بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُوْنَ ﴿١٥٣﴾

153. Na kwa hakika hii ndiyo njia yangu iliyonyooka, basi ifuateni wala msifuata njia nyingine zikawatenga mbali na njia yake (Mwenyezi Mungu). Hayo amewausia ili muwe na takua.

### ALIYOWAHARAMISHA MOLA WENU

Aya 151 – 153

#### MAANA

Katika Aya zilizoatangulia, Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameonyesha kuwa washirikina walihalalisha na wakaharamisha kwa dhana na matamania; na kwamba wao walimnasibishia Mwenyezi Mungu shirki kwa uzushi na bila ya ujuzi wowote. Akawajibu kwa mantiki ya kiakili na kimaumbile, na akataja katika vilivyo haramu: Mfu, damu ya kutirizika, nyama ya nguruwe na kilichochinjwa bila ya kutajwa jina la Mwenyezi Mungu.

Katika Aya hizi tatu (tulizo nazo) ametaja baadhi ya yaliyo haramu, Kwa upande mwingine ametaja baadhi ya mambo yaliyowajibu; kama vile kutopunja katika vipimo, kutekeleza ahadi na kufuata usawa.

Kimsingi ni kuwa kila ambalo ni wajib kulifanya, basi ni haramu kuliacha na kila lililoharamu kulifanya basi ni wajib kuliacha.

Baadhi ya wafasiri wameuita mkusanyiko wa Aya hizi tatu kuwa nasaha kumi.

### **NASAHA KUMI**

**Sema: Njoooni niwasomee aliyowaharamishia Mola wenu: Kwamba msimshirikishe na chohote.**

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameanzia na msingi wa kwanza wa itikadi, ambao ni kukana shirki ambako mkabala wake ni kuthibitisha Tawhid. Haki zote na wajibu wote unategemea kwenye msingi huu, na kwa msingi huu hukubaliwa twaa na amali za kheri. Maana ya Tawhid yanafupika katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ﴾

“Hakuna chochote kama mfano wake” (42:11)

Si katika dhati wala sifa au vitendo.

**Na kuwafanyia wema wazazi wawili.**

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amekutanisha nasaha kwa wazazi wawili pamoja na uungu wake, kutambulisha kuwa kuwafanyiwa wema wazazi wawili kunapasa kuwe kwa aina yake. Ni kama kwamba amesema: Msimshirikishe Mwenyezi Mungu na kitu wala msishirikishe kuwafanyia wema wazazi wawili na wema wowote. Tumeyafafanua hayo katika kufasiri Juz.1 (2:83)

**Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa kuishiwa, sisi tutawaruzuku nyinyi na wao pia.**

Baada ya kuwausia watoto kwa mababa, sasa anawausia mababa kwa watoto, Yametangulia maelezo yake katika kufasiri Aya 137 ya Sura hii.

**Wala msikurubie mambo machafu, yaliyodhihirika na yaliyofichika.**

Kila linalopetuka mpaka katika ubaya ni ovu; kama vile zina, ulawiti, dhuluma na kuvunja heshima. Vilevile uwongo, kusengenywa, fitina, na husuda. Uovu mkubwa zaidi ni ulahidi, kumshirikisha Mwenyezi Mungu, kuwaudhi wazazi wawili, kuua nafsi isiyo na hatia na kula mali ya yatima.

Mwenyezi Mungu amehusisha kuyataja haya pamoja na kuwa yanaingia katika uwovu, kwa kufahamisha kuwa yamefikilia ukomo wa ubaya na uovu; ni sawa yawe yamefanywa kisiri au kidhahiri.

Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas kwamba watu wa wakati wa ujahiliya walikuwa wakichukia zinaa kufanywa dhahiri na walikuwa wakiifanya kisiri, ndipo akawakataza Mwenyezi Mungu katika hali zote mbili. Na imepokewa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.w.t), amesema: “Je, niwafahamishe yule aliye mbali na mimi?” Wakajibu: “Ndio Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!” Akasema: “Ni mwovu mno, mwenye kuchukiza, bahili, mwenye kiburi, hasidi, aliyesusuwaa moyo, aliye mbali na kila kheri inayotarajiwa na asiyeaminiwa na kila shari inayoogopwa.”

**Wala msiuue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharamisha (kuiua), ila kwa haki.**

Kimsingi, kuua nafsi ni haramu, wala hakuwi halali ila kwa sababu moja kati ya nne ambazo tatu katika hizo zimeelezwa na Hadith ya Mtume (s.a.w.w): “Haiwi halali damu ya Mwislamu (kuuawa) ila kwa moja ya mambo matatu: Kukufuru baada ya kuamini, kuzini baada ya kuoa na kuua nafsi bila ya haki.” Qur’an nayo imeelezea sababu ya nne iliposema:



﴿ إِنَّمَا جَزَاءُ الَّذِينَ يُحَارِبُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَسْعَوْنَ فِي الْأَرْضِ فَسَادًا أَنْ يُقَتَّلُوا أَوْ يُصَلَّوْا ﴾

“Hakika malipo ya wale wanaopigana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kufanya ufisadi katika ardhi, ni kuuawa au kusulubiwa” (5:33).

Hayo amewausia Mwenyezi Mungu ili mpate kufahamu.

Yaani mjue ubaya wa ushirikina, kuuu nafsi, kufanya uovu na mjue uzuri wa kuwafanyia wema wazazi wawili.

Wala msiikurubie mali ya yatima isipokuwa kwa njia bora zaidi.

Kuzuia kukurubia ndio ufasaha zaidi wa kukataza kuliko kukataza tendo lenyewe, na kunahusu njia zote za matumizi; kama ambavyo bora zaidi ni nzuri kuliko bora tu.

Maana yaliyokusudiwa ni kutilia mkazo katika kutunza mali ya kila asiyeweza kutumia mali yake; awe yatima, mwendawazimu, safihi, aliyepotea au mtoto mdogo anayesimamiwa mali zake na baba yake. Kwa hiyo ni juu ya wasimamizi kuzichunga mali za wanaowasimamia na kuangalia vizuri mambo yao.

Kuanzia hapa ndio wamesema kundi la mafakihi wakubwa, kwamba haiwezekani kwa msimamzi kutumia mali ya anayemsimamia ila kwa masilahi ya mwenye mali. Na sisi tuko pamoja na rai hii; hata kama msimamizi ni baba au babu. Dalili yetu ni neno ‘njia bora zaidi’ Ama Hadith isemayo: “Wewe na mali yako ni (milki) ya baba yako”, ni hukumu ya kimaadili tu, si ya kisharia; kwa dalili ya neno ‘Wewe’, kwa sababu, mtoto si bidhaa anayomiliki baba.

**Utauliza kuwa:** neno yatima linahusika na yule aliyefiwa na baba yake akiwa mdogo, sasa imekuaje kulihusisha na kila asiyeweza kutumia?

Sisi tunajua kabisa kwamba sababu ya kutumia kwa njia iliyo bora zaidi ni kule kushindwa kutumia yule mwenye mali na wala sio uyatima; na kushindwa kutumia kumethibitika kwa wote waliotajwa bila ya tofauti.

Mpaka afikie kukomaa kwake. Utaipata tafsiri yake katika Juz.5 (4:6)

Na kamilisheni vipimo vya ujazo na uzani kwa uadilifu mkiuza au mkininua.

Hatuikalifishi nafsi ila kwa uweza wake. Jumla hii imeingia katikati ikiwa na makusudio ya kufahamisha kuwa ukamilishaji wa vipimo uliotajwa ni ule uliozoelekea kwa watu; husamehewa kiasi kichache kilichozidi au kupungua. Kwa sababu kutekeleza kipimo cha sawaswa kabisa ni aina ya uzito:

﴿ وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ ﴾

“Wala hakuwawekea mambo mazito katika dini” (22:78)

Kwa hali yoyote ni kuwa msingi katika aina zote za biashara ni kuridhia pande zote mbili, iwe ni bidhaa inayopimwa kwa kilo, kwa kuhesabiwa kwa mita, kukadiriwa kwa kifikra, kama kuandika, au kwa kuangalia tu, kama sanaa iliyoundwa kwa mkono.

Na msemapo semeni kwa uadilifu hata kama ni jamaa.

Huu ndio ushupavu wa yule anayemwogopa Mwenyezi Mungu na kumfanyia ikhalsi na kutambua kuwa mbele yake kuna majukumu, sio kuwa mbele yake kuna mke, baba, mama, mtoto au mkwe. Hakuna chochote isipokuwa haki na uadilifu tu. Ama mwenye kutumia jina la dini, kisha afuate matamanio yake kwa ndugu au rafiki, basi huyo hana dini kitu.

Na tekelezeni ahadi ya Mwenyezi Mungu.

Kila aliloharamisha Mwenyezi Mungu na alilolikataza ni ahadi yake. Utekelezaji wake ni kufuata amri na kutii. Hayo amewausia ili mpate kukumbuka, Msimsahau kumtii yule asiyewasahau.

Na kwa hakika hii ndiyo njia yangu iliyonyooka.

Hii ni ishara ya yote yaliyotajwa; ndiyo njia ya Mwenyezi Mungu iliyonyooka, vinginevyo ni upotevu.

Basi ifuateni wala msifuat njia nyingine; kama vile shirki, ulahidi, vikundi na dini za ubatilifu. Zikawatenga mbali na njia yake (Mwenyezi Mungu).

Njia yoyote isiyokuwa Qur'an na Uislam basi hiyo ni njia ya matamanio tu, Na matamanio hayana udhibiti wala mpaka wowote. Watu wakiyafuata ndipo hugawanyika vikundi na vyama mbalimbali. Lakini kama wote wakifuata dini ya Mwenyezi Mungu basi itikadi ya kweli na imani ya sawa itawaweka pamoja.

Kuna Hadith isemayo kuwa Mtume (s.a.w.w) alipiga msitari kwa mkono wake kisha akasema: “Hii ndiyo njia ya Mwenyezi Mungu iliyonyooka:” Kisha akapiga msitari kuumeni na kushotoni mwa msitari ule, akasema: “Hii siyo njia ispokuwa shetani ndiyo anayoilingania; kisha akasoma: “Na kwa hakika hii ndiyo njia yangu iliyonyooka, basi ifuatie wala msifuat njia nyingine zikawatenga mbali na njia yake (Mwenyezi Mungu).”

ثُمَّ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ تَمَامًا عَلَى الَّذِي أَحْسَنَ وَتَفْصِيلًا لِكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً لَّعَلَّهُمْ بِلِقَاءِ

رَبِّهِمْ يُؤْمِنُونَ ﴿١٥٤﴾

154. Kisha tulimpa Musa Kitab, kwa kumtimizia yule aliyefanya wema. Na kuwa ni ufafanuzi wa kila kitu na mwongozo na rehema ili wapate kuamini kukutana na Mola wao.

وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ فَاتَّبِعُوهُ وَاتَّقُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿١٥٥﴾

155. Na hii ni Kitab tulichokiteremsha kilicho barikiwa. Basi kifuateni na muwe na takua ili mrehemwiwe.

أَنْ تَقُولُوا إِنَّمَا أَنْزَلَ الْكِتَابَ عَلَى طَائِفَتَيْنِ مِنْ قَبْلِنَا وَإِنْ كُنَّا عَنْ دِرَاسَتِهِمْ لَغَافِلِينَ ﴿١٥٦﴾

156. Msije mkasema kuwa vitabu viliteremshiwa makundi mawili tu, yaliyokuwa kabla yetu nasi tulikuwa hatuna habari ya yale waliyoyasoma.

أَوْ تَقُولُوا لَوْ أَنَّا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ لَكُنَّا أَهْدَى مِنْهُمْ ۖ فَقَدْ جَاءَكُمْ بَيِّنَةٌ مِنْ رَبِّكُمْ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ ۖ فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ كَذَبَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَصَدَفَ عَنْهَا ۗ سَنَجْزِي الَّذِينَ يَصْدِفُونَ

عَنْ آيَاتِنَا سُوءَ الْعَذَابِ بِمَا كَانُوا يَصْدِفُونَ ﴿١٥٧﴾

157. Au mkasema: Lau tungeliteremshiwa Kitab bila shaka tungelikuwa waongofu zaidi kuliko wao. Basi imewafikia hoja kutoka kwa Mola wenu, uwongofu na rehema. Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayezikadhibisha ishara za Mwenyezi Mungu na akajitenga nazo? Tutawalipa wale wanaojitenga na ishara zetu, adhabu mbaya kwa sababu ya kule kujitenga kwao.

## KISHA TULIMPA MUSA KITAB

Aya 154 – 157

## MAANA

### Kisha tulimpa Musa Kitab.

Wameduwaa wafasiri kuhusu neno ‘Kisha’ Kwa sababu mazungumzo ni ya Qur’an katika Aya zilizotangulia. Na Aya hii inazungumzia Tawrat iliyoshuka kabla ya Qur’an; na ‘Kisha’ inafahamisha kuja nyuma ya kilicho kabla yake kwa wakati. Sasa imekuwaje itajwe Qur’an kisha Tawrat na iliyoanza ni Tawrat?

Razi ametaja njia tatu, na Tabrasi akazidisha ya nne, Sisi hatuoni jambo lolote la kurefusha maneno hapo. Kwa sababu mpangilio hapa ni wa maneno sio wa wakati, na uunganisho ni wa habari kuungana na habari nyingine sio maana kuungana na maana nyingine.

### Kumtimizia yule aliyefanya wema.

Yaani tumempa Musa Kitab nacho kinatimiza upungufu wa aliyefanya wema, kunafaika nacho; kama kusema kwake Mwenyezi Mungu:

﴿الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيْتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا﴾

“Leo nimewakamilishia dini yenu na kuwatimizia neema yangu na nimewapendelea Uislamu kuwa dini” (5:3)

### Na kuwa ni ufafanuzi wa kila kitu.

Hii ni sifa ya pili ya Kitab cha Musa <sup>(a.s)</sup> kwamba kimekusanya hukumu zote walizozitaja watu wa wakati ule. Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

﴿وَكَتَبْنَا لَهُ فِي الْأَلْوَابِ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ مَوْعِظَةً وَتَفْصِيلًا لِكُلِّ شَيْءٍ﴾

“Na tukamwandikia katika mbao mawaidha ya kila kitu na ufafanuzi wa kila kitu” (7:144).

### Na mwongozo na rehema.

Sifa mbili nyingine za Kitab cha Musa, Kwa mwongozo, watu watajua haki na kheri, na kwa rehema, watu wataishi maisha ya utulivu.

### Ili wapate kuamini kukutana na Mola wao.

Dhamiri inawarudia waisrael, kwa maana tumempa Musa Kitab kilichokusanya sifa zilizotajwa, ili watu wake wamwamini Mwenyezi Mungu na thawabu zake na adhabu yake. Lakini wao waling’ang’ania inadi yao, na wakasema miongoni mwa waliloyasema:

﴿يَا مُوسَىٰ لَنْ نُؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ نَرَى اللَّهَ جَهْرَةً﴾

“Ewe Musa! Hatutakuamini mpaka tumwone Mungu waziwazi” Juz.1 (2:55)

Tukadrie kama wangemwona Mwenyezi Mungu waziwazi - na kukadiria muhali si muhali - basi wao wangesema kuwa huyu si Mola, kwa vile yeye si pauni wala dola.

### Na hii ni Kitab tulichokiteremsha kilichobarikiwa na baraka.

Hii ni Qur’an tukufu, nayo ni yenye baraka kwa sababu ina kheri na manufaa mengi.

### Basi kifuateni na muwe na takua ili mrehamiwe.

Fuateni aliyowaamrisha na muache aliyowakataza ili iwaenee rehema yake duniani na akhera.

Msije mkasema kuwa vitabu viliteremshiwa makundi mawili tu, yaliyokuwa kabla yetu nasi tulikuwa hatuna habari ya yale waliyoyasoma.

Wanaambiwa washirikina wa Kiarabu. Makusudio ya vitabu ni Tawrat na Injil; na makundi mawili ni watu wa Kitab: Mayahudi na Manaswara (Wakristo).

Maana ni kuwa enyi Waarabu, tumewateremshia Qur'an kwa lugha yenu na kwa mtu wenu anayetokana nanyi ili msiwe na udhuru wa shirki yenu, kwamba hakikuteremshwa Kitab kwa lugha yenu na kuwa hamkujua kukisoma na kujifundisha mafunzo yake.

**Au mkasema: Lau tungeliteremshiwa Kitab bila shaka tungelikuwa woangofu zaidi kuliko wao.**

Katika Aya iliyotangulia Mwenyezi Mungu anawaondolea udhuru wa lugha, na katika Aya hii anawaondolea udhuru wa kufikiwa na Kitabu chenyewe. Kwa ufupi ni kuwa Aya hii na iliyo kabla yake inafanana na kauli ya asemaye: "Fulani ni tajiri na mimi sina chochote, lau ningekuwa na kitu basi ningelifanya mengi." Ndipo Mwenyezi Mungu akawajibu kwa jawabu mkataa:

**Basi imewafikia hoja kutoka kwa Mola wenu, na uwongofu na rehema.**

Makusudio ya hoja ni Qur'an, ndani yake mna dalili na ubainifu wa kumsadikisha Muhammad (s.a.w.w). Vilevile mna hukumu na mafunzo yenye kuwatoa watu kwenye giza kwenda kwenye mwanga.

**Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayezikadhibisha ishara za Mwenyezi Mungu na akajitenga nazo?**

Hakuna kabisa dhalimu mkubwa wa nafsi yake na watu kuliko yule anayekana haki na kheri, akahangaika katika dunia kufanya ufisadi na kupinga njia ya Mwenyezi Mungu.

**Tutawalipa wale wanaojitenga na ishara zetu adhabu mbaya kwa sababu ya kule kujitenga kwao.**

Ishara za Mwenyezi Mungu ni hoja zake na dalili zake. Maana ni kuwa yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu amesimamisha dalili na hoja mkataa juu ya umoja wake na juu ya utume wa Muhammad na ukweli wa aliyokuja nayo kutoka kwa Mola wake, lakini washirikina walipinga wakakataa kuzingatia vizuri hoja hizo kwa kuifanyia inadi haki na watu wa haki. Kwa hiyo wakastahiki hizaya na adhabu kali.

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ تَأْتِيَهُمُ الْمَلَائِكَةُ أَوْ يَأْتِيَ رَبُّكَ أَوْ يَأْتِيَ بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ ۗ يَوْمَ يَأْتِي بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ لَا يَنْفَعُ نَفْسًا إِيْمَانُهَا لَمْ تَكُنْ آمَنَتْ مِنْ قَبْلُ أَوْ كَسَبَتْ فِي إِيمَانِهَا خَيْرًا ۗ قُلْ انْتَظِرُوا إِنَّا مُنْتَظِرُونَ ﴿١٥٨﴾

158. Je, wananogoja jingine ila wawafikie Malaika au afike Mola wako au ziwafikie baadhi ya ishara za Mola wako? Siku zitakapofika baadhi ya ishara za Mola wako, basi mtu haitamfaa imani yake ambaye hakuamini zamani, au hakuchuma kheri kwa imani yake. Sema: Ngojeni , sisi pia tunangoja.

إِنَّ الَّذِينَ فَرَقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شِيعًا لَسْتَ مِنْهُمْ فِي شَيْءٍ ۗ إِنَّمَا أَمْرُهُمْ إِلَى اللَّهِ ثُمَّ يُنَبِّئُهُم بِمَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿١٥٩﴾

159. Hakika wale walioigawa dini yao na wakawa makundi makundi, huna uhusiano nao wowote. Hakika shauri lao liko kwa Mwenyezi Mungu tu. Kisha atawaambia yale waliyokuwa wakiyafanya.

مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَمْثَالِهَا ۗ وَمَنْ جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَى إِلَّا مِثْلَهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٦٠﴾

160. Mwenye kufanya vizuri atalipwa mfano wake mara kumi. Na mwenye kufanya vibaya hatalipwa ila sawa na hivyo tu, Nao hawatadhulumiwa.

### HAITAMFAA MTU ILA IMANI YAKE

**Aya 158 – 160**

#### MAANA

Je, wananogoja jingine ila wawafikie Malaika au afike Mola wako au ziwafikie baadhi ya ishara za Mola wako?

Swali hapo si la kuuliza bali ni la kukanusha. Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kutaja kwamba washirikina wamekana dalili za Qur'an, wakakataa kuzingatia maana yake, sasa anasema katika Aya hii kuwa wao hawataamini isipokuwa mambo matatu: Kuja Malaika, kuja Mola na kuja baadhi ya ishara. Hata hivyo Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakubainisha Malaika ambaye anapasa kuwajia ili waamini.

Je, ni Malaika wa mauti au mwingine? Wala pia hakubainisha makusudio ya kuja Mola, Je, ni kuja kwake kwa madai yao au ni kuja amri yake, kama ilivyotokea? Vilevile hakubainisha baadhi ya ishara, Je, ni ishara walizozitaka au ni alama za Kiyama?

Wafasiri wengi wamesema kuwa makusudio ya Malaika ni Malaika wa mauti. Na makusudio ya kuja Mola ni kuja adhabu na mateso yake. Na baadhi ya ishara, ni ishara za Kiyama.

Tafsir hii ndiyo iliyo karibu zaidi na maana. Kwa sababu, maneno yanayofuatia yanataja mambo haya matatu yakitambulisha kauli ya wafasiri na kuitilia nguvu; nayo ni kauli yake Mwenyezi Mungu:

Siku zitakapofika baadhi ya ishara za Mola wako, basi mtu haitamfaa imani yake ambaye hakuamini zamani, au hakuchuma kheri kwa imani yake.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu kwamba toba na imani wakati wa kuja mojawapo ya mambo haya matatu, haifai kitu; isipokuwa inayofaa ni imani na amali njema anayoichuma mumin kabla ya kutokea hayo. Kwani wakati wa kutolewa roho, au ishara za Kiyama au wakati wa kushuka adhabu huwa hakuna taklifa yoyote. Ikiwa hivyo, basi kuweco imani na kutokuweco ni sawa tu.

Kauli yake Mwenyezi Mungu: Au kuchuma kheri kwa imani yake, inaishiria kuwa kumwamini Mungu kunamwoko mtu na kukaa milele tu motoni, lakini hakumwoko na adhabu ya moto. Ama anayemwamini Mwenyezi Mungu na akafanya amali njema, basi hataguswa na moto.

**Sema: Ngojeni haya mambo matatu, sisi pia tunangoja.**

﴿ فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ مَنْ يَأْتِيهِ عَذَابٌ يُخْزِيهِ ﴾

“Punde tu mtajua ni nani itakayemjia adhabu ya kufedhehesha” (11:39).

Hakika wale walioigawa dini yao na wakawa makundi makundi, huna uhusiano nao wowote.

Hapa anaambiwa Mtume (s.a.w.w)

Kama ambavyo walihitalifiana wale walioigawa dini yao na wakawa makundi makundi, vilevile wafasiri nao wamekuwa makundi makundi katika kufasiri makusudio ya ‘walioigawa dini yao.’ Baadhi wamesema kuwa hao ni washirikina kwa kuwa baadhi yao wanaabudu masanamu, wengine nyota na baadhi yao mwanga na giza. Wafasiri wengine wamesema kuwa ni watu wa Kitab.

Kwani Mayahudi waligawanyika makundi ya Masadukayo, Mafarisayo na Mahaasid<sup>1</sup> Ama Wakristo wao waligawanya kanisa la Mashariki na la Magharibi.

Pia imesemekana kuwa ni makundi ya Kiislamu. Na ikasemekana kuwa ni wote wenye mila na vikundi.

Maelezo bora niliyosoma kuhusu tafsir ya Aya hii ni yale aliyosema mwenye tafsir Al-Manar: “Makusudio ya wale walioigawa dini yao wakawa vikundi ni watu wa Kitab. Na makusudio ya kujitenga nao Mtume ni kuhadharishwa Waislamu wasigawanye dini yao wakawa na vikundi kama watu wa Kitab, ili wajue kwamba wao wakifanya vitendo vya watu wa Kitab, basi Muhammad (s.a.w.w) atakuwa mbali nao.”

**Hakika shauri lao liko kwa Mwenyezi Mungu tu.**

Yeye peke yake ndiye anayemiliki hisabu na adhabu ya mwenye kufarikisha waja wake na kuleta uadui na chuki katika dini na penginepo.

Kisha atawaambia yale waliyokuwa wakiyafanya. Kuanzia wale watakaokubali mpaka wale wanaochochea:

---

1 Miongoni mwa kauli za wa mafarisayo ni kuwa wafu watarudi kwenye dunia hii washiriki katika ufalme wa Masih atakayekuja. Katika kauli za wa masadukayo ni kuwa hakuna uhai kabisa baada ya kufa si duniani wala akhera. Na miongoni mwa kauli za wa Haasid ni usawa baina ya watu, Soma Kitabu kiiwacho Asfar Muqaddasa cha Aliy Abdul Wahid Wafi.

﴿وَقَالَتْ أُولَاهُمْ لِأَخْرَاهُمْ فَمَا كَانَ لَكُمْ عَلَيْنَا مِنْ فَضْلٍ فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ

﴿تَكْسِبُونَ﴾

“Na wa mwanzo wao watawaambia wa mwisho wao; basi nyinyi pia hamkuwa na ubora kuliko sisi. Basi onjeni adhabu kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyachuma.” (7:39)

Mwenye kufanya vizuri atalipwa mfano wake mara kumi. Na mwenye kufanya vibaya hatalipwa ila sawa na hivyo tu, Nao hawatadhulumiwa.

Kila lililo na radhi ya Mwenyezi Mungu na manufaa kwa watu basi ni zuri; na kila lenye machukivu ya Mwenyezi Mungu na ufisadi kwa watu basi ni baya.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ni mwadilifu, mkarimu. Miongoni mwa uadilifu wake ni kumlipa mwenye kufanya uovu, adhabu inayolingana nao. Na miongoni mwa ukarimu wake ni kusamehe, na kumwongozea mtenda mema ziada inayofikia kumi, au mia saba, au isiyo na idadi kulingana na lengo la mtenda mema, sifa zake na hali yake. Angalia Juz 2. (2:261).

Kuna Hadith ya Mtume (s.a.w.w) isemayo: “Hakika Mwenyezi Mungu amesema: “Wema malipo yake ni kumi au zaidi, na uovu ni moja au kusamehewa. Basi ole wake yule ambaye kumi yake imeshindwa na moja yake”.

Anaendelea kusema Mtume: “Mwenyezi Mungu anasema: ‘Mja wangu akikusudia wema mwandikieni jema moja hata kama hatafanya; na akifanya basi mwandikieni kumi mfano wake, Kama atakusudia uovu, msimwandikie kitu; kama ataufanya basi mwandikieni moja.”

قُلْ إِنِّي هَدَانِي رَبِّي إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ دِينًا قِيمًا مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا ۚ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

﴿١٦١﴾

161. Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu ameniongoza katika njia iliyonyooka, dini yenye msimamo ndiyo mila ya Ibrahim mnyoofu, Wala hakuwa miongoni mwa washirikina.

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٢﴾

162. Sema: Hakika Swala yangu na ibada zangu na uhai wangu na mauti yangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu.

لَا شَرِيكَ لَهُ ۚ وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٦٣﴾

163. Hana mshirika. Na hayo ndiyo niliyoamrisha, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu.

قُلْ أَعْيَرَ اللَّهُ أَبْنِي رَبًّا وَهُوَ رَبُّ كُلِّ شَيْءٍ ۚ وَلَا تَكْسِبُ كُلُّ نَفْسٍ إِلَّا عَلَيْهَا ۚ وَلَا تَزِرُ

وَأِزْرَةَ وِزْرَ أُخْرَى ۚ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ مَرْجِعُكُمْ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿١٦٤﴾

164. Sema: Je, nimtafute Mola mwingine asiye kuwa Mwenyezi Mungu? Na hali yeye ni Mola wa kila kitu? Na kila nafsi haichumii ila (inajichumia) yenyewe. Wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine. Kisha marejeo yenu ni kwa Mola wenu, naye atawaambia yale mliyokuwa mkihitalifiana.

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ خَلَائِفَ الْأَرْضِ وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ لِيُبْلُوَكُمْ فِي مَا

آتَاكُمْ ۚ إِنَّ رَبَّكَ سَرِيعُ الْعِقَابِ وَإِنَّهُ لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٦٥﴾

165. Naye ndiye aliyewafanya makhalifa wa ardhi na akawainua baadhi yenu juu ya wengine ili awajaribu katika aliyowapa. Hakika Mola wako ni mwepesi wa kuadhibu. Na hakika yeye ni mwingi wa maghufira, mwenye huruma.

## SEMA MOLA WANGU AMENIONGOZA

Aya 161 – 165

### MAANA

Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu ameniongoza katika njia iliyonyooka.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuwataja wale walioigawanya dini yao wakawa vikundi, alimwamrisha Mtume wake kuwatangazia washirikina, watu wa Kitab na wengineo kuwa Mwenyezi Mungu amemwongoza Mtume kwa umbile safi, akili kamili na kwa wahyi utokao kwake, kwenye njia inayomweka mbali na batili na kumfikisha kwenye dini yenye msimamo ndiyo mila ya Ibrahim mnyoofu.

Yaani njia ambayo Mwenyezi Mungu amemuongoza nayo Mtume wake Muhammad ndiyo dini ya Nabii Ibrahim <sup>(a.s)</sup> kipenzi cha Mwenyezi Mungu ambayo wanaitukuza watu wa dini zote.

Wala hakuwa miongoni mwa washirikina.

Bali ni katika maadui wakubwa wa ushirikina na watu wake. Hili ni jibu la Washirikina wa Kiquraish ambao wanadai kwamba wao wako kwenye dini ya Nabii Ibrahim <sup>(a.s)</sup>.

Sema: Hakika Swala yangu na ibada zangu na uhai wangu na mauti yangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu.

Maudhui ya Aya iliyotangulia ni misingi ya dini na itikadi kwa kulinganisha na neno: ‘Wala hakuwa miongoni mwa washirikina’ na maudhui ya Aya hii ni matawi ya dini na sharia, kwa kulinganisha Swala na ibada.

Kuunganisha ibada kwenye Swala ni katika hali ya kuunganisha ujumla kwenye mahsusi; kama vile kauli yake Mwenyezi Mungu:

﴿وَمَا أَوْتِي مُوسَىٰ وَعِيسَىٰ وَالنَّبِيُّونَ مِنْ رَبِّهِمْ﴾

“Na waliyopewa Musa na Isa na Mitume kutoka kwa Mola wao” (3:84)

Uhai na mauti hapa ni fumbo la uthabiti na kuendelea. Maana ni kuwa ibada za Muhammad (s.a.w.w) na maisha yake yote ya kiitikadi, nia na amali, yanaekelea kwa Mwenyezi Mungu peke yake wala hakengeuki nayo mpaka kufa.

Hana mshirika, Na hayo ndiyo niliyoamrisha, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu.

Aya hii ni ufafanuzi na usisitizo wa yaliyo katika Aya iliyotangulia – Tawhid na ikhlasi. Na Muhaammad ni Mwislamu wa kwanza katika umma wake kwa sababu yeye ndiye mwenye wito huo.

Sema: Je, nimtafute Mola mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu?

﴿فَأَيْنَمَا تُولُوا فَتَمَّ وَجْهَ اللَّهِ﴾

Atakayemtafuta Mola huyo atampata wapi, na hali: “Mahala popote mnakoelekea ndiko kwenye uelekeo wa Mwenyezi Mungu?”Juz. 1 (2:115)

Na hali yeye ni Mola wa kila kitu?



Na Mola wa kila kitu ni mmoja tu, hana wa kinyume chake.

### **KILA MTU NA MZIGO WAKE**

**Na kila nafsi haichumii ila (inajichumia) yenyewe.**

Kila alifanyalo mtu liwe kheri au shari basi ni mazao ya silika yake na hali yake kwa ujumla. Anayenasibisha matendo ya mtu kwa mwingine, ni sawa na anayemasibisha mtoto kwa asiyekuwa mama yake, na matunda kwa usiokuwa mti wake.

**Wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine.**

Makusudio ya mzigo hapa ni dhambi. Jumla hii inatilia mkazo jumla iliyo kabla yake, na maana yake ni kwamba:

﴿لَهَا مَا كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا اكْتَسَبَتْ﴾

**“Faida ya yale iliyoyachuma ni yake na hasara iliyochuma ni yake.”** Juz. 2 (2:286).

Sio yaliyochumwa na nafsi nyingine.

Hii ndiyo asili ya kidini na kiakili; haiwezekani kuifuta au kuigeuza. Maulama wa lugha na fasaha wametoa masuala mengi na hukumu kwenye asili hii.

**Utauliza:** Aya hii inaonyesha kuwa kila mtu na lake tu, sasa uko wapi wajibu wa Jihadi, kutoa nasaha na kusaidiana katika wema na takua.

**Jibu:** Maadhui ya Aya hii yanahusiana na adhabu tu, na kwamba mtu hataadhibiwa kwa kosa la mwingine; wala haina uhusiano wowote na jihadi na nasaha na mengineyo, kwa umbali au karibu. Kwa sababu kuadhibiwa kwa kosa la mwingine ni jambo mbali na wajibu wa jihadi na kurekebisha ufisadi ni jambo jengine.

**Swali la pili:** watu wamezoea kutoa sadaka ya mali na chakula kwa ajili ya roho za maiti wao; wakasoma Qur'an na kuwapelekea thawabu; je, hii inajuzu kisharia? Na je, maiti wananufaika nayo, Kama ni hivyo, itakuwaje na ilivyo ni kuwa wafu hawaadhibiwi kwa maovu ya walio hai, basi iwe pia wasineemeke na mema yao?

**Jibu:** Tumesema kuwa akili na sharia inakataa kuadhibiwa mtu kwa kosa la mtu mwingine na kushirikishwa kwenye kosa hilo. Kuhusu thawabu, katika mtazamo wa akili, hakuna kizuizi kwa aliyefanya wema kumshirikisha asiyefanya wema ule katika thawabu anazostahiki kwa amali yake.

Na sharia imelieleza hilo, hivyo imepasa kulisadiki. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) anasema: “Mwanadamu akifa, hukatika amali yake isipokuwa mambo matatu: Sadaka inayoendelea, au elimu inayopatiwa manufaa, au mtoto mwema atakayemwombea, dua?” Akaendelea kusema: “Atakayekufa na ana saumu anayodaiwa basi na amfungie walii wake”.

Akasema tena: “Mwenye kuingia makaburini akasoma Sura ya Yasin huwahafifishia waliozikwa hapo siku hiyo. Na anapata wema kwa idadi ya waliomo makaburi.” Imam Jafar As-sadiq <sup>(a.s)</sup> naye anasema: “Ni jambo gani linalomzuia mtu kuwafanyia wema wazazi wake mara kwa mara?”

Kwa hiyo Hadith hizi na nyinginezo zinafahamisha kwamba maiti ananufaika kwa kupelekewa thawabu kwa amali ya kheri. Na akili hailikatai hilo kabisa. Kwa sababu hilo linaafikiana na fadhila za Mwenyezi Mungu na ukarimu wake.

Lakini watu wamezidisha mno na kupetuka mipaka ya ilivyoelezwa. Na mafakihhi wameafikiana kuwa kila mwenye kufanya ambalo halikuelezwa kwa makusudio ya kuwa linatiliwa mkazo na sharia basi amefanya uzushi (bid'a) katika dini na amemzulia Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Kwa hiyo ni bora ampelekee thawabu maiti kwa kutarajia anufaike nazo, bila ya kukusudia kuwa hilo llimependekezwa na dini na sharia.

**Kisha marejeo yenu ni kwa Mola wenu, naye atawaambia yale mliyokuwa mkihitalifiana.**

Bila ya kutegemea akili au Wahyi; mkakubali yale mliyoyazoea na sio haki, na mkayakana yale yanayochukiwa na mapenzi yenu na matamania yenu.

### **ARDHI NA NYUMBA**

**Naye ndiye aliyewafanya makhalifa wa ardhi na akawainua baadhi yenu juu ya wengine ili awajaribu katika aliyowapa.**

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameiumba ardhi hii akaifanya ni mahali pema panapofaa kwa maisha ya binadamu kutokana na mazingira yake, mpangilio wake, umbo lake na kuwa mbali kwake na jua na mwezi. Akaiandalia yote anayoyahitaji mtu mpaka nyenzo za kujipumbaza na kujistarehesha; sawa na nyumba iliyokamilika kila kitu. Kisha akamweka mtu, ndani ya hiyo ardhi baada ya kumwandalia nyenzo zote za kunufaika na kheri zake na baraka zake.

Na hekima yake ikataka watu watofautiane katika nyenzo hizo na kwamba baadhi yao wawe zaidi ya wengine katika akili, elimu na nguvu za mwili. Na akawawekea njia iliyo sawasawa ili awajaribu wenye nguvu kuwa je wataishukuru neema hii na kuzielekeza nguvu zao kwenye masilahi yao na maslahi ya ndugu zao wanaadamu; au watazifanya ni nyezo za kudhulumu, kunyang'anya, kujiadhimisha na kujifaharisha?

Aya hii imefahamisha kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemleta mtu katika ardhi hii kwa ajili ya elimu na matendo yenye kunufaisha.

**Utauliza:** Utaunganishaje Aya hii na Aya isemayo:

﴿ وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴾

“Na sikuumba majini na watu ila waniabudu?.” (51:56)

**Jibu:** Hazipingani Aya hizi mbili. Kwa sababu elimu na kazi yenye kunufaisha ni ibada ya Mwenyezi Mungu, bali ni katika ibada bora, na twaa iliyo kamili.

**Hakika Mola wako ni mwepesi wa kuadhibu.**

Anawajaribu waja wake ili ampambanue mwovu na mwema, amwadhibu huyu na kumpa thawabu yule.

**Na hakika yeye ni mwingi wa maghufira, mwenye huruma.**

Huruma yake haina mpaka, wala msamaha wake hauna kifungu chochote, Ndio! Toba inajaalia msamaha ndio malipo yake yenye kulingana na unabaki msamaha wa ukarimu na kutoa kwa aombaye, hana wa kumlazimisha, isipokuwa yeye mwenyewe mtukufu. Hii ndiyo dalili ya kauli yake:

﴿ وَمَا أَصَابَكُمْ مِنْ مُصِيبَةٍ فِيمَا كَسَبَتْ أَيْدِيكُمْ وَيَعْفُو عَنْ كَثِيرٍ ﴾

“Na masaiibu yanayowasibu ni kwa sababu ya yaliyochumwa na mikono yenu; na Mwenyezi Mungu husamehe mengi.” (42:30).

Yaani mengi yaliyochumwa na mikono yetu.  
Mola! tuokoe na yanayotokana na sisi wenyewe na tunakuomba  
utusamehe mizigo yetu wenyewe!

**MWISHO WA SURA YA SITA: AL-AN'AM**

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

Sura Ya Saba: Sura Al-A'raf

Imeteremshwa Makka, isipokuwa Aya 163, Mwenye Majmau anasema imeshuka Madina. Ina Aya 205.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu

﴿المص﴾ (1)

1. Alif Lam Mim Swad

﴿كِتَابٌ أَنْزَلَ إِلَيْكَ فَلَا يَكُنْ فِي صَدْرِكَ حَرَجٌ مِّنْهُ لِتُنذِرَ بِهِ وَذِكْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ﴾ (٢)

2. Kitab kimeteremshwa kwako, basi isiwe dhiki kifuani mwako kwacho ili upate kuonya kwacho na kiwe ni ukumbusho kwa wanaoamini.

﴿اتَّبِعُوا مَا أَنْزَلَ إِلَيْكُم مِّن رَّبِّكُمْ وَلَا تَتَّبِعُوا مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءَ قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ﴾ (٣)

3. Fuatani mliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wenu, Wala msifuate wasimamizi badala yake, Ni machache mnayoyakumbuka.

### KITABU KIMETEREMSHWA KWAKO

**Aya 1 – 3**

#### MAANA

Alif Lam Swad

Hizi huandikwa na kutamkwa kwa majina ya herufi zake kama zilivyo. Yamepita maelezo yake katika Juz.1 mwanzo wa Sura ya pili (Al- Baqara).

Kitab kimeteremshwa kwako, basi isiwe dhiki kifuani mwako kwacho, Ili upate kuonya kwacho na kiwe ni ukumbusho kwa wanaoamini.

Maneno anaambiwa Mtume Muhammad (s.a.w.w), Makusudio ya Kitab ni Qur'an, na waumini ni kila anayenufaika na Qur'an, ni sawa iwe ni sababu ya kuamini kwake au kuimarisha imani yao waendeleo nayo.

Maana ni kuwa: Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameteremsha Qur'an kwa Mtume (s.a.w.w) ili awaonye kwayo walahidi na washirikina na watu wa dini za ubatifu; na ili wanufaike nayo watu wenye maumbile safi.

Kazi hii inampa uzito Mtume (s.a.w.w) kutoka kwa makafiri ambao anawakabili kwa Qur'an. Kwa sababu, inalenga katika kubatilisha itikadi zao na hali zao ambazo wamezirithi kutoka kwa mababu zao wa jadi. Hapo Mtume alipata dhiki kutokana na inadi na upinzani wao.

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَلَقَدْ نَعْلَمُ أَنَّكَ يَضِيقُ صَدْرَكَ بِمَا يَقُولُونَ﴾ (٩٧)

“Na kwa hakika sisi tunajua kwamba kifua chako kinadhikika kwa yale wayasemayo” (15:97) .

Na akasema tena Mwenyezi Mungu:

﴿إِنَّا سَنُلْقِي عَلَيْكَ قَوْلًا ثَقِيلًا﴾ (٥)

“Hakika sisi tutakuteremshia kauli nzito” (73:5)

Fuatani mliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wenu.

Katika Aya iliyotangulia Mwenyezi Mungu amemwamrisha Mtume wake kufikisha na kutojali upinzani. Katika Aya hii anawaamrisha watu wamfu- ate Mtume na waitumie Qur'an.

Ali Al-Murtadha <sup>(a.s)</sup> anasema: “Hatawaadhibu Mwenyezi Mungu watu wajinga kwa kutojifundisha, mpaka awaadhibu wenye elimu kwa kutofundisha” Na kinyume chake pia.

**Wala msifuate wasimamizi badala yake.**

Kwa sababu hakuna badala ya Qur'an ila upotevu na matamano.

**Ni machache mnayoyakumbuka** na hali mnawaidhika na mawaidha ya Mwenyezi Mungu na nasaha zake. Kwa sababu nyinyi hamwogopi mwisho utakuwaje; na anayewaidhika ni yule anayeogopa.

Kauli yake ‘ni machache mnayoyakumbuka’ ni kuashiria uchache wa wale wanaowaidhika.

﴿ ٤ ﴾ وَكَمْ مِّن قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا فَجَاءَهَا بَأْسُنَا بَيَاتًا أَوْ هُمْ قَائِلُونَ

4. Na vijiji vingapi tuliangamiza; ikafikia adhabu yetu usiku au katika wakati wa kailula.

﴿ ٥ ﴾ فَمَا كَانَ دَعْوَاهُمْ إِذْ جَاءَهُمْ بَأْسُنَا إِلَّا أَنْ قَالُوا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ

5. Basi hakikuwa kilio chao, ilipowafikia adhabu yetu, ila kusema: Hakika sisi tulikuwa madhalimu.

﴿ ٦ ﴾ فَلَنَسْأَلَنَّ الَّذِينَ أُرْسِلَ إِلَيْهِمْ وَلَنَسْأَلَنَّ الْمُرْسَلِينَ

6. Kwa hakika tutawauliza wale waliopelekwa (Mitume) na pia kwa hakika tutawauliza (Mitume) waliopelekwa.

﴿ ٧ ﴾ فَلَنَقُصَّنَّ عَلَيْهِم بِعِلْمٍ وَمَا كُنَّا غَائِبِينَ

7. Tena kwa hakika tutawasimulia kwa ujuzi, wala hatukuwa mbali.

﴿ ٨ ﴾ وَالْوَزْنُ يَوْمَئِذٍ الْحَقُّ فَمَن تَقَلَّتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

8. Na kipimo siku hiyo kitakuwa haki, Basi ambao uzani wao utakuwa mzito, hao ndio wenye kufaulu.

﴿ ٩ ﴾ وَمَن خَفَّتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ بِمَا كَانُوا بِآيَاتِنَا يَظْلِمُونَ

9. Na ambao uzani wao utakuwa hafifu, basi hao ndio waliozitia hasara nafsi zao kwa sababu ya kuzidhulumu Ishara zetu.

﴿ ١٠ ﴾ وَلَقَدْ مَكَّنَّاكُمْ فِي الْأَرْضِ وَجَعَلْنَا لَكُمْ فِيهَا مَعَايِشَ قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ

10. Na hakika tumewamakinisha katika ardhi na tukawawekea humo mahitaji ya maisha, Ni shukrani ndogo mnazotoa.

## **NA MIJI MINGAPI TULIANGAMIZA**

### **Aya 4-10**

#### **MAANA**

Na miji mingapi tuliangamiza; ikafikia adhabu yetu usiku au katika wakati wa kailula<sup>1</sup>.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kumwamrisha Mtume wake Mtukufu kuonya kwa Qur'an na kuamrisha watu kuifuata, katika Aya hii, anataja maangamizo ya waliopita ambao aliwaangamiza kwa sababu ya kupinga

1 Kulala wakati wa mchana, nyakati za aduhuri

kwao Mwenyezi Mungu na kukadhibisha Mitume yake, na kwamba yeye Mwenyezi Mungu aliwateremshia adhabu usiku au wakati wa kailula, mchana, ambao ni wakati wa raha na amani, ili adhabu iwaumize zaidi.

Wafasiri wengi wanasema kuwa kaumu ya Nabii Lut walijiwa na adhabu usiku. Nami nashangaa sijui wameyatoa wapi haya, na Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

﴿...إِنَّ مَوْعَدَهُمُ الصُّبْحُ أَلَيْسَ الصُّبْحُ بِقَرِيبٍ﴾ (٨١)

“Hakika miadi yao ni asubuhi, Je, asubuhi si karibu” (11:81).

Kuna kikundi cha wafasiri waliosema kuwa kuna mageuzi ya kutanguliza maneo katika Aya hii tunayoifasiri; Kwa sababu kuangamia kunakuja baada adhabu, Kwamba isomeke hivi: Ni miji mingapi ilifikiwa na dhabu yetu tuliangamiza? Razi ametaja njia tatu za kuawili Aya hii na Tabrasi akazidisha ya nne.

Ilivyo hasa ni kuwa hakuna wajibu wowote wa kupangilia maneno kulingana na maana ya hali halisi, ikiwa utaratibu wa hali halisi uko wazi na unajulikana na wote; kama ilivyo katika Aya. Na herufi ‘Fa’, kama ambavyo inakuja kwa maana ya kufuatisha, vilevile inakuja ikiwa ni ya ziada na ya kufasiri, Hapa, herufi ‘Fa’ inafasiri aina ya maangamivu waliyoyapata washirikina.

Basi hakikuwa kilio chao, ilipowafikia adhabu yetu, ila kusema: Hakika sisi tulikuwa madhalimu.

Washirikina walikuwa wakitambika kwa majina ya masanamu wakiwa wameamini kabisa. Lakini walipoona adhabu walijitenga na waungu wao na wakaelekea kwa Mwenyezi Mungu wakikiri ukafiri na ushirikina wao, lakini ni baada ya kukatika taklifa zote na kufungwa mlango wa toba.

Kwa hakika tutawauliza wale waliopelekewa (Mitume) na pia kwa hakika tutawauliza (Mitume) waliopelekwa.

Baada ya Mwenyezi Mungu kuelezea maangamivu yao duniani anaelezea kuwa wao wataulizwa huko akhera na wataulizwa Mitume pia, wawatolee ushahidi.

Tena kwa hakika tutawasimulia kwa ujuzi, wala hatukuwa mbali.

Mwenyezi Mungu hatatosheka na kuwauliza tu na kuwauliza Mitume, bali yeye pia atawasomea kila kitu walichokisema na kukifanya:

يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ جَمِيعًا فَيُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُوا أَحْصَاهُ اللَّهُ وَنَسُوهُ وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ

﴿شَهِيدٌ﴾ (٦)

“Siku Mwenyezi Mungu atakapowafufua wote, awaambie yale waliyoyatenda; Mwenyezi Mungu ameyadhibiti, na wao wameyasahau; na Mwenyezi Mungu ni shahidi wa kila kitu.” (58:6)

Mkusudio yake ni kuwatia msukosuko watambue nakama ya Mwenyezi Mungu na ghadhabu yake kwao, yakiwa ni malipo ya uasi na ukaidi wao.

## MIZANI YA MATENDO

Na kipimo siku hiyo kitakuwa haki.

Maneno yamekuwa mengi kuhusu hakika ya mizani ambayo atapimia Mwenyezi Mungu matendo ya watu; mpaka baadhi ya watu wakasema kuwa mizani hiyo itakuwa na mikono miwili.

Tunavyofahamu sisi kuhusu mizani hii – na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi – ni kuwa ni kipimo ambacho kitampambanua mtiifu na mwasi na mwema na mwuovu. Kipimo chenyewe ni amri ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake.

Ukifika wakati wa Hisabu, huangaliwa aliyoyafanya na aliyoyaacha mwanaadamu, na hulinganisha kati ya aliyoamrisha na Mwenyezi Mungu kuyafanya na aliyoyaacha. Vitendo vyake vikifuatana na amri ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake, basi atakuwa ni katika waliofaulu, na kama si hivyo atakuwa ni katika wale ambao uzani wao umekua hafifu na kuwa katika madhalimu waliojahasiri wenyewe na adhabu ya moto.

Kwa maneno mengine ni kwamba kila kitu katika maisha haya kina misingi na udhibiti wake, iwe ni sayansi, fasihi au fani yoyote nyingine. Na kwayo hutofautiana na kingine, bali uzuri wake na ubaya wake unajulikana kutokana na misingi hiyo.

Misingi hiyo na udhibiti huo inaitwa mizani, makisio, njia na mwamuzi. Basi hivyo hivyo hisabu katika akhera ina misingi na udhibiti ambao Qur'an imeipa jina la Mizan na Swirat.

Kwa hiyo misingi hii au Mizani hii ya matendo ya watu ni amri ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake. Kazi yake katika kumhukumu mtu kesho, ni kama kazi ya fiqhi na kanuni katika kuhukumiwa mshitakiwa katika maisha ya hapa duniani.

**Basi ambao uzani wao utakuwa mzito.**

Nao ni wale ambao matendo yao yamelingana na misingi ya amri za Qur'an na makatazo yake yakawa makamilifu.

**Hao ndio wenye kufaulu.**

Kwa sababu hawakuanguka mtihani.

**Na ambao uzani wao utakuwa hafifu.**

Nao ni wale ambao umedhihirika umbali baina ya matendo yao na hukumu za Mwenyezi Mungu na mafunzo yake.

**Basi hao ndio waliozitia hasara nafsi zao kwa sababu ya kuzidhulumu Aya zetu.**

Wafasiri wengi wamesema kuwa makusudio ya kuzidhulimu hapa ni kuzikufuru, lakini sawa ni kukadhibisha Aya za Mwenyezi Mungu kwa hali yoyote, kama inavyoonyesha Aya yenyewe, ni sawa Aya hizo ziwe zinafahamisha umoja wa Mwenyezi Mungu, ujumbe wa Mitume yake, ufufuo au halali yake na haramu yake.

**Na hakika tumewamakinisha katika ardhi na tukawawekea humo mahitaji ya maisha, Ni shukrani ndogo mnazotoa.**

Baada ya Mwenyezi Mungu kuwamrisha washirikina kufuata waliyoteremshiwa, na kuwahofisha na adhabu ya dunia na akhera, sasa anawakumbusha neema yake kwao; na kwamba yeye ndiye aliyewaweka katika ardhi hii akawapa uwezo wa kuitumia kwa maslahi yao.

Mmoja wa wafasiri wa kisasa anasema: “Lau si Mwenyezi Mungu kumakinisha mtu katika ardhi hii, asingeliweza kiumbe huyu dhaifu kuyamudu maumbile”.

وَلَقَدْ خَلَقْنَاكُمْ ثُمَّ صَوَّرْنَاكُمْ ثُمَّ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ لَمْ

يَكُن مِّنَ السَّاجِدِينَ ﴿١١﴾

11. Na hakika tuliwaumba, kisha tukawatia sura, Kisha tukawaambia Malaika: Msujudieni Adam; Basi waka- sujudu wote isipokuwa Iblisi hakuwa miongoni mwa walio- sujudu.

﴿ قَالَ مَا مَنَّكَ إِلَّا تَسْجُدَ إِذْ أَمَرْتُكَ قَالَ أَنَا خَيْرٌ مِنْهُ خَلَقْتَنِي مِنْ نَارٍ وَخَلَقْتَهُ مِنْ طِينٍ ﴾ (١٢)

12. Akasema (Mwenyezi mungu): Nini kilichokuzuia kumsujudia nilipokuamrisha? Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye, umeniumba kwa moto naye umemuumba kwa udongo.

﴿ قَالَ فَاهْبِطْ مِنْهَا فَمَا يَكُونُ لَكَ أَنْ تَتَكَبَّرَ فِيهَا فَاخْرُجْ إِنَّكَ مِنَ الصَّاغِرِينَ ﴾ (١٣)

13. Akasema: Basi shuka kutoka huko, haikufalii kufanya kiburi humo. Basi toka, hakika wewe ni miongoni mwa walio duni.

﴿ قَالَ أَنْظِرْنِي إِلَى يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴾ (١٤)

14. Akasema: Nipe muda mpaka siku watakapofufuliwa.

﴿ قَالَ إِنَّكَ مِنَ الْمُنظَرِينَ ﴾ (١٥)

15. Akasema (Mwenyezi mungu): Utakuwa katika waliopewa muda.

﴿ قَالَ فَبِمَا أَغْوَيْتَنِي لَأَقْعُدَنَّ لَهُمْ صِرَاطَكَ الْمُسْتَقِيمَ ﴾ (١٦)

16. Akasema: Kwa kuwa umenipoteza, basi hakika nitawakalia katika njia yako.

﴿ ثُمَّ لَا تَيَسَّرُ لِمَنْ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ وَعَنْ أَيْمَانِهِمْ وَعَنْ شَمَائِلِهِمْ وَلَا تَجِدُ أَكْثَرَهُمْ

﴿ شَاكِرِينَ ﴾ (١٧)

17. Kisha hakika nitawaandea kwa mbele yao na nyuma yao na kuumeni kwao na kushotoni kwao; wengi katika wao hutawakuta wenye kushukuru.

﴿ قَالَ اخْرُجْ مِنْهَا مَذْءُومًا مَدْحُورًا لَمَنْ تَبِعَكَ مِنْهُمْ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنْكُمْ أَجْمَعِينَ ﴾ (١٨)

18. Akasema: Toka humo, hali ya kuwa ni mwenye kufedheheka na mwenye kufukuzwa. Atakayekufuata miongoni mwao, basi hakika nitaijaza Jahannam kwa nyinyi nyote.

## NA HAKIKA TULIWAUMBA

Aya 11-18

### ASILI YA MTU

#### MAANA

Na hakika tuliwaumba, kisha tukawatia sura.

Maneno haya wanaambiwa wanaadamu, Maana ya ‘tuliwaumba’ ni kuwa yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu aliianzisha asili yetu ya kwanza kutokana na mchanga na sisi akatutoa kutokana na tone la manii ambalo linaishia kwenye mchanga. Makusudio ya tuliwatia sura ni kwamba yeye amejaalia mada ya kwanza aliyotuumba kwayo kuwa ni mtu kamili; kama alivyosema:

﴿... أَكْفَرْتِ بِالَّذِي خَلَقَكَ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ مِنْ نُطْفَةٍ ثُمَّ سَوَّاكَ رَجُلًا ﴾ (٣٧)

“Je, unamkufuru yule aliyekuumba kwa udongo, tena kwa tone la manii, kisha akakufanya mtu kamili?. (18:37).

Kwa hiyo tofauti baina ya kuumba na kutia sura ni kwamba kuumba maana yake ni kukipatisha kitu na kukianzisha. Ama kukitia sura ni kukipa kitu sura hasa baada ya kukianzisha.



**Unaweza kuuliza kuwa:** wafuasi wa Darwin wanasema kwamba mtu kwanza alipatikana katika sura isiyokuwa hii aliyo nayo sasa; kisha ikageukageuka mpaka kufikia ilivyo sasa.

**Jibu:** sisi tuko pamoja na dalili za kielimu zisizokubali shaka na dhana za kupinga; Kwa sababu pale tu inapozuka dhana, basi dalili hubatilika. Hii ni hakika ya ubainifu iliyo wazi hawaipingi hata wenye nadharia ya majaribio ambao wamesema chimbuko la maarifa ni lazima litokane na majaribio ya kuhisi.

Dalili kubwa waliyoitegemea wenye nadharia ya mageuzi ni ufukuaji wa vitu vya kale; kuwa wamegundua aina za wanyama, wengine ni bora zaidi. Na kwamba muda wa wale waliokuwa bora zaidi umechelewa kuliko wa wale walio duni na kwamba kuna kushabihiana na binadamu katika mambo mengi.

Sisi hatupingi ugunduzi huu lakini, hauthibitishi nadharia ya Darwin, Kwa sababu hauleti uhakika usio na shaka kuwa aliye bora amekuwa kutokana na aliye duni, bali hilo haliwezekani na inawezekana kuwa kila mmoja kati ya aliye bora na duni ni aina nyingine iliyopatikana kutokana na hali inayo afikiana nayo, kisha ikatoweka wakati ilipobadilika hali yake, kama zilivyotoweka aina nyinginezo za wanyama na mimea.

Ikiwa mambo mawili yanawezekana, basi kuchukua moja tu, na kuacha jingine ni kujichukulia madaraka.

Katika niliyoyasoma ni kwamba wataalamu wengi, wakiwemo walahidi, walikuwa wakiamini nadharia ya Darwin, lakini walipoingia katika nyanja za elimu wakabadilika kutokana na yale tuliyoyataja; na kwamba mtu ana aina pekee za kiakili na kiroho zinzohusiana naye, zinazomfanya awe tofauti na viumbe vingine.

**Kisha tukawaambia Malaika: Msujudieni Adam, Basi wakasujudu wote isipokuwa Iblisi hakuwa miongoni mwa waliosujudu.**

Umetangulia mfano wake katika Juz.1 (2:82)

**Akasema: Nini kilichokuzuia kumsujudia nilipoamrisha?**

Makusudio ya kusujudu hapa ni kusujudu kwa kimaamkuzi, sio kwa kiibada, nako ni kumtii Mwenyezi Mungu, kwa sababu ni amri yake.

**Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye, umeniumba kwa moto naye umemuumba kwa udongo.**

Chochote akifanyacho Iblisi, lazima atakitafutie visibabu; na sharti la msingi la kila kisababu katika mantiki yake ni kukhalifu matakwa ya Mwenyezi Mungu na radhi yake. Hiyo ndiyo asili ya kwanza anayoitegemea Iblis katika kauli zake na vitendo vyake.

Fakihi anajitahidi kufanya utafiti ili aongoke kwenye hukumu alizoziwekea sharia Mwenyezi Mungu, lakini Iblisi kwake yeye sharia za hukumu ni zile zenye msingi wa “Mwenyezi Mungu anasema hivyo nami nasema hivi.”

Mwenyezi Mungu alimwamuru Iblisi amsujudie Adam, lakini akakataa wala asiombe msamaha, bali alijigamba kwa kusema: “Vipi nimsujudie ambaye mimi ni mbora wake.” Kama kwamba anamwambia Mwenyezi Mungu Mtukufu: Ilikuwa wafaa wewe umwamuru Adam anisujudie mimi, sio mimi nimsujudie yeye.

Kwa hivyo utukufu, kwa mantiki ya Iblis ni kwa kuangalia asili, sio kwa kumcha Mwenyezi Mungu; na kwa Mwenyezi Mungu ni vitendo na takua si kwa asili. Na elimu kwa Iblis ni kukisia (Qiyasi) na matamano; na kwa Mwenyezi Mungu ni Wahyi na hukmu ya kiakili ambayo uwazi wake haufanyi kutofautiana watu wawili.

Kwa hiyo, mwenye kuangalia asili yake au akaifanyia kiasi dini kwa rai yake, basi atakuwa amemfuata Iblis atake asitake.

Mwenye Tafsir Al-Manar anasema: “Imepokewa Hadith kutoka kwa Jafar As-sadiq, kutoka kwa baba yake, naye kutoka kwa babu yake kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amesema: “Wa kwanza aliyeifanyia makisio (qiyas) dini ni Iblis, Mwenyezi Mungu alimwambia amsujidie Adam, yeye akasema ni bora kuliko huyo”

Kisha akaendelea kusema Jafar: “Mwenye kulifanyia makisio (qiyas) jambo la dini, Mwenyezi Mungu atamkutanisha na Iblis siku ya kiyama.”

**Utauliza:** Aya hii inafahamisha kuwa uhai unapatikana kutokana na moto kama vile Aya nyingine isemayo:

﴿١٥﴾ وَخَلَقَ الْجَانَّ مِنْ مَّارِجٍ مِنْ نَّارٍ

“Na akaumba majini kwa ulimi wa moto” (55:15)

Na Aya nyingine inasema:

﴿٣٠﴾ وَجَعَلْنَا مِنَ الْمَاءِ كُلَّ شَيْءٍ حَيٍّ

“Na tukafanya kwa maji kila kitu kilicho hai” (21:30)

**Jibu:** Vitu hai vilivyotajwa katika Qur’an tukufu viko aina nyingi: Kuna ulimwengu wa Malaika, wa majini na vile vilivyomo katika ardhi hii. Aina hii ya tatu ndiyo ambayo uhai wake uko katika maji, kama vile wanyama, mimea na watu. Hiyo ndiyo iliyokusudiwa kiujumla katika kauli yake Mwenyezi Mungu: ‘Na tukafanya kwa maji kila kitu kilicho hai.’

Na kuna viumbe vingine ambavyo uhai wake uko katika moto. Kwa maneno mengine ni kwamba maji ni lazima kwa maisha ya mwanaadamu kulingana na maumbile yake, pia wanyama na mimea. Lakini hii haikanushi kuwa kuna viumbe vingine ambavyo moto ni lazima katika maisha yao. Wataalamu wa elimu ya wadudu wanasema: Kuna aina ya wadudu ambao maisha yao yanategemea hewa ya sumu na visima vya mafuta (Petroli)!

**Akasema:** Basi shuka kutoka huko, haikufalii kufanya kiburi humo. Basi toka, hakika wewe ni miongoni mwa walio duni.

Imesemeka kuwa dhamir ya ‘huko’ inarudia Pepo, Wengine wakasema ni mbinguni. Sisi hatujishughulishi na ufafanuzi ikiwa haukutajwa katika Qur’an wala Hadith, tunatosheka na ujumla.

Mfumo wa maneno unaonyesha kwamba dhamir inarudia kwenye daraja ya juu mbele ya Mwenyezi Mungu; maana yakiwa kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimfukuza Iblis kutoka katika rehema yake hadi kwenye laana yake, ikiwa ni malipo ya kiburi chake na kujizuilia kwake kumtii Mwenyezi Mungu. Kwani kumsujudia Adam ni amri ya Mwenyezi Mungu na ni kumtii Mwenyezi Mungu na sio Adam. Kila anayejiona kuwa sawa ni kukataa hukumu ya Mwenyezi Mungu, basi anastahiki laana mpaka siku ya malipo.

**Akasema:** Nipe muda mpaka siku watakapofufuliwa.

Iblis alikuwa na haja nafsini mwake - atakayoifafanua - ya kutaka kupewa muda.

**Akasema** - Mwenyezi Mungu Mtukufu -: **Utakuwa katika waliopewa muda.** Inasemekana Iblis alitaka muda mpaka siku ambayo watafufuliwa wafu wote kwa ajili ya hisabu na malipo, Mwenyezi Mungu akakataa maombi haya, akampa muda mpaka siku ya kufa wote walio hai, ambao umeashiriwa na Aya isemayo:

﴿ ٣٧ ﴾ إِلَى يَوْمِ الْوَقْتِ الْمَعْلُومِ ﴿ ٣٨ ﴾

“Akasema: Hakika wewe ni katika waliopewa muda mpaka siku ya wakati maalum” (15: 37 – 38).

Na siku hiyo ni ile saa ya kupuziwa Parapanda ambayo imeelezwa na Aya isemayo:

﴿ ٦٨ ﴾ وَرَفِخَ فِي الصُّورِ فَصَعِقَ مَنْ فِي السَّمَاوَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ ﴿ ٦٩ ﴾

“Na itapulizwa parapanda watoke roho waliomo ardhini na waliomo mbinguni ...” (39: 68)

**Akasema:** Kwa kuwa umenipoteza, basi hakika nitawakalia katika njia yako iliyonyooka.

Iblis alijiwekea mkakati kuwa atalipizia kisasi kwa kiumbe huyu aliyekuwa ni sababu ya kufukuzwa kwake kutoka katika rehema ya Mwenyezi Mungu kwenda kwenye laana. Akabainisha aina hii ya kujilipiza kwamba yeye ataikalia na kuziba njia, kwa Adam na kizazi chake, ile ilelekeayo kwa Mwenyezi Mungu na kwenye twaa yake.

**Kisha hakika nitawaendea kwa mbele yao na nyuma yao na kuumeni kwao na kushotoni kwao; wengi katika wao hutawakuta wenye kushukuru.**

Kuwaendea kwake kwa pande hizi nne ni fumbo la ushawishi wake na jitihada yake katika kuwapoteza, kiasi ambacho hataacha maasi yoyote ila huwahada kwayo, wala twaa yoyote ila huwazuia.

Mwenyezi Mungu akiwaamrisha jihadi na kujitolea mhanga, basi Iblisi huwapendekezea uhai. Na kama Mwenyezi Mungu (s.w.t) akiwahimiza kujitolea mali katika njia yake Mwenyezi Mungu, basi mlaanifu huyu huwahofisha na ufukara.

Ikiwa Mwenyezi Mungu Mtukufu anawakataza pombe, zinaa na kamari, yeye huwavutia huko kwenye anasa na matamano. Mungu akiwapa kiaga cha moto na kuwaahidi Pepo, basi adui huyu wa Mwenyezi Mungu huwaambia, hakuna Pepo wala moto.

Basi namna hii huhisabu kila haki kuwa ni batil na kila msimamo kuwa ni kombo. Hii inafanana kabisa na wale waliouza dini yao kwa shetani wakiboresha vitendo vya wakoloni, wakiua wanawake na kuwafukuza wasio na hatia nchini mwao.

**Akasema:** Toka humo, hali ya kuwa ni mwenye kufedheheka na mwenye kufukuzwa.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemhusisha Iblisi na kufedheheka na kufukuzwa kwa kuwa yeye Mwenyezi Mungu alimteremsha cheo alichokuwa nacho.

Atakayekufuata miongoni mwao, basi hakika nitaijaza Jahannam kwa nyinyi nyote.

Yaani Jahannam itakuwa yake na wanachama wake waliomfuata. Aya hii ni kama ile isemayo:

لَأْمَلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنْكَ وَمِمَّن تَبِعَكَ مِنْهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٨٥﴾

“Kwa hakika nitajaza Jahannam kwa wewe na wale wanaokufuata miongoni mwao wote” (38:85)

Hapa kuna maswali yanayotaka kujibiwa:

1. **Kwanza**, Je, maneno yalikuwa ni moja kwa moja au ni kwa kupitia hali fulani?

2. **Pili**, kauli ya Iblis: “Umenipoteza” inafahamisha kwamba kupotea kwake kulitokana na Mwenyezi Mungu, vipi atamwadhibu?

3. **Tatu**, kwa nini Mwenyezi Mungu amempa muda Iblis naye anajua ufisadi wake na kuwaharibu wengine?

Tutajibu maswali haya matatu kwa ufupi sana:

**Jibu** la kwanza, ni kuwa sisi tunaamini kuweko kwa majibizano hayo, kwa vile Wahyi umefahamisha hilo na akili hailipingi hilo, na si juu yetu kufanya utafiti wa aina ya majibizano hayo yalivyokuwa, maadamu Wahyi haukufafanua.

Kuhusu jibu la pili, upotevu unatokana na Iblis, na wala hautokani na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Iblis mwenyewe amekiri kuwa yeye ni mpotezaji katika Aya isemayo:

وَلَأَعُوْبَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٣٩﴾ إِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ الْمُخْلَصِينَ ﴿٤٠﴾

“Na nitawapoteza wote isipokuwa waja wako waliosafishwa” (15:39 – 40)

Na vipi Mwenyezi Mungu ampoteze mja kisha amwadhibu kwa upotevu? Mwenyezi Mungu ametakata kabisa na hayo.

Ama kauli ya Iblis “Umenipoteza” Maana yake ni kwa kuwa umenifanyia mtihani wa kuniamrisha kumsujudia Adam, mtihani ambao umeniingiza katika uovu na uasi, basi nami nitafanya hivi na vile. Kwa maneno mengine ni kuwa Iblis anasema kwa kuwa umeniamrisha na nikaasi amri yako, basi sitamwacha yeyote atii amri yako.

**Jibu** la swali la tatu ni kuwa: matakwa ya Mwenyezi Mungu yamehukumia kumpa mtu akili, ukumbusho kupita utume, uwezo wa kufanya kheri na shari na kumwachia hiyari na kumjaribu kwa matamano na hadaa ana- zoshawishiwa na Iblis na majeshi yake; ili kumpambanua mwema na mwovu na mwenye ikhlas na mwenye khiyana.

Kwa maelezo zaidi angalia Juz.7 (5:94) kifungu ‘Maana ya mtihani wa Mwenyezi Mungu.’

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

وَيَا آدَمُ اسْكُنْ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ فَكُلَا مِنْ حَيْثُ شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا هَذِهِ الشَّجَرَةَ فَتَكُونَا مِنَ

الظَّالِمِينَ ﴿١٩﴾

19. Na Ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani (Pepo); na kuleni humo maridhawa popote mpendapo, wala msiukurubie mti huu msije mkawa miongoni mwa waliodhulumu (nafsi zao).

فَوَسْوَسَ لَهُمَا الشَّيْطَانُ لِيُبْدِيَ لَهُمَا مَا وُورِيَ عَنْهُمَا مِنْ سَوَاتِهِمَا وَقَالَ مَا نَهَاكُمَا رَبُّكُمَا عَنْ أَنْ

هَذِهِ الشَّجَرَةَ إِلَّا أَنْ تَكُونَا مَلَكَتَيْنِ أَوْ تَكُونَا مِنَ الْخَالِدِينَ ﴿٢٠﴾

20. Basi shetani aliwatia wasiwasi ili kuwafichulia tupu zao walizofichiwa. Na akasema: Mola wenu hakuwakataza mti huu ila msije mkawa Malaika au kuwa miongoni mwa wakaao milele.

وَقَاسَمَهُمَا إِنِّي لَكُمَا لَمِنَ النَّاصِحِينَ ﴿٢١﴾

21. Na akawaapia: Kwa hakika mimi ni miongoni mwa watoa nasaha kwenu.

فَدَلَاهُمَا بِغُرُورٍ فَلَمَّا ذَاقَا الشَّجَرَةَ بَدَتْ لَهُمَا سَوَاتُهُمَا ا وَظَفِقَا يَخْضِفَانِ عَلَيْهِمَا مِنْ وَرَقِ الْجَنَّةِ

وَنَادَاهُمَا رَبُّهُمَا أَلَمْ أَنْهَكُمَا عَنْ تِلْكَ الشَّجَرَةِ وَأَقُلْ لَكُمَا إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُمَا عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿٢٢﴾

22. Basi akatelezeshwa kwa hadaa. Walipouonja mti ule, tupu zao ziliwadhihirikia, wakaanza kujibandika majani ya kwenye Bustani (Pepo), Na Mola wao akawaita: Je, sikuwakataza mti huo na kuwaambia kwamba shetani ni adui yenu wa dhahiri?

قَالَ رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنْفُسَنَا وَإِنْ لَمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٢٣﴾

23. Wakasema: Mola wetu! Tumedhulumu nafsi zetu; na kama hutatughufiria na kuturehemu tutakuwa miongoni mwa waliohasirika.

قَالَ اهْبِطُوا بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ وَلَكُمْ فِي الْأَرْضِ مُسْتَقَرٌّ وَمَتَاعٌ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٢٤﴾

24. Akasema: Shukeni, nyinyi kwa nyinyi ni maadui. Na makao yenu na starehe yatakuwa katika ardhi kwa muda.

قَالَ فِيهَا تَحْيَوْنَ وَفِيهَا تَمُوتُونَ وَمِنْهَا تُخْرَجُونَ ﴿٢٥﴾

25. Akasema: Mtaishi humo na mtafia humo na mtatolewa kutoka humo.

### NA WEWE ADAM KAA PEPO NI PAMOJA NA MKEO

Aya 19 – 25

#### MAANA

Na Ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani (Pepo); na kuleni humo maridhawa popote mpendapo, wala msiukurubie mti huu; msije mkawa miongoni mwa waliodhulumu (nafsi zao).

Imepita tafsir yake kwa ufafanuzi katika Juz.1 (2:35).

Basi shetani aliwatia wasiwasi ili kuwafichulia tupu zao walizofichiwa.

Maana ya walizofichiwa ni kuwa kila mmoja hakuweza kuona tupu yake wala ya mwenziwe. Hatujui wasiwasi wa shetani ulikuwaje, lakini

tunaamini kuwa mawazo yoyote, kauli au kitendo chochote kinachokikingama katika njia ya uhai basi kinatokana na mawazo ya shetani.

Vyovyote iwavyo ni kwamba shetani alidhihirisha nasaha kwa Adam na Hawa na akaficha uwongo. Na dhahiri ya Aya inaonyesha kuwa Iblisi alikuwa akijua kwamba mwenye kula mti huu basi atakuwa uchi na kwamba mwenye kuwa uchi hufukuuzwa Peponi; na ndio akafanya hila hiyo ya kuwatoa Peponi na akasema:

Mola wenu hakuwakataza mti huu ila msije mkawa Malaika au kuwa miongoni mwa wakaaao milele. Na akaawapia: Kwa hakika mimi ni miongoni mwa watoa nasaha kwenu.

Mlaanifu alibadilisha mambo kichwa chini miguu juu, aliapa kwamba yeye anawanasihi, na hali yeye ni adui mhasimu. Akaapa kuwa wao wakila mti watakuwa katika watakaokaa milele, naye anajua wazi kuwa mwisho wa kula huko ni kufukuzwa na mauti. Hivi ndivyo wafanyavyo mashetani wa kibinadamu, huwatia mawazo wenye akili ndogo, wakaona mangati ni maji na maji ni mangati.

Basi akawatelezesha kwa hadaa.

Yaani, baada ya Shetani kuwapia Adam na Hawa kwamba yeye ni mtoaji nasaha aliye mwaminifu walimwitikia hadaa zake wakidhani kuwa hakuna yeyote anayeweza kuapa kwa Mungu uwongo. Kwa sababu mlaanifu huyu ndiye wa mwanzo kuthubutu kula kiapo cha uwongo; kama ambavyo yeye ndiye wa kwanza kujinaki kwa asili yake na ndiye wa kwanza kukisia kwa rai yake.

Walipouonja mti ule, tupu zao ziliwadhihirikia, wakaanza kujibandika majani ya kwenye Bustani (Pepo)

Yaani walipokula mti kila mmoja akaiona tupu ya mwenziwe, ambapo mwanzo zilikuwa zimesitiriwa, wakatahayari na wakaona iko haja ya kujisitiri. Wakaanza kukusanya majani ya mti wa Peponi na kuyaweka kwenye tupu zao.

Na Mola wao akawaita: Je, sikuwakataza mti huo na kuwaambia kwamba Shetani ni adui yenu wa dhahiri?

Hii ni lawama kwa Adam na mkewe kutoka kwa Mwenyezi Mungu kutokana na kughurika kwao na kauli ya Iblisi, na udhaifu wa kukabiliana na upotevu wake; wakati huo huo akitanabahisha wajibu wa kutubia na kurejea.

Kwa hiyo ndio wakaharakisha kukiri dhambi na kuomba maghufira, wakasema:

Mola wetu! Tumedhulumu nafsi zetu; na kama hutatughufiria na kuturehemu tutakuwa miongoni mwa waliohasirika.

Na Mwenyezi Mungu alighufiria na kurehemu, kwa dalili ya Aya isemayo:

فَتَلَقَىٰ آدَمَ مِنْ رَبِّهِ كَلِمَاتٍ فَتَابَ عَلَيْهِ إِنَّهُ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿٣٧﴾

“Akapokea Adam maneno kutoka kwa Mola wake na Mola wake akapokea toba yake; hakika Yeye ni Mwingi wa kukubali toba, Mwenye kurehemu.” Juz, 1 (2:37).

Akasema (Mwenyezi Mungu): Shukeni, nyinyi kwa nyinyi ni maadui.

Maneno haya anaambiwa Adam, mkewe na Iblisi. Makusudio ya nyinyi ya kwanza ni Iblis na kabila yake, na ya pili ni Adam na kizazi chake. Sababu ya uadui huu ni kuwa Iblisi alikusudia kumpoteza mtu na kumharibu kwa kuchukua kisasi cha maafa yake.

Ama mtu hamwoni Iblisi kuweza kumpa udhia, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

إِنَّهُ يَرَاكُمْ هُوَ وَقَبِيلُهُ مِنْ حَيْثُ لَا تَرَوْنَهُمْ ﴿٢٧﴾

“Hakika yeye na kabila lake anawaona, na nyinyi hamuwaoni.” (7:27)

Na akasema tena:

إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُمْ عَدُوٌّ فَاتَّخِذُوهُ عَدُوًّا ﴿٦﴾

“Kwa hakika Shetani ni adui yenu, basi mfanyeni adui” (35:6)

Na makao yenu na starehe yatakuwa katika ardhi kwa muda. Akasema mtaishi humo na mtafia humo na mtatolewa kutoka humo.

Hivi ndivyo alivyotuandikia Mwenyezi Mungu, baada ya kutokea yaliyotokea kwa Adam, kwamba tuishi na tufe katika ardhi hii, kisha tutolewe humu kwa ajili ya hisabu na malipo baada ya kupata taabu na mashaka.

#### **KISA CHA ADAM KAMA KILIVYO KATIKA QUR'AN**

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja kisa cha Adam, Katika Juz.1 (2:33) na Aya zinazofuatia, Juz.8. (7:18) na Aya zinazofuatia, na katika Juz.16 (20:116) na Aya zinazofuatia.

Muhtasari wa kisa chenye, kama kilivyoielezwa katika Aya hizo, ni huu ufuatao:

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwafahamisha Malaika wake kwamba yeye ataumba viumbe katika ardhi hii, watakaotembea katika pande zake zote na kula riziki yake. Na Malaika wakamwambia: Vipi unataka kuweka katika ardhi atakayefanya ufisadi na kumwaga damu kwa kushindania matunda yake; na sisi hapa tuko, tukikuabudu wewe milele? Mwenyezi Mungu akawapa jibu la kutuliza nyoyo zao na kuwataka wamsujudie Adam alipomkamilisha kuwa mtu.

Baada ya kwisha kumuumba kutokana na mchanga na kumweka sura ya mwisho, Malaika walimuadhimisha na kumsujudia, isipokuwa Iblisi akadhahirisha uasi na akatangaza jeuri.

Mwenyezi Mungu alipomuuliza akasema: “Mimi ni bora kuliko yeye.” Mwenyezi Mungu akampa malipo ya kumfukuza na laana.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimfundisha Adam majina ya viumbe vyote, ambapo Malaika walikuwa hawayajui, Mwenyezi Mungu akaamwamuru Adam awaambie, ili kubainisha ubora wake na kudhahirishaa hekima yake Mungu, ya kumweka Adamu kuwa khalifa katika Ardhi.

Mwenyezi Mungu akamfanyia Adam mke kutokana jinsi yake, Akawakalisha kwenye Bustani (Pepo) ya neema zake, akawaruhusu kula matunda yote na akawakataza mti mmoja katika miti yake. Akawapa dhamana, kama wakifuata amri, hawatakuwa na njaa wala kiu au kuwa uchi. Kisha akawatahadharisha na Iblisi na hadaa zake.

Mlanifu Iblisi aliona uchungu yeye kuwa mwovu na kuneemeka yule aliyekuwa ni sababu ya uovu wake na kufukuuzwa kwake kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu. Akawafitini kwa kuwapambia maneno na kuwahadaa.

Walikuwa na kivazi cha kuwasitiri tupu zao, hawajioni wala hawaonani uchi, lakini walipomaliza kula tunda hilo tu, sitara iliwaondoka wakawa uchi. Ndipo wakaharakisha kujifunika kwa majani ya Peponi.

Mwenyezi Mungu, Mtukufu akawalingania huku akiwalaumu, kwa kughafilika na nasaha yake na kusahau hadhari aliyowapa juu ya Iblisi.

Hapo wakanyenyekea kwake kwa kukiri na kujuta huku wakitaka rehema na maghufira. Lakini aliwatoa kwenye neema waliyokuwa nayo na akawakalisha kwenye ardhi hii aliyowafanyia njia mbili: Uongofu na upotevu.

Na akamwahidi Pepo yule atakayefuata uongozi wake; na kumpa kiaga cha moto yule atakayepotea. Akamfahamisha Adam na kizazi chake kwamba uadui baina yao na Iblisi utaendelea mpaka siku ya mwisho na kuwatahadharisha na fitina yake.

Huu ndio muhtasari wa yaliyo katika Qur'an kuhusu kisa cha Adam na mkewe. Kuhusu kisa hiki, watu wana kauli mbili: wale wanaopinga Wahyi na wale wanaouamini. Na hawa nao wako makundi mawili: Kuna kundi lilipetuka dhahiri ya Qur'an, wakategemea ngano za Kiyahudi katika kufasiri Bustani (Pepo) ya Adam na mengineyo.

Kwamba bustani hiyo ilikuwa duniani ikiitwa Bustani ya Aden; na mti aliokula Adam na Hawa ni ngano, na wao walijisitiri na majani ya mti wa Tini; na kwamba Iblisi aliingia kwenye Bustani akiwa ndani ya nyoka na mengineyo yasiyokuwa na asili yoyote ya Hadith wala Qur'an.

Kundi jingine likakimbilia kwenye mambo yasiyohisiwa, Wakafasiri mti kuwa ni mtihani, shetani kuwa ni matamanio, uchi kuwa uchafu na mengineyo katika fahamu za kisufi.

Sisi tuko katikati, tunaamini kiujumla yale yaliyotolewa Wahyi na dhahir ya Qur'an kwamba mti, uchi na majani, yote hayo yalikuwa ni vitu hasa vya kuhisiwa. Kwa sababu ndio ufahamisho wa kihakika wa tamko, wala hakuna la kuwajibisha kuleta taawili, maadam akili inakubali maana ya dhahiri wala haikatai.

Hatuwezi kuzungumzia hakika ya Bustani ya Adam, kwamba ilikuwa hapa duniani au penginepo; wala aina ya majani aliyojisitiria Adam na Hawa, aina ya mti, wala jinsi alivyonyapa Iblisi na kujipenyeza Peponi. Kwa sababu ufafanuzi wa haya ni katika ilimu ya ghaibu wala haukuteremshiwa wahyi na akili inashindwa kufahamu.

Imepokewa kutoka kwa Imam Ahmad amesema: "Mambo matatu hayana asili: Tafsir, mapigano na vita." Anakusudia Tafsir ya Maneno ya Mwenyezi Mungu kwa yasiyokuwa maana ya dhahiri. Kwa sababu yeye ni katika ambao wanatoa dalili kwa dhahiri hii katika msingi na matawi.

يَا بَنِي آدَمَ قَدْ أَنْزَلْنَا عَلَيْكُمْ لِبَاسًا يُؤَارِي سَوْآتِكُمْ وَرِيشًا وَلِبَاسَ التَّقْوَىٰ ذَٰلِكَ خَيْرٌ ذَٰلِكَ مِنْ آيَاتِ اللَّهِ لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ ﴿٢٦﴾

26. Enyi wanadamu! Hakika tumewateremshia vazi lifichalo tupu zenu na vazi la pambo, Na vazi la takua ndiyo bora. Hiyo ni katika Ishara za Mwenyezi Mungu ili wapate kukumbuka.



يَا بَنِي آدَمَ لَا يَفْتِنَنَّكُمُ الشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَجَ أَبَوَيْكُم مِّنَ الْجَنَّةِ يَنزِعُ عَنْهُمَا لِبَاسَهُ مَا لَيْرِيَهُمَا سَوَاتِيمَا إِنَّ بَرَآكُم هُوَ وَقَبِيلُهُ مِنْ حَيْثُ لَا تَرَوْنَهُمْ إِنَّا جَعَلْنَا الشَّيَاطِينَ أَوْلِيَاءَ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٢٧﴾

27. Enyi wanaadamu! shetani asiwatie katika fitina, kama alivyowatoa wazazi wenu katika Bustani (Pepo) akiwavua nguo zao ili kuwaonyesha tupu zao. Hakika yeye na kabila lake anawaona, na nyinyi hamuwaoni. Hakika sisi tumewajaalia mashetani kuwa watawala wa wale ambao hawaamini.

## KIVAZI CHA KUONEKANA NA KISICHOONEKANA

Aya 26 – 27

### MAANA

Katika Sura 6:141, Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja fadhila ya chakula aliyowapa waja wake. Na katika Aya hii tuliyo nayo anataja neema ya kivazi.

Enyi wanadamu! Hakika tumewateremshia vazi lifichalo tupu zenu na vazi la pambo.

Maneno wanaambiwa wanadamu wote, Maana ya kuwateremshia ni kuwapa. Mwenyezi Mungu amewaneemesha waja wake, katika aliyowaneemesha, aina kwa aina za kivazi; kuanzia cha hali ya chini ambacho kinasitiri uchi mpaka cha hali ya juu cha kifahari.

Na vazi la takua ndiyo bora.

Nalo ni kumuogopa Mwenyezi Mungu na kufanya amali njema. Takua imetumiwa kuwa ni vazi kwa sababu imekinga mtu na adhabu ya Mwenyezi Mungu, kama vazi linavyomkinga mtu na joto na baridi, Mwenyezi Mungu anasema “Na amewafanyia nguo za kuwakinga na joto na za kuwakinga na vita vyenu” (16: 81).

Hiyo ni katika Ishara za Mwenyezi Mungu ili wapate kukumbuka.

Yaani Mwenyezi Mungu amewapa kivazi kwa fadhila zake, ili mjue twaa yake na muache kumwasi.

Enyi wanaadamu! Shetani asiwatie katika fitina, kama alivyowatoa wazazi wenu katika Bustani (Pepo) akiwavua nguo zao ili kuwaonyesha tupu zao.

Asi watie katika fitina; yaani msighafilike na fitina yake na hadaa yake. Kuwavua nguo zao ni kuwa yeye alikuwa ni sababu ya kuvuliwa nguo.

Katika Aya iliyotangulia Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameashiria uadui wa Shetani kwa Adam na jinsi alivyomfanyia vitimbi mpaka akamtoa yeye pamoja mkewe kwenye maisha ya raha kwenda kwenye maisha ya tabu na mashaka.

Katika Aya hii Mwenyezi Mungu anawahadharisha wanaadamu wasiingie katika mtego wa Shetani na fitina yake na kuwateka kwenye maasi ili kuwazuia kuingia Peponi; kama alivyowahadaa wazazi wao, na kuwa ni sababu ya kuwa uchi na kutolewa Peponi.

Ilivyo hasa ni kwamba kuzuia kuingia Peponi ni rahisi zaidi kuliko kutoa. Kwani kumtoa mlowezi ni kuzito sana kuliko kumzuia anayetaka kulowea na kukalia ardhi ya watu. Mmoja wa watoaji waadhi anasema:

“Kosa moja tu lilimtoa Adam Peponi baada ya kuingia akiwa mtulivu, je, watoto wake wataingia vipi na hali makosa yamewajaa?”

**Hakika yeye na kabila lake anawaona, na nyinyi hamuwaoni.**

Shetani na majeshi yake anatuona, na sisi hatumuoni hata mmoja, kwa mujibu wa habari hizi za Wahyi, nasi tunauamini.

**Hakika sisi tumewajaalia mashetani kuwa watawala wa wale ambao hawaamini.**

Kifungu hiki kinaashiria jibu la swali la kukadiriwa ambalo ni: Ikiwa Shetani anatuona na sisi hatumuoni, maana yake ni kuwa yeye anatumudu na sisi hatumuwezi na kwamba yeye anaweza kutumaliza wakati wowote akitaka bila kuweza kujikinga naye. Sasa imekuwaje tukaamrisha kujikinga naye na kutomsikiliza?

**Jibu** kwa ufafanuzi zaidi, ni kweli kwamba sisi hatumuoni Shetani, lakini tunahisi athari yake ambayo ni wasiwasi wake ukituambia kuwa hakuna Pepo wala moto na mfano wa hayo.

Mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho huachana na wasiwasi huu wala hautikii; na na anijlinda na yule mwenye kumtia wasiwasi. Kwa hiyo Shetani anarudi akiwa amehizika na kupata hasara.

Ama yule anayemkufuru Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho huingiwa na wasiwasi huu na hutawaliwa na Shetani, hivyo humwongoza vile atakavyo na wakati atakao. Ama waumini hawawezi kusimamiwa na Shetani; Kwa sababu wao wamempa uongozi Mwenyezi Mungu peke yake. Hayo ndio maana ya kauli ya Mwenyezi Mungu:

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ آمَنُوا يُخْرِجُهُمْ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ وَالَّذِينَ كَفَرُوا أُولَئِكَ هُمُ الظَّاغُوتُ  
يُخْرِجُونَهُمْ مِنَ النُّورِ إِلَى الظُّلُمَاتِ ﴿٢٥٧﴾

“Mwenyezi Mungu ni mtawala wa wale walioamini, huwatoa gizani na kuwaingiza katika mwangaza, lakini waliokufuru watawala wao ni mataghuti, Huwatoa kwenye mwangaza, na kuwaingiza katika giza.” Juz.3 (2:257).

Baadhi wafasiri wamesema kuwa mashetani tusiowaona ni viini na virusi vya magonjwa vinavyobebwa na nzi na mbu kumwambukiza mwanadamu. Huzalikana humo na kukua kwa haraka na kusababisha maradhi yasiyoponyeka. Hii ni kufasiri makusudio ya Mwenyezi Mungu kwa kukisia na kubahatisha; na hiyo sio njia yetu kabisa!

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

وَإِذَا فَعَلُوا فَاحِشَةً قَالُوا وَجَدْنَا عَلَيْهَا آبَاءَنَا وَاللَّهُ أَمَرَنَا بِهَا قُلْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ  
أَتَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٨﴾

28. Na wanapofanya machafu husema: Tumewakuta nayo baba zetu na Mwenyezi Mungu ametuamrisha hayo. Sema: Hakika Mwenyezi Mungu haamrishi machafu Je, mnasema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua?

قُلْ أَمَرَ رَبِّي بِالْقِسْطِ وَأَقِيمُوا وُجُوهَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَادْعُوهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ كَمَا بَدَأَكُمْ  
تَعُودُونَ ﴿٢٩﴾

29. Sema: Mola wangu ameamrisha uadilifu. Na elekezeni nyuso zenu katika kila msikiti, na muombeni yeye tu kwa ikhlas kama alivyowaumba kwanza ndivyo mtarudi.

فَرِيقًا هَدَىٰ وَفَرِيقًا حَقَّ عَلَيْهِمُ الضَّلَالَةُ إِنَّهُمْ اتَّخَذُوا الشَّيَاطِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ اللَّهِ  
وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ مُّهْتَدُونَ ﴿٣٠﴾

30. Kundi moja ameliongoa. Na kundi jingine limethibitikiwa na upotofu, Hakika wao wamefanya mashetani kuwa watawala wao badala ya Mwenyezi Mungu, Na wanadhani kwamba wao wameongoka.

### WANAPOFANYA UCHAFU

**Aya 28-30**

#### MAANA

Na wanapofanya machafu.

Dhamir inawarudia wale ambao hawaamini, waliotajwa mwisho wa Aya iliyotangulia. Kundi la wafasiri wamesema kuwa makusudio ya uchafu ni walivyokuwa wakifanya Waarabu wakati wa ujahilia kutufu Al-Kaaba wakiwa uchi, wake kwa waume. Lakini ilivyo hasa ni kuwa neno hilo linaenea yote ya haramu waliyokuwa wakifanya.

Wanapokatazwa husema:

Tumewakuta nayo baba zetu na Mwenyezi Mungu ametuamrisha hayo.

Kitendo cha mababa kimekuwa ni hoja ya washirikina na wengineo; hata kwa maulamaa wengi wa kidini, lakini hawatambui. Ama madai ya washirikina kuwa Mwenyezi Mungu amewaamrisha machafu yameetolewa dalili na Aya isemayo:

“Watasema walioshirikisha: Lau angelitaka Mwenyezi Mungu tusingelimshirikisha sisi wala baba zetu;” Mwenyezi Mungu akawarudi kwa kuwaaambia:

قُلْ هَلْ عِنْدَكُمْ مِّنْ عِلْمٍ فَتُخْرِجُوهُ لَنَا إِنْ تَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ أَنْتُمْ إِلَّا تَخْرُصُونَ ﴿١٤٨﴾

“Je, mnayo elimu mtutolee? Nyinyi hamfuati ila dhana tu, na hamsemi ila uwongo tu.” (6:148).

Na hapa Mwenyezi Mungu akawarudi kwa kusema: Sema:

Hakika Mwenyezi Mungu haamrishi machafu.

Bali “Shetani anawatisha na ufukara na anawaamrisha ubakhili”Juz.3 (2:257)

**Je, mnasema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua?**

Na kila anayesema, bila ya ujuzi wowote, basi ni mzushi mwongo, na ameruka patupu.

**Sema: Mola wangu ameamrisha uadilifu.**

Nao ni usawa na msimamo. Amesema Tabrasi: “Uadilifu ni neno linaloku- sanya kheri zote.” Maana yoyote yatakayokuwa ni kuwa kuamrisha uadilifu ni kupinga madai yao kuwa Mwenyezi Mungu amewaamrisha uovu.

**Na elekezeni nyuso zenu katika kila msikiti, na muombeni yeye tu kwa ikhlas.**

Makusudio ya elekezeni nyuso zenu ni kumwabudu Mwenyezi Mungu. Neno ‘Masjid’ ni mahali pa kusujudia na pia wakati wa kusujudu.

Lakini limetumika sana kwa maana ya jengo maalum la ibada (msikiti) mpaka likawa ni jina lake mahsusi. Makusudio ya kila msikiti sio misikiti yote bali ni msikiti wowote.

Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu anawaamrisha kufanya ibada kwenye msikiti, kwa kumwabudu yeye tu kwa ikhlas katika dini yenu na ibada yenu.

**Kama alivyowaumba kwanza ndivyo mtarudi** kwake siku ya Kiyama kwa ajili ya hisabu na malipo. Hili ni kemeo na onyo kwa yule anayekhalifu aliyoamrisha na Mwenyezi Mungu. Miongoni mwa uadilifu, kufanya ibada na ikhlasi.

**Kundi moja ameliongoa** nao ni wale waliomfanya Mwenyezi Mungu ndiye mtawala wao na wakafuata amri yake na kujizuia makatazo yake, na wala wasihadaike na mambo ya shetani na ubatilifu wake.

**Na kundi jingine limethibitukiwa na upotofu.**

Nao katika akhera wana adhabu kubwa, Hilo ni kuwa Hakika wao wamefanya mashetani kuwa watawala wao badala ya Mwenyezi Mungu, Na anayemfanya shetani kuwa msimamizi badala ya Mwenyezi Mungu basi amepata hasara kubwa.

Na wanadhani kwamba wao wameongoka katika kufanya machafu, kuwafuata mababa na kumzulia Mwenyezi Mungu uwongo. Mwenyezi Mungu anasema:

قُلْ هَلْ نُنَبِّئُكُمْ بِالْأَخْسَرِينَ أَعْمَالًا ﴿١٠٣﴾ الَّذِينَ ضَلَّ سَعِيَّهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَهُمْ يَحْسَبُونَ  
أَنَّهُمْ يُحْسِنُونَ صُنْعًا ﴿١٠٤﴾

**Sema: Je, tuwaambie wenye hasara zaidi kwa vitendo, ni ambao bidii yao imepotea katika maisha ya dunia, nao wanafikiri kuwa wanafanya vyema.”** (18: 103-104).

يَا بَنِي آدَمَ خُذُوا زِينَتَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَكُلُوا وَاشْرَبُوا وَلَا تُسْرِفُوا إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ  
﴿٣١﴾

31. Enyi Wanadamu! Chukueni mapambo yenu katika kila msikiti, na kuleni na kunyweni wala msifanye ufujaji (israf), hakika Yeye hawapendi wafanyao ufujaji (israf).

قُلْ مَنْ حَرَّمَ زِينَةَ اللَّهِ الَّتِي أَخْرَجَ لِعِبَادِهِ وَالطَّيِّبَاتِ مِنَ الرِّزْقِ قُلْ هِيَ لِلَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ  
الدُّنْيَا خَالِصَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ كَذَلِكَ نَفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٣٢﴾

32. Sema: Ni nani aliyeharamisha pambo la Mwenyezi Mungu ambalo amewatolea waja wake, na vilivyo vizuri katika riziki? Sema: Hivyo ni kwa wale walioamini katika maisha ya dunia, ni vyao tu siku ya Kiyama. Namna hii tunazieleza ishara kwa watu wajuao.

قُلْ إِنَّمَا حَرَّمَ رَبِّي الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَّنَ وَالْإِثْمَ وَالْبَغْيَ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَأَنْ تُشْرِكُوا بِاللَّهِ  
مَا لَمْ يُنَزَّلْ بِهِ سُلْطَانًا وَأَنْ تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٣﴾

33. Hakika Mola wangu ameharamisha mambo machafu yaliyodhihirika na yaliyofichika. Na dhambi, na dhulma bila ya haki. Na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na ambacho hakukiteremshia dalili, Na kusema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua.

لِكُلِّ أُمَّةٍ أَجَلٌ فَإِذَا جَاءَ أَجْلُهُمْ لَا يَسْتَأْخِرُونَ سَاعَةً وَلَا يَسْتَقْدِمُونَ ﴿٣٤﴾

34. Kila umma una muda, utakapofika muda wao hawatakawia (hata) saa moja wala hawatatangulia.

## CHUKUENI MAPAMBO YENU

### Aya 31-34

#### MAANA

Enyi Wanadamu! Chukueni mapambo yenu katika kila msikiti

Wafasiri wanasema watu wa wakati wa ujahiliya walikuwa wakitufu Al-Kaaba wakiwa uchi, wake kwa waume: Na walikuwa hawali mafuta wakati wa Hijja; wala hawali chakula ila kiasi tu cha kuzuia tumbo, kwa ajili ya kuadhimisha Hijja, ndipo ikashuka Aya hii.

Na kwamba Mtume (s.a.w.w) alisema: “Baada ya mwaka huu pasihijiwe na mshirikina yeyote wala Al-kaaba haitazungukwa uchi”, basi kauli yake hiyo ikatangazwa kwenye msimu. Miongoni mwa visa vinavavyoingia katika maudhui haya ni kile cha mwanamke mmoja mzuri wa Kiarabu aliyevua nguo na kuweka mkono kwenye tupu yake na akatufu. Macho ya watu yalipompata sana alitunga shairi hili:

Kuona yote au sehemu sihalali kitachoonekana

Kivuli kikubwa adhimu hata akali hamtavuna

Hata mwenye fahamu naye pia hudangana

Akimaanisha kuwa tupu yake ni adhimu pale ilipo, ina haiba na hifadhi, wala hakuna yeyote anayeweza kuifikia; na kwamba yeye anamkemea na kumchukiua anayemwangalia.

Kwa vyovyote itakayokuwa sababu ya kushuka Aya ni kwamba Mwenyezi Mungu ameharamisha kwa mtu kando kuangalia uchi wa mwingine awe mwanamume au mwanamke.

Na amewajibisha kusitiri tupu mbili katika Swala na tawafu.

Makusudio ya kila msikiti ni kama yale tuliyoyaeleza katika Aya iliyotangulia. Maana ni kuhimiza usafi na utwahara kutokana na uchafu na hadath na vilevile kujipamba nguo nzuri katika Swala ya Ijumaa, ya Jamaa, ya Idd au kutufu, ambapo sehemu hizo wanakusanyika watu, ili watu wasimkimbie kwa harufu yake mbaya na mandhari yake. Kujipamba ni

vizuri, hata kwa fukara pia ajipambe kwa kiasi cha hali yake. Kuna Hadith isemayo: “Hakika Mwenyezi Mungu ni mzuri na hupenda uzuri.”

**Na kuleni na kunyweni.**

Hii ni kupinga mwenye kuharamisha baadhi ya vyakula na vinywaji.

**Wala msifanye ufujaji (israf)** katika kula na kunywa na katika kujipamba kwa mavazi.

**Hakika yeye hawapendi wafanyao ufujaji (israf)**

Katika Aya nyingine anasema Mwenyezi Mungu:

﴿ إِنَّ الْمُبَدَّرِينَ كَانُوا إِخْوَانَ الشَّيَاطِينِ ﴾

“Hakika wabadhirifu ni ndugu wa mashetani” (17:27)

Na kuna Hadith isemayo: “Tumbo ni nyumba ya kila ugonjwa, na kula kwa makadirio ni msingi wa kila dawa, na uzoesheni kila mwili vile ulivyozea.” Na Ali Al-Murtadha <sup>(a.s)</sup> anasema: “Ni mara ngapi tonge moja imezua matonge mengi?”

**Sema: Ni nani aliyeharamisha pambo la Mwenyezi Mungu ambalo amewatolea waja wake, na vilivyo vizuri katika riziki?**

Dhahiri ya maneno ni swali na maana yake ni kukana sana uharamu wa kujipamba na vilivyo vizuri katika riziki. Na kwamba ni katika wasiwasi wa Shetani na si katika Wahyi wa Mwenyezi Mungu.

Kutegemeza neno mapambo kwa Mwenyezi Mungu kunafahamisha uhalali, na neno vitu vizuri linajifahamisha hilo lenyewe. Kwa sababu kila lililo haramu ni baya na wala si zuri.

Neno pambo linakusanya aina zake zote, ikiwa na pamoja na nyumba, na neno vitu vizuri linakusanya vyakula, vinywaji, kustarehe kwa mambo mazuri na wanawake, sauti nzuri, mandhari nzuri na kila starehe iliyo nzuri ambayo, sharia haikukataza.

Maulamaa wa Kiislam wameafikiana kwa kauli moja kwamba kila kitu ni halali mpaka uje ukatazo. Wakatoa dalili kwa hukumu ya akili, kwamba hakuna adhabu bila ya ubainifu, na kwa kauli ya Mtume Mtukufu (s.a.w.w):

“Watu wako katika wasaa wa wasiyoyajua.” na kauli yake: “Yale ambayo Mwenyezi Mungu amewafunikia waja kuyajua basi yameondolewa kwao.” Amesema tena: “Kila kitu kimeachiwa mpaka uje ukatazo kwenye kitu hicho.”

**Sema: Hivyo ni kwa wale walioamini katika maisha ya dunia, ni vyao tu siku ya Kiyama.**

Yaani katika maisha haya ya dunia wataneemeka wote waumini na makafiri, lakini kesho watakaoneemeka kwa mapambo ya Mwenyezi Mungu na vitu vizuri katika riziki, ni wale walioamini tu, peke yao bila ya kushirikiana na wale waliokufuru na kumshirikisha Mwenyezi Mungu.

**Namna hii tunazieleza ishara kwa watu wajuao.**

Mwenye kuifuatilia Qur’an ataona kuwa Mwenyezi Mungu anatumia neno Wajuzi (Ulama) kwa yule anayejua hukumu za Mwenyezi Mungu na akazitumia. Vilevile hilitumia kwa yule anayetarajiwa kuzijua na kuzitumia akifafanuliwa.

Kwa hiyo, makusudio ya watu wanaojua hapa ni aina ya pili ambao wanan- ufaika na ubainifu wa hukumu ya mapambo na vitu vizuri na vinginevyo na wanaowarejea maulama wa dini katika kujua hukumu za

Mwenyezi Mungu (s.w.t) na kutoa dalili kwa Aya za Mwenyezi Mungu kwa halali yake na haramu yake.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kumkana anayeharamisha mapambo na vitu vizuri, sasa anabainisha misingi ya vilivyo haramu kama ifuatavyo:

**Sema: Hakika Mola wangu ameharamisha mambo machafu, yaliyodhihirika na yaliyofichika.**

Umetangulia ubainifu wake katika kufasiri Sura 6:151 kifungu cha wasia.

**Na dhambi** ni kila jambo ambalo anaasiwa kwalo Mwenyezi Mungu, iwe kauli au kitendo. Kuunganisha machafu kwenye dhambi ni katika hali ya kuunganisha mahsus kwenye ujumla; kama ilivyo katika kauli yake Mwenyezi Mungu:

﴿ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَى نُوحٍ وَالتَّيِّبِينَ ﴾

“Kama tulivyompa Wahyi Nuh (a.s) na Mitume...” (4:163).

**Na dhulma bila ya haki.**

Kuna hadith inayosema “Lau jabali lingedhulu- mu jabali jingine, basi Mwenyezi Mungu angelifanya lile lililodhulumu lipondekepondeke” Na Amirul-Muminin anasema: “Mwenye kuchomoa upanga wa dhuluma atauwawa nao.”

**Na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na ambacho hakukiteremshia dalili.**

Hakuna dhambi nyingine baada ya ukafiri na shirk. Shirk ni kinyume cha Tawhid ambayo muhtasari wake ni:

﴿ لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ﴾

“Hakuna chochote kama mfano wake” (42:11).

Umetangulia ufafanuzi katika kufasiri Sura 6:153, kifungu cha ‘Wasia kumi.’

**Na kusema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua.**

Miongoni mwa hayo ni yale yaliyoashiriwa katika Aya 28 ya Sura hii: “**Na wanapofanya machafu husema tumewakuta nayo baba zetu na Mwenyezi Mungu ametuamrisha.**” Hakuna uchafu mbaya kama kusema bila ya kujua; na hakuna tofauti katika hukumu baina ya kumzulia Mungu na kumshirikisha. Imam Ali amesema: “Mwenye kuliacha neno ‘sijui’ atakuwa hana salama.”

**Kila umma una muda** makusudio ya umma hapa ni kundi, kama lilivyotumika neno hilo katika Aya isemayo:

﴿ وَلَمَّا وَرَدَ مَاءَ مَدْيَنَ وَجَدَ عَلَيْهِ أُمَّةً مِّنَ النَّاسِ يَسْقُونَ ﴾

“Alipofikia maji ya Madian alikuta umma wa watu wakinyweshwa.” (28:23)

Baada ya Mwenyezi Mungu kutaja uovu wa washirikina katika Aya 28; na yale aliyohalalisha katika Aya 31: na aliyoyaharamisha katika Aya 33. Baada ya haya yote anasema kila kundi, ikiwa ni pamoja na washirikina waliomzulia Mwenyezi Mungu, lina muda maalum katika maisha haya; kisha watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu waambiwe yale waliyokuwa wakiyafanya.

Katika haya mna makemeo na kiaga kwa washirikina na wenye kufanya uovu na watu wa dhulma na kila anayesema juu ya Mwenyezi Mungu bila ya ujuzi.

Utakapofika muda wao, hawatakawia (hata) saa moja wala hawatatangulia.

Imepita tafsir yake katika kufasiri Juz. 4 (3:145).

﴿ يَا بَنِي آدَمَ إِنَّمَا يَأْتِيَنَّكُمْ رُسُلٌ مِنْكُمْ يَقُصُّونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِي فَمَنِ اتَّقَى وَأَصْلَحَ فَلَا خَوْفٌ

عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴾

Enyi: Wanadamu! Watakapowafikia Mitume kutoka miongoni mwenu, wakawaeleza ishara zangu, basi watakaogopa na kufanya mema, haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.

﴿ وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَاسْتَكْبَرُوا عَنْهَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴾

Na wale watakaokadhibisha ishara zetu na kuzifanyia kiburi, hao ndio watu wa motoni, watadumu humo.



## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَى عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ أُولَئِكَ يَنَالُهُمْ نَصِيبُهُم مِّنَ الْكِتَابِ حَتَّىٰ إِذَا جَاءَهُمْ رَسُولٌ مُّرْسَلٌ أَيْتَوْقَوْهُمْ قَالُوا آيِنَ مَا كُنْتُمْ تَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّهِ قَالُوا ضَلُّوا عَنَّا وَشَهِدُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ أَنَّهُمْ كَانُوا كَافِرِينَ ﴿٣٧﴾

37. Basi ni nani dhalimu zaidi kuliko yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo au anayezikadhibisha Aya zake? Hao ndio itawafikia sehemu yao waliyoandikiwa. Mpaka watakapowafikia wajumbe wetu ambao ni Malaika, kuwafisha, watasema: Wako wapi mliokuwa mkiwaabudu badala ya Mwenyezi Mungu? Watasema wametupotea, Na watajishuhudia wenyewe kwamba wao walikuwa makafiri

قَالَ ادْخُلُوا فِي أُمَّةٍ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِكُمْ مِنَ الْجِنِّ وَالإِنسِ فِي النَّارِ كُلَّمَا دَخَلَتْ أُمَّةٌ لَعَنَتْ أُخْتَهَا حَتَّىٰ إِذَا ادَّارَكُوا فِيهَا جَنبًا قَالَتْ أُخْرَاهُمْ لِأَوْلَاهُمْ رَبَّنَا هَلْؤَلَاءِ أَضَلُّونَا فَآتَاهُمُ عَذَابًا ضِعْفًا مِّنَ النَّارِ قَالَ لِكُلِّ ضِعْفٍ وَلَكِن لَّا تَعْلَمُونَ ﴿٣٨﴾

38. Atasema: Ingieni motoni pamoja na umma zilizopita kabla yenu za majini na watu, Kila utakapoingia umma utalaani ndugu zake. Mpaka watakapokusanyika wote humo, wa mwisho wao watawasema wa mwanzo wao: Mola wetu! Hawa ndio waliotupoteza basi uwape adhabu ya moto maradufu, Hawa ndio waliopoteza, Atasema: Itakuwa maradufu kwenu nyote, lakini hamjui.

وَقَالَتْ أَوْلَاهُمْ لِأَوْلَاهُمْ فَمَا كَانَ لَكُمْ عَلَيْنَا مِن فَضْلٍ فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْسِبُونَ ﴿٣٩﴾

39. Na wa mwanzo wao watawambia wa mwisho wao; basi nyinyi pia hamkuwa na ubora kuliko sisi. Basi onjeni adhabu kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyachuma.

### WANAOOGOPA NA KUFANYA MEMA

Aya 35-39

#### MAANA

Enyi: Wanadamu! Watakapowafikia Mitume kutoka miongoni mwenu, wakawaeleza ishara zangu, basi watakaogopa na kufanya mema, haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.

Mwenyezi Mungu alimuumba Adamu na kizazi chake na akawawekea njia ya kufuata, akawapelekea Mitume wa kuwafahamisha njia hiyo. Akawafanya Mitume ni jinsi ya wale wanaopelekewa Mitume hao. Kwa sababu hilo lina athari zaidi na ni hoja zaidi. Basi atakayesikia na akatii atasalimika na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu na adhabu yake.

Na wale watakaokadhibisha ishara zetu na kuzifanyia kiburi, hao ndio watu wa motoni, watadumu humo.

Mwalimu wetu- Mungu awe radhi naye - alikuwa akiwasomea wanafunzi wake sehemu za Kitab anachofundisha na kuwafafanulia kwa maneno

wanayoyafahamu wote. Ikiwa sehemu iko wazi na inaeleweka kwa wote, basi husema “Kufafanua ufafanuzi ni mushkeli zaidi ya mishikeli!”. Hapo huiacha sehemu hiyo na kuendelea.

**Basi ni nani dhalimu zaidi kuliko yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo au anayezikadhibisha Aya zake?**

Yametangulia maelezo katika Juz, 7 (6:21)

**Hao ndio itawafikia sehemu yao waliyoandikiwa.**

Hao ni wale waliotangulia kutajwa-ambao wamezusha yasiyokuwapo na wakakanusha yaliyopo. Makusudio ya waliyoandikiwa ni ajali na riziki. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu anawaacha wakadhibishaji wamalize umri na riziki waliyoandikiwa.

**Mpaka watakapowafikia wajumbe wetu ambao ni Malaika, kuwafisha, watasema: Wako wapi mliokuwa mkiwaabudu badala ya Mwenyezi Mungu? Watasema wametupotea hatujui wako wapi wala hawaji kutuokoa na adhabu.**

**Na watajishuhudia wenyewe kwamba wao walikuwa makafiri.**

Kukiri dhambi kunafaa pale inapowezekana kuificha na kukimbia malipo yake. Lakini baada ya kudhihiri kama jua na wakati wa kutekelezwa adhabu yake, hapo kukiri hakufai chochote.

Baada ya makafiri kujishuhudia wenyewe mahakama itafungwa na kutolewa hukumu ya adhabu ya moto.

**Atasema: Ingieni motoni pamoja na umma zilizopita kabla yenu za majini na watu.**

Makusudio ya uma ni wale wenye mila za kikafiri. Yaani Mwenyezi Mungu atawaambia wale waliokufuru Utume wa Muhammad (s.a.w.w): Ingieni motoni ikiwa ni malipo ya kukufuru kwenu; kama walivyoingia waliokadhibisha Mitume kabla yenu.

**Kila utakapoingia umma utalaani ndugu zake.**

Wataalaniana nao walikuwa ndugu katika dini, nasaba na ukwe. Hivi ndivyo wafanyavyo watu wa hawaa na upotevu, wanapendana wakati wa utulivu na siku ya mutumaini, na kuchukiana na kulaaniana wakati ambapo hakuna matumaini wala matarajio yoyote.

**Mpaka watakapokusanyika wote humo.**

Yaani wakikutana humo, utanza ugomvi na malumbano **wa mwisho wao watawasema wa mwanzo wao: Mola wetu! Hawa ndio waliotupoteza basi uwape adhabu ya moto maradufu.**

Baadhi ya wafasiri wamesema kuwa makusudio ya wa mwanzo wao ni wa kwanza kuingia motoni, na wa nyuma ni wa nyuma kuingia. Wengine wakasema kuwa makusudio ya wa mwanzo ni viongozi na wa nyuma ni wafuasi. Kauli hii ndiyo iliyo sahihi kutokana na kusema: ‘**Hawa ndio waliotupoteza.**’

Kwa sababu mwenye kupoteza hufuatwa, na mwenye kupotezwa hufuata. Wenye kufuata wanataka kuongezewa adhabu wale waliofuata. Kwa vile wao ndio sababu ya kupotea kwao.

**Atasema: Itakuwa maradufu kwenu nyote, lakini hamjui.**

Yaani nyote mtapata adhabu maradufu, lakini kila kundi halijui kiasi cha adhabu ya kundi jingine.

Na wa mwanzo wao watawaambia wa mwisho wao: Basi nyinyi pia hamkuwa na ubora kuliko sisi.

Wafuasi wanataka wazidishiwe adhabu viongozi, Kwa hiyo viongozi nao wanasema: Kwa nini mnataka hayo, nasi sote tuna malipo sawa wala hatutofautiana na chochote, kwa nini basi Mwenyezi Mungu atuongezee sisi adhabu zaidi ya nyinyi? Kisha wataendelea kusema ikiwa ni majibu ya maombi ya kuzidishiwa adhabu:

Basi onjeni adhabu kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyachuma sisi hatukuwalazimisha mlikuwa na hiyari.

إِنَّ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَاسْتَكْبَرُوا عَنْهَا لَا تُفَتِّحُ لَهُمْ أَبْوَابُ السَّمَاءِ وَلَا يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ حَتَّى يَلِجَ الْجَمَلُ فِي سَمِّ الْخِيَاطِ وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُجْرِمِينَ ﴿٤٠﴾

40. Hakika wale waliokadhibisha ishara zetu na kuzifanyia kiburi, hawatafunguliwa milango ya mbinguni, Wala hawataingia Peponi mpaka ngamia aingie katika tundu ya sindano, Na hivi ndivyo tunavyowalipa wakosefu.

لَهُمْ مِنْ جَهَنَّمَ مِهَادٌ وَمِنْ فَوْقِهِمْ غَوَاشٍ وَكَذَلِكَ نَجْزِي الظَّالِمِينَ ﴿٤١﴾

41. Watakuwa na matandiko ya Jahanamu na juu yao shuka za kujifunika, Na hivi ndivyo tunavyowalipa madhalimu.

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَا نُكَلِّفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا أُولَئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٤٢﴾

42. Na wale walioamini na wakatenda amali njema; hatukalifishi nafsi yoyote ila uweza wake; hao ndio watu wa Peponi, watadumu humo.

وَنَزَعْنَا مَا فِي صُدُورِهِمْ مِنْ غَلٍّ تَجَّ رِي مِنْ تَحْتِهِمُ الْأَنْهَارُ وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي هَدَانَا لِهَذَا وَمَا كُنَّا لِنَهْتَدِيَ لَوْلَا أَنْ هَدَانَا اللَّهُ لَقَدْ جَاءَتْ رَسُولٌ رَ بَّنَا بِالْحَقِّ وَتُودُوا أَنْ تُلَكُمُ الْجَنَّةَ أَوْرَثْتُمُوهَا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٤٣﴾

43. Na tutaondoa chuki vifuani mwao; chini yao itapita mito. Na watasema: Sifa njema zote zinamstahiki Mwenyezi Mungu ambaye ametuongoza kwenye haya. Na hatukuwa wenye kuongoka wenyewe kama asingetuongoza Mwenyezi Mungu. Hakika Mitume wa Mola wetu walileta haki. Na watanadiwa kuwa hii ndiyo Pepo mliyorithishwa kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyafanya.

## NGAMIA NA TUNDU YA SINDANO

### Aya 40-43

#### MAANA

Hakika wale waliokadhibisha ishara zetu na kuzifanyia kiburi, hawatafunguliwa milango ya mbinguni.

Ishara za Mwenyezi Mungu zinakusanya dalili za kuwapo Mwenyezi Mungu, Utume wa Mitume yake na kila walilolieza kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kusema kwake Mwenyezi Mungu: Hawatafunguliwa milango ya mbingu- ni ni fumbo la kukataliwa amali zao na kwamba hazitakubaliwa; kama zikubaliwavyo amali za watu wema.

Mwenyezi Mungu anasema:

إِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ ﴿١٠﴾

“Kwake hupanda neno zuri na tendo jema huliinua” (35: 10)

Wala hawataingia Peponi mpaka ngamia aingie katika tundu ya sindano.

Hili ni sharti lisilowezezana; sawa na kusema:

إِنْ كَانَ لِلرَّحْمَنِ وَلَدٌ فَأَنَا أَوَّلُ الْعَابِدِينَ ﴿٨١﴾

“Kama mwingi wa rehema angelikuwa na mtoto ningekuwa wa kwanza kumwabudu” (43: 81).

Kupatikana sharti la muhali ni muhali. Waarabu hupigia mfano jambo lisilowezezana kwa kusema: “Sitafanya mpaka kunguru aote mvi!” Au “Mpaka ngamia aingie katika tundu ya sindano!”

Na hivi ndiyo tunavyowalipa wakosefu.

Yaani tunawalipa kwa kuwazuilia Pepo. Pamoja na kuzuiliwa huku watakuwa na matandiko ya Jahanamu na juu yao shuka za kujifunika Yaani Jahanamu itawazunguka pande zote.

Na wale walioamini na wakatenda amali njema; hatukalifishi nafsi yoyote ila uweza wake; hao ndio watu wa Peponi, watadumu humo.

Mwenyezi Mungu alipowapa kiaga waasi kwa adhabu ya Jahanamu sasa anawaahidi watiifu Pepo yenye neema watakayo starehe nayo bila ya kuwa na mwisho.

Ameishiria kwa kauli yake: “Hatukalifishi nafsi yoyote ila uweza wake,” kwamba Pepo kwa kadiri ya ukubwa wake, lakini mtu anaweza kuifikia bila ya mashaka wala uzito wowote.

Na kwamba atakayeingia Jahanam ataingia kwa kutaka kwake na hiyari yake.

Na tutaondoa chuki vifuani mwao; chini yao itapita mito.

Kwa nini iweko chuki? Duniani kulikuwa na chuki husuda, ria, uwongo na unafiki, kwa sababu kulikuwa na mafukara na matajiri, madhalimu na wenye kudhulumwa na aliye mashuhuri na asiyejulikana, lakini Peponi hakuna ufukara, dhuluma wala umashuhuri baada ya Mwenyezi Mungu kumuweka kila mmoja katika daraja yake anayostahiki na cheo alichojichumia. Kila mmoja katika watu wa Peponi anahisi raha kwa kuokoka na Moto wa Jahanamu wala hamwangalii kabisa aliye juu yake:

فَمَنْ رُحِّحَ عَنِ النَّارِ وَأُدْخِلَ الْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ ﴿١٨٥﴾

“Mwenye kuepushwa na moto akatiwa Peponi, basi huyo amefuzu” Juz.4 (3:185)

Na watasema: Sifa njema zote zinamstahiki Mwenyezi Mungu ambaye ametuongoza kwenye haya. Yaani kwenye njia ya neema hii.

Na hatukuwa wenye kuongoka wenyewe kama asingetuongoza Mwenyezi Mungu.

Hiyo ni shukrani kwa Mwenyezi Mungu juu ya neema zake.

Hakika Mitume wa Mola wetu walileta haki.

Mitume waliwapa habari ya Pepo wakaamini mambo ya ghaibu. Walipoiona kwa macho yao walifurahi ambapo ghaibu imeonekana.

Na watanadiwa kuwa hii ndiyo Pepo mliyorthishwa kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyafanya.

Neno “Kurithishwa” kwa sababu ya kufanya amali, linafahamisha kwamba Pepo ni haki ya lazima kwa wanaoifanyia amali; sawa na mirathi. Kwa maneno mengine ni kuwa Aya inafahamisha kwamba thawabu ni haki siyo fadhila.

وَنَادَى أَصْحَابُ الْجَنَّةِ أَصْحَابَ النَّارِ أَنْ قَدْ وَجَدْنَا مَا وَعَدَنَا رَبُّنَا حَقًّا فَهَلْ وَجَدْتُمْ مَا وَعَدَ رَبُّكُمْ حَقًّا قَالُوا نَعَمْ فَأَذَّنَ مُؤَذِّنٌ بَيْنَهُمْ أَنْ لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿٤٤﴾

44. Na watu wa Peponi watawanadia watu wa Motoni kwamba tumekuta aliyotuahidi Mola wetu kuwa ni kweli, Je, nanyi pia mmekuta aliyowaahidi Mola wenu kuwa kweli? Watasema ndio, Basi mtangazaji atatangaza kati yao kwamba laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya madhalimu.

الَّذِينَ يَصُدُّونَ عَنِ سَبِيلِ اللَّهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجًا وَهُمْ بِالْآخِرَةِ كَافِرُونَ ﴿٤٥﴾

45. Ambao wanazulia njia ya Mwenyezi Mungu, Na wakataka kuipotosha, Nao hawaiamini Akhera.

## WATU WA PEPONI WATAITA

Aya 44 – 45

### MAANA

Na watu wa Peponi watawanadia watu wa Motoni kwamba tumekuta aliyotuahidi Mola wetu kuwa ni kweli, Je, nanyi pia mmekuta aliyowaahidi Mola wenu kuwa kweli?

Watu wa Peponi wanajua fika kwamba watu wa Motoni wamekuta ukweli waliyoahidiwa na kutishiwa, lakini wao watawaelekezea swali hili kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu juu ya aliyowaneemesha na kuwakumbusha yale waliyokuwa wakiyasema yakiwa ni pamoja na dharau na stihzai kwa dini ya haki na wafuasi wake.

Watasema ndio.

Maana hakuna njia ya kukataa.

Basi mtangazaji atatangaza kati yao kwamba laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya madhalimu.

Kwa laana hii, mtangazaji atainua sauti siku ya Kiyama akiwataja madhal- imu kwa sifa tatu:

1. Ambao wanazulia njia ya Mwenyezi Mungu. Yaani wanawazuia watu kuifuata haki kwa njia mbali mbali.
2. Na wakataka kuipotosha. Hawataki ukweli na ikhlasi wala msimamo, isipokuwa wanataka uwongo, unafiki na hiyana.
3. Nao hawaiamini Akhera. Hawaogopi hisabu wala adhabu kutokana na makosa yao na madhambi.

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

وَبَيْنَهُمَا حِجَابٌ وَعَلَى الْأَعْرَافِ رِجَالٌ يَعْرِفُونَ كُلًّا بِسِيمَاهُمْ وَنَادَوْا أَصْحَابَ الْجَنَّةِ أَنْ سَلَامٌ  
عَلَيْكُمْ لَمْ يَدْخُلُوهَا وَهُمْ يَطْمَعُونَ ﴿٤٦﴾

46. Na Baina Yao Patakuwa Na Pazia, Na Juu Ya A'raf Watakuwako Watu Watakaowafahamu Wote Kwa Alama Zao, Na Watanadia Watu Wa Peponi: Salamun Alaykum. Hawajaingia Nao Wanatumai.

وَإِذَا صُرِفَتْ أَبْصَارُهُمْ تِلْقَاءَ أَصْحَابِ النَّارِ قَالُوا رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٤٧﴾

47. Na Macho Yao Yanapogeuzwa Kuelekea Watu Wa Motoni, Husema: Mola Wetu Usituweke Pamoja Na Watu Waliodhulumu.

وَنَادَى أَصْحَابُ الْأَعْرَافِ رِجَالًا يَعْرِفُونَهُمْ بِسِيمَاهُمْ قَالُوا مَا أَغْنَىٰ عَنْكَ مِ جَمْعُكُمْ وَمَا كُنْتُمْ  
تَسْتَكْبِرُونَ ﴿٤٨﴾

48. Na Watu Wa A'raf Watawanadia Watu Wanaowafahamu Kwa Alama Zao, Waseme: Haukuwasaidia Mjumuiiko Wenu Wala Mliivyokuwa Mkiyivunia.

أَهْلُوآءِ الَّذِينَ أَقْسَمْتُمْ لَا يَنَالُهُمُ اللَّهُ بِرَحْمَةٍ ادْخُلُوا الْجَنَّةَ لَا خَوْفٌ عَلَيْكُمْ وَلَا أَنْتُمْ تَحْزَنُونَ

﴿٤٩﴾

49. Je, Hawa Ndio Wale Mliokuwa Mkiwaapia Kwamba Mwenyezi Mungu Hatawafikishia Rehema? Ingieni Peponi, Hakuna Hofu Juu Yenu Wala Hamtahuzunika.

### WATU WA A'RAF

**Aya 46 – 49**

#### A'RAF

Sisi tunaamini siku ya Kiyama, hisabu na malipo, kwa ujumla, ikiwa ni msingi katika misingi ya dini. Ama ufafanuzi na mafungu yake, hayo ni katika elimu ya ghaibu. Wala hakithibiti kitu chochote katika ulimwengu huo ila kwa Aya iliyo wazi au kwa Hadith wazi iliyothibiti kutoka kwa Ma'sum kwa khabar Mutawatir, na wala sio habari Ahad. Kwa sababu Habari Ahad ni hoja katika matawi tu, si katika misingi.

Khabar Mutawatir ni ile ambayo wanaipokea watu wengi bila ya kutokea mgongano wa uwongo. Kinyume chake ni Khabar Ahad.

Imethibiti kutokana na Wahyi kwamba huko Akhera kutakuwa na mahali, baina ya Pepo na moto, panaitwa A'raf. Hapo si mahali pa Pepo wala moto, lakini kwa undani ni rehema inayofuata Pepo; na kwa dhahiri ni adhabu inayofuatia Moto. Mwenyezi Mungu anasema:

فَضْرِبَ بَيْنَهُمْ بِسُورٍ لَهُ بَابٌ بَاطِنُهُ فِيهِ الرَّحْمَةُ وَظَاهِرُهُ مِنْ قِبَلِهِ الْعَذَابُ ﴿١٣﴾

“... utiwe baina yao ukuta wenye mlango; ndani yake mna rehema na nje kwa upande wake wa mbele kuna adhabu.” (57:13).

Katika mahali hapo paitwapo A'raf kutakuwa na watu wanaowajua watu wote wa Peponi na wa Motoni. Hawawajui kwa majina au hali yao; bali wanawajua kwa alama zinazowatofautisha.

Wao watawaangalia wa Peponi na kuwasalimia wakitumai kuwa pamoja nao wakati fulani. Na jicho lao likiwaangukia watu wa motoni tu, humwomba Mwenyezi Mungu asiwajaalie kuwa pamoja na watu madhalimu walioangamia. Kisha mwisho wa mambo watu wa A'raf wataingia Peponi. Kwa sababu wao ni katika watu wa Lailaha illa Ilah na Mwenyezi Mungu ana usaidizi maalum kwa watu wa aina hiyo.

Hayo ndiyo ujumla wa yaliyoelezwa na Qur'an kuhusu A'raf na watu wake, lakini Wafasiri wengi wamepetuka mpaka katika ufafanuzi huu, sasa tunaingilia kufasiri yanayofahamishwa na Aya:

**Na baina yao patakuwa na pazia.**

Yaani baina ya Pepo na Moto au baina ya watu wa sehemu hizo mbili. Pazia ni hiyo A'raf iliyoashiriwa na kauli yake Mwenyezi Mungu:

**Na juu ya A'raf watakuwako watu watakaowafahamu wote kwa alama zao.**

Yaani watu wa A'raf watawajua wote watu wa Peponi, na watu wa motoni kwa alama zitakazowatambulisha sio mbali kuwa alama hizi ni zile zilizoashiriwa na Aya isemayo:

﴿يَوْمَ تَبْيَضُّ وُجُوهٌ وَتَسْوَدُّ وُجُوهٌ﴾ ﴿١٠٦﴾

“Siku ambayo nyuso zitang'aa na nyuso (nyingine) zitasawijika.” (3:106).

Na pia Aya isemayo:

﴿وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ مُّسْفِرَةٌ﴾ ﴿٣٨﴾ ﴿صَا حِكَّةٌ مُّسْتَبْشِرَةٌ﴾ ﴿٣٩﴾ ﴿وَوُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ عَلَيَّهَا غَبْرَةٌ﴾ ﴿٤٠﴾  
﴿تَرْهَقَهَا قَتْرَةٌ﴾ ﴿٤١﴾ ﴿أُولَئِكَ هُمُ الْكٰفِرَةُ الْفٰجِرَةُ﴾ ﴿٤٢﴾

“Nyuso siku hiyo zitanawiri. Zitacheka na kufurahika. Na nyuso nyingine siku hiyo zitakuwa na mavumbi. Zimefunikwa na weusi weusi, Hao ndio makafiri, watendao maovu” (80:38-42)

Imesemekana kuwa alama hizo ni za ujumla watazijua watu wote; na dhahiri ya Aya inafahamisha kuwa alama hizo watazijua watu wa A'raf tu.

Kwa vyovyote itakavyokuwa, mambo ni mepesi sana hakuna taabu, maadamu sisi si wenye kukalifiwa wala hatutaulizwa kuhusu alama hizo zitakavyokuwa na hakika yake au sifa zake maalum au za ujumla.

**Utauliza:** Ni nani hao watu wa A'raf?

**Jibu:** Wafasiri wana kauli nyingi, yenye nguvu ni ile waliyoielezea wengi kwamba wao ni wale ambao uzani wao umekuwa sawa sawa; si mema yao yatakayozidi wala maovu yao. Lau mojawapo lingezidi jingine kwa uzani wa tonoradi, basi mwisho wao ungelijulikana, kuwa aidha Peponi au motoni.

**Swali la pili:** watu wa Peponi watajulikana kwa kuingia humo; vilevile watu wa Motoni, Sasa kuna haja gani ya alama?

**Jibu:** Huenda ikawa alama hizo ni za kupambanua baina ya makundi mawili kabla ya hisabu na adhabu; kama ambavyo mhalifu anavyotambulika kutokana na hali ya uso wake unavyokuwa anapopelekwa mahakamani.

**Na watanadia watu wa Peponi: Salamun Alaykum.**

Dhamir ya Watanadi ni ya watu wa A'raf. Maana ni kuwa wao watakapowaangalia watu wa Peponi watawasalimia kwa maamkuzi ya heshima.

Hawajaingia nao wanatumai kuingia Peponi, Kwa sababu wao ni katika watu wa Lailaha illa Allah. Na kila anayemwamini Mwenyezi Mungu anatumaini rehema yake na maghufira yake. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿إِنَّهُ لَا يَيْئَسُ مِنْ رَوْحِ اللَّهِ إِلَّا الْقَوْمُ الْكَافِرُونَ﴾ (٨٧)

“Hakika hawakati tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu isipokuwa watu makafiri.” (12:87).

Kuna Hadith isemayo kuwa mtu mmoja alisema: “Wallahi Mwenyezi Mungu hatamsamehe fulani.” Mwenyezi Mungu akasema: “Ni nani huyu anayeniapia mimi kuwa nisimsamehe fulani?” Hakika mimi nimekwisha msamehe fulani na nimezishusha amali za mwenye kuapa.”

Na macho yao yanapogeuzwa kuelekea watu wa Motoni, husema: Mola wetu usituweke pamoja na watu waliodhulumu.

Neno ‘Yanapogeuzwa’ linafahamisha kuwa kuangalia kwa watu wa A'raf kwa watu wa motoni si kwa kukusudia.

Makusudio ya dhulma hapa ni ushirikina na kufu. Maana ni kuwa wao wakisadifu kuyaona ya watu wa Motoni huogopa na kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu asiwajaalie kuwa pamoja na watu makafiri walioangamia.

Na watu wa A'raf watawanadia watu wanaowafahamu kwa alama zao, waseme: Haukuwasaidia mjumuiko wenu wala mlivyokuwa mkijivuna.

Wale waliokuwa wakijivuna katika ardhi walikuwa wakiwadharau waumini na wakijitukuza kwa yale waliyokuwa wakimiliki miongoni mwa mali na jaha; na wakiwaambia: Hamtapata kamwe rehema ya Mwenyezi Mungu, lakini kitakapofika kiyama na waovu kulipwa matendo yao, basi watu wa A'raf watawakumbusha mambo mawili:

**Kwanza:** yale waliyokuwa wakiyakusanya na kujivunia nayo, mali na kadhalika. Hayo yanaashiriwa na kauli yake Mwenyezi Mungu: ‘Haukuwasaidia mjumiko wenu wala mlivyokuwa mkijivunia.’

**Pili:** Yale waliyokuwa wakiwaambia waumini kuwa hamtaingia Peponi. Hayo yameashiriwa na kauli yake Mwenyezi Mungu:

Je, hawa ndio wale mliokuwa mkiwaapia kwamba Mwenyezi Mungu hatawafikishia rehema?

Kwa hiyo neno ‘Hawa’ ni waumini wadhaifu na neno mkiwaapia wanaam- biwa wajivuni.

Ingieni Peponi, hakuna hofu juu yenu wala hamtahuzunika.

Yaani waumini walioambiwa na wajivuni kuwa hawataingia Peponi, ndio sasa wanaambiwa ingieni Peponi.

﴿وَتَادَى أَصْحَابُ النَّارِ أَصْحَابَ الْجَنَّةِ أَنْ أَفِيضُوا عَلَيْنَا مِنَ الْمَاءِ أَوْ مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ حَرَّمَهُمَا عَلَى الْكَافِرِينَ﴾ (٥٠)

50. Watu wa Motoni watawanadia watu wa Peponi: Tumiminieni maji au katika vile alivyowapa Mwenyezi Mungu. Watasema: Hakika Mwenyezi Mungu ameyaharamisha vyote viwili hivyo kwa makafiri.



الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَهُمْ لَهْوًا وَلَعِبًا وَغَرَّتْهُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا فَالْيَوْمَ نَنسَاهُمْ كَمَا نَسُوا لِقَاءَ يَوْمِهِمْ هَذَا وَمَا كَانُوا بِآيَاتِنَا يَجْحَدُونَ ﴿٥١﴾

51. Ambao waliifanya dini yao kuwa upuuzi na mchezo na yakawahadaa maisha ya dunia. Basi leo sisi tunawasahau kama walivyosahau kukutana na siku yao hii na kwa sababu walikuwa wakizikataa ishara zetu.

وَلَقَدْ جِئْتَهُمْ بِكِتَابٍ فَصَّلْنَاهُ عَلَىٰ عِلْمٍ هُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٢﴾

52. Na hakika tumewaletea Kitab tulichokipambanua kwa ujuzi, ambacho ni mwongozo na rehema kwa watu wanaoamini.

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا تَأْوِيلَهُ يَوْمَ يَأْتِي تَأْوِيلَهُ يَقُولُ الَّذِينَ كَسُوهُ مِنْ قَبْلُ قَدْ جَاءَتْ رُسُلًا بِآلِحَقِّقٍ فَهَلْ لَنَا مِنْ شَفْعَاءَ فَيَشْفَعُوا لَنَا أَوْ نُرَدُّ فَنَعْمَلْ غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ قَدْ خَسِرُوا أَنْفُسَهُمْ وَصَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٥٣﴾

53. Hawangojei ila matokeo yake siku yatakapotokea matokeo yake, watasema wale walioisahau hapo zamani: Hakika Mitume wa Mola wetu walileta haki, Je, tunao waombezi watuombe. Au turudishwe ili tufanye yasiyokuwa yale tuliyoukuwa tukiyafanya? Hakika wamejitia hasarani nafsi zao na yamewapotea waliyoukuwa wakiyazua.

## WATU WA PEPONI NA WA MOTONI

Aya 50 – 53

### MAANA

Imeelezwa katika Hadith kwamba furaha ya watu wa Peponi kwa kuokoka na Moto itawazidishia neema na kwamba masikitiko ya watu wa Motoni kwa kukosa neema yatawazidisha adhabu; nao watajua kuwa watu wa Peponi wako kwenye neema. Ndio maana:

watu wa Motoni watawanadia watu wa Peponi: Tumiminieni maji au katika vile alivyowapa Mwenyezi Mungu.

Nao watu wa Peponi watawajibu:

Hakika Mwenyezi Mungu ameyaharamisha vyote viwili hivyo kwa makafiri.

Baada kukata tamaa na watu wa Peponi, watataka waokolewe na walinzi wa Motoni; kama anavyosema Mwenyezi Mungu:

وَقَالَ الَّذِينَ فِي النَّارِ لِخَازِنَةِ جَهَنَّمَ ادْعُوا رَبَّكُمْ يُحَقِّقْ عَنَّا يَوْمًا مِنَ الْعَذَابِ ﴿٤٩﴾ قَالُوا أَوْلَمْ تَكُنْ تَأْتِيكُمْ رُسُلُكُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا بَلَىٰ قَالُوا فَادْعُوا وَمَا دُعَاءُ الْكَافِرِينَ إِلَّا فِي ضَلَالٍ ﴿٥٠﴾

Na wale waliomo Motoni watawambia walinzi wa Jahanamu: “Muombeni Mola Wenu atupunguzie siku moja ya adhabu.” Na (walinzi) watasema: “Je, hawakuwawajia Mitume wenu kwa hoja zilizo wazi? Waseme: Kwa nini? Watasema: Basi ombeni, na dua ya makafiri haiwi ila ni ya kupotea bure.” (40: 49-50).

Baada ya kukata tamaa na walinzi watataka kujiokoa kwa Mwenyezi Mungu Mola wa ulimwengu, jambo ambalo lilikuwa rahisi wakati wa raha.

قَالُوا رَبَّنَا عَلَّيْنَا شِقْوَتُنَا وَكُنَّا قَوْمًا ضَالِّينَ ﴿١٠٦﴾ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْهَا فَإِنْ عُدْنَا فَإِنَّا ظَالِمُونَ ﴿١٠٧﴾ قَالَ اخْسَرُوا فِيهَا وَلَا تُكَلِّمُونَ ﴿١٠٨﴾

Watasema: “Mola wetu tulizidiwa na ubaya wetu na tukawa watu wenye kupotea. Mola wetu, tutuoe humu na tukirudia tena hakika tutakuwa wenye kudhulumu. Na (Mwenyezi Mungu) atasema: Hizikieni humo wala msiniseshe.” (23: 106 - 108).

Ambao waliifanya dini yao kuwa upuuzi na mchezo na yakawahadaa maisha ya dunia.

Imepita tafsir yake katika Juz.7 (6: 70).

Basi leo sisi tunawasahau kama walivyosahau kukutana na siku yao hii na kwa sababu walikuwa wakizikataa ishara zetu.

Makusudio ya kusahau hapa ni kupuuzi, kwani:

﴿ وَمَا كَانَ رَبُّكَ نَسِيًّا ﴾ ٦٤

“Mola wako si Mwenye kusahau” (19: 64)

Na hakika tumewaletea Kitab tulichokipambanua kwa ujuzi, ambacho ni mwongozo na rehema kwa watu wanaoamini.

Katika Aya zilizotangulia Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja watu wa Peponi, wa Motoni na wa A’raf . Na Aya hii na inayofuatia zinahusika na watu wa motoni tu, ambao wameghurika na maisha ya dunia.

Mwenyezi Mungu anasema kuwa tumewaletea hawa Qur’an inayoongoza kwenye uongofu na inayobainisha kwa ujuzi yake wanayoyahitajia watu katika maisha yao na marejeo yao na imemdhaminia – yule anayeamini na akayatumia mafunzo yake – uongofu wa kheri katika dunia na rehema ya Mwenyezi Mungu na thawabu katika Akhera. Ama mwenye kuachana nayo akafuata matamano yake, basi marejeo yake ni Jahanamu.

Hawangojei ila matokeo yake.

Dhamir ya ‘yake’ inarudia Kitab; yaani kila linalotamkwa na Qur’an litatokea tu hapana budi.

Siku yatakapofika matokeo yake.

Kwa kutokea yale iliyoyatolea habari na uwabainikie makafiri kwa macho ukweli wake.

Watasema wale walioisahau hapo zamani: Hakika Mitume wa Mola wetu walileta haki.

Watayasema haya baada ya kuona adhabu, Na kabla yake waliwaambia Mitume kuwa ni wachawi na wazushi. Vilevile wataendelea kusema baada ya kuona adhabu:

Je, tunao waombezi watuombe kwa Mwenyezi Mungu atusamehe makosa yetu na asitufanyie hizaya na adhabu kama tunayvostahiki?

Au turudishwe ili tufanye yasiyokuwa yale tuliyokuwa tukiyafanya?

Lau Mwenyezi Mungu ataitikia maombi yao haya, misimamo yote ingelibatilika, na mwovu, ambaye haamini mpaka awekewe upanga kichwani mwake, asingekuwa ana tofuati na mwema ambaye anaamini haki bila kulazimishwa na kujitolea mhanga katika njia ya haki kwa pumzi zake zote.

Hakika wamejitia hasarani na yamewapotea waliyokuwa wakiyazua.

Hivi ndivyo zinavyokwenda bure amali za wabatilifu na hupotelewa na waombezi na wasimamizi waliokuwa wakiwafanyia amali.

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ يُغْشِي  
الَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ تَبَارَكَ  
اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٥٤﴾

54. Hakika Mola wenu ni Mwenyezi Mungu aliyeziumba mbingu na ardhi katika siku sita, Kisha akatawala juu ya Arshi. Huufunika usiku kwa mchana, ufuatiao upesi upesi, Na jua na mwezi na nyota zinatumiwa kwa amri yake. Fahamuni! Kuumba na amri ni yake. Ametukuka Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote.

ادْعُوا رَبَّكُمْ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ ﴿٥٥﴾

55. Mwombieni Mola wenu kwa unyenyekevu na kwa uficho, Hakika yeye hawapendi wapetukao mipaka.

وَلَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا وَادْعُوهُ خَوْفًا وَطَمَعًا إِنَّ رَحْمَتَ اللَّهِ قَرِيبٌ مِّنَ  
الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٦﴾

57. Wala msifanye ufasidi katika ardhi baada ya kutengenea kwake. Na mwombeni kwa kuogopa na kwa kutumai. Hakika rehema ya Mwenyezi Mungu iko karibu na wanaofanya mema.

### KATIKA SIKU SITA

**Aya 54 – 56**

#### MAANA

Hakika Mola wenu ni Mwenyezi Mungu aliyeziumba mbingu na ardhi katika siku sita.

Wafasiri wana kauli zenye kugongana katika Aya hii, Sababu yake ni mambo mawili:

**Kwanza:** kwamba vitendo vya Mwenyezi Mungu havipimwi kwa wakati. Mwenyezi Mungu anasema: “Na amri yetu haikuwa ila ni moja tu kama kupepesa jicho.” (54:50).

Yaani neno moja tu, “Kuwa, ikawa”

**Pili:** kwamba wakati unahisabiwa baada ya kumbwa mbingu na ardhi na matukio yanayotokea ndani yake. Kwa hiyo kabla ya ulimwengu hakukuwa na wakati wala siku.

Sasa Je, hiyo si ni sawa na kusema: Nimejenga nyumba kutokana na paa?

Kwa hiyo basi hakuna budi kuleta taawili ya siku kwa maana inayokubalika na inayoingia akilini, Wametofautiana katika kuainisha maana hayo ya majazi, Kuna waliosema kuwa kuna maneno yaliyokadiriwa; yaani katika kipimo cha siku sita.

Wengine wakasema kuwa siku hapo ni fumbo la awamu, na kwamba Mwenyezi Mungu hakuumba huu ulimwengu kwa mkupuo mmoja bali ni kwa awamu sita ili kila kitu kiwe na kiwango na wakati wenye kukadiriwa.

Pia wako waliosema kwamba siku ni fumbo la vipindi na mabadiliko; kwamba yeye Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakuumba ulimwengu mwanzo

kama ulivyo sasa, bali uligeuka umbo mpaka umbo jingine, sawa na nadharia ya kukua mpaka kufikia umbo la sita na la mwisho, ambalo tunalionna hivi sasa.

Njia zote hizi ni za kufikiri, wala hatuna cha kutuwezesha kuipendekeza zaidi kauli mojawapo; ingawaje tumefuatilia tafsir za zamani na za sasa.

Kwa hiyo tunasema pamoja na yule anayesema: “Siku inawezekana kuwa ni awamu sita; au mambo sita; au siku sita katika siku za Mwenyezi Mungu ambazo hazipimwi kwa kiasi cha kipimo cha wakati wetu. Na inawezekana kuwa ni kitu kingine.

Hivyo basi, haifai kukata kabisa maana yoyote ya idadi hii, Na dhana ni jaribio la suluhu na kushindwa mbele ya kile kinachoitwa elimu – nayo si zaidi ya kudhani na kukadiria.”

**Kisha akatawala juu ya Arshi.**

Jumla hii inafasiriwa na ile inayofuatia - **Fahamuni Kuumba na amri ni yake.** Yaani yeye anamilki dunia na kupanga mambo yake. Mfano wake ni Aya isemayo:

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ يُدَبِّرُ الْأُمْرَ

﴿٣﴾

**Hakika Mola wenu ni Mwenyezi Mungu aliyeziumba mbingu na ardhi katika siku sita, kisha akatawala juu arshi anapangilia (kila) jambo...**” (10:3).

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amekuita kumiliki kwake na kupanga kwake mambo, kuwa ni kutawala juu ya kiti cha enzi (arshi). Kwa sababu mfalme hutawala mambo na kuyaendesha akiwa yuko kwenye kiti chake cha enzi (arshi).

Makusudio ya kusema hivyo ni kukurubisha maana, na sio tashbihi, (ukamfananisha Mungu na Mfalme wa duniani). Amesema: “Hakuna chochote kama mfano wake.”

**Huufunika usiku kwa mchana, uufuatiao upesi upesi.**

Hii ni katika mipango yake Mungu ya mambo ya ulimwengu. Maana yake ni kwamba usiku unafuata mchana na huufuatia haraka haraka na kuushinda ulivyokuwa kwa kufanya giza baada ya kuwa ni mwangaza. Mfano wa hayo ni kauli yake Mwenyezi Mungu:

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ ﴿١﴾

“Naapa kwa usiku unapofunika” (92:1)

Na vilevile kauli yake:

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَاهَا ﴿٤﴾

“Na (kwa) usiku unapolifunika” (91:4)

Yaani unaushinda mwanga wa jua.

**Na jua na mwezi na nyota zinatunika kwa amri yake.**

Yaani na ameumba sayari hizi zinazo kwenda kwa matakwa yake na kwen- da kwa mujibu wa hekima na masilahi, Mazungumzo kuhusu sayari hizi yanahitajia elimu ya falaki, Nasi hatujui chochote katika elimu hiyo.

**Fahamuni! Kuumba na amri ni yake.**

Huu ni ubainifu na tafsir ya kauli yake: Kisha akatawala juu ya arshi; kama tulivyotangulia kusema. Kuna Hadith isemayo: “Mwenye kudai

kwamba Mwenyezi Mungu amewajaalia waja kuwa na amri, basi amekufuru yaliyoteremshiwa Mitume yake, kutokana na kauli yake: “Fahamuni! Kuumba na amri ni yake”

**Ametukuka Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote** kwa umoja wake, ufalme wake na upangaji wake.

**Muombeni Mola wenu kwa unyenyekevu na kwa uficho.**

Maana ya mja kumwomba Mola wake sio kusema ‘Ewe Mwenyezi Mungu naomba rehema zako na maghufira yako’ Hapana! Isipokuwa kuomba kwa haki ni kumwogopa, kumcha na kushikamana na amri zake na kujiepusha na makatazo yake. Na pia sio makusudio ya kunyenyekea kusema: ‘Ewe Mwenyezi Mungu nanyenyekea kwako natubia, na najilinda kwako,’ bali mtu awe mkweli, mwenye ikhlasi katika anayoyasema na anayoyafanya.

Ama maana ya kwa uficho ni kutojifaharisha na kutangaza kwa watu kheri anayoifanya. Kwani hiyo ni aina ya kupetuka mipaka, na Mwenyezi Mungu anasema:

**Hakika yeye hawapendi wapetukao mipaka.**

Na Mwenyezi Mungu amekataza kujifaharisha kwa ibada na kufanya kheri.

## **MWENYEZI MUNGU AMEITENGENEZA VIZURI ARDHI NA BINADAMU AKAIHARIBU**

**Wala msifanye ufisadi katika ardhi baada ya kutengenea kwake.**

Mwenyezi Mungu aliitengeza vizuri ardhi hii kwa kuweka hazina zisizo na idadi za vitu vizuri na starehe za kiroho na kimaada. Kuanzia maumbile asili ya kupendeza hadi kwenye uzuri wa mwanamke, na kwenye utekelezaji urafiki hadi wema wa watoto; na kuanzia kukua maarifa na utalii hadi sauti za minong’ono na nyimbo mpaka yasiyo na mwisho.

Vitu vizuri vya kimaada katika vyakula ni pamoja na nafaka, mboga, nyama na matunda. Kila jamii katika hivyo ziko aina, rangi na maumbo mbali mbali.

Katika mavazi ni pamoja na sufu, pamba, ngozi na hariri. Kisha binadamu akagundua Nailoni na ataendelea kugundua ambayo tunadhani ni katika mambo yasiyowezekana kama alivyogundua namna ya kupunguza masafa ya ardhi na mbinguni kwa mtu kuweza kusafiri kwa madakika tu.

Ama katika nishati ni kuanzia miti hadi makaa ya mawe, na petroli hadi umeme, nguvu za jua (Solar) na Tonoradi. Miongoni mwa niliyosoma ni kwamba sayansi imevumbua katika petroli vioo visivyovunjika, mabomu ya Napalm, Nailoni, Samadi ya kemikali, sahani na mabomba ya kunyunyizia maji.

Vilevile imetoa vipodozi, kama vile poda, rangi za mdomo, wanja na rangi za kucha. Pia imetoa maua ya bandia, vifunikia meza, dawa za meno, wino na filamu. Na vingine vingi hadi kufikia aina elfu tatu walizozihisabu Wataalamu, bali ni mpaka kufikia isiyo na idadi ila kwa yule ambaye anajua kila kitu:

**وَإِنْ تَعُدُّوا نِعْمَتَ اللَّهِ لَا تَحْصُوهَا إِنَّ الْإِنْسَانَ لَظَلُومٌ كَفَّارٌ ﴿٣٤﴾**

**“Na mkizihesabu neema za Mwenyezi Mungu, hamtaweza kuzidhibiti, Hakika binadamu ni dhalimu mkubwa mwenye kukufuru sana” (14: 34)**

Aya hio ina matamko ya sana na kubwa pamoja na kutilia mkazo usisitizo huo, kwa neno hakika. Ni udhalimu gani mkubwa na utovu mkubwa wa shukran na ufisadi mkubwa kuliko kugeuza riziki njema kuwa mabomu ya Napalm, ya kuua watoto na kuwalemaza wakubwa, na hewa ya sumu inayochoma nyasi mbichi na kavu. Ama hayo mabomu ya Nuklia na Haidrojeni, ndiyo hayabakishi wala hayasazi!

Binadamu ameibadilisha neema kuwa kufuru na kuigeuza neema ya ardhi yake kuwa Jahanamu. Mwisho wa binadamu umefungamanishwa na manuklia. Mwenyezi Mungu ameweka katika ardhi hii starehe na riziki njema kwa waja wake.

Na yule dhalimu mkubwa asiye na shukrani ameweka mabomu ya Nuklia katika maghala yake na kwenye ndege zake zikizunguka angani, anangoja fursa tu aigeuze ardhi na vilivyomo kuwa majivu na mavumbi.

Hiyo ndiyo tafsir ya kauli yake Mwenyezi Mungu: “Wala msifanye ufisadi katika ardhi baada ya kutengenea kwake.” Kwa hiyo ni wajibu tumjue yule aliyeharibu ardhi baada ya Mwenyezi Mungu kututengenezea, na tumkatie njia kwa nyenzo zote tulizo nazo; angalau tumtangaze ajulikane na tumwite kwa jina lile alilopewa ‘Adui wa Mwenyezi Mungu na wa ubinadamu’ ili watu wote wawe na hadhari naye kutokana na vitimbi na hadaa zake.

**Na mwombeni kwa kuogopa na kwa kutumai.**

Kuwa na roho ya kukata tamaa ni hiyana. Kwa sababu hakuna maisha pamoja na kukata tamaa na kuacha kujihadhari pia ni hiyana kwa sababu ni kughurika. Njia ya kuokoka ni ile ya katika kati. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَيَرْجُونَ رَحْمَتَهُ وَيَخَافُونَ عَذَابَهُ﴾ (٥٧)

“Na wanatumai rehema zake na wanaogopa adhabu yake” (17:57)

Na amesema tena:

﴿نَبِيُّ عِبَادِي أَنِّي أَنَا الْغُفُورُ الرَّحِيمُ﴾ (٤٩) ﴿وَأَنَّ عَذَابِي هُوَ الْعَذَابُ الْأَلِيمُ﴾ (٥٠)

“Waambie waja wangu kwamba mimi ni mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu, Na kwamba adhabu yangu ndiyo adhabu iliyo chungu” (15: 49 – 50).

Mumin mwenye akili anafanya amali hali ya kuwa anamcha Mwenyezi Mungu asijeikataa amali yake kwa makosa katika amali hiyo, na wakati huo huo anatarajia kuokoka na kukubaliwa. Na yote hayo mawili, kuhofia na kutarajia yanaleta kujichunga na kufanya amali kwa uzuri.

**Hakika rehema ya Mwenyezi Mungu iko karibu na wanaofanya mema.**

Hapo kuna kuashiria kwamba mwenye kumwogopa Mwenyezi Mungu na akamtarajia, basi huyo ni katika watu wafanyao wema na kwamba Mwenyezi Mungu anawalipa wema kwa mfano wake.

﴿وَهُوَ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ حَتَّىٰ إِذَا أَقْلَّتْ سَحَابًا ثِقَالًا سُقْنَاهُ لِبَدٍ لَّيْمٍ﴾

﴿فَأَنْزَلْنَا بِهِ الْمَاءَ فَأَخْرَجْنَا بِهِ مِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ كَذَٰلِكَ نُخْرِجُ الْمَوْتَىٰ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ﴾ (٥٧)

57. Na yeye ndiye azipelekaye pepo kuwa ni bishara kabla ya kufika rehema yake. Hata zinapobeba mawingu mazito tunayasukuma kwa ajili ya mji uliokufa, Kisha tunateremsha hapo maji, Kwa hayo tukaotesha kila matunda. Kama hivi tutawafufua wafu ili mpate kukumbuka.

وَالْبَلَدُ الطَّيِّبُ يَخْرِجُ نَبَاتَهُ لِإِذْنِ رَبِّهِ وَالَّذِي خَبثَ لَا يَخْرِجُ إِلَّا نَجَسًا كَذَلِكَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ

لِقَوْمٍ يَشْكُرُونَ ﴿٥٨﴾

58. Na mji mzuri hutoa mimea yake kwa idhini ya Mola wake. Na ule ulio mbaya hau- toi ila kwa taabu tu. Namna hii tunazipambanua ishara kwa watu wanaoshukuru.

## **APELEKAYE PEPO KUWA BISHARA**

**Aya 57 – 58**

### **MAANA**

Na yeye ndiye azipelekaye pepo kuwa ni bishara kabla ya kufika rehema yake. Hata zinapobeba mawingu mazito tunayasukuma kwa ajili ya mji uliokufa, Kisha tunateremsha hapo maji, Kwa hayo tukaotesha kila matunda.

Makusudio ya rehema hapa ni mvua. Makusudio ya mawingu mazito ni yaliyotiwa uzito na mvuke wa maji. Na mji uliokufa ni ule usio na mimea.

Na kila matunda, makusudio yake ni ujumla wa kidesturi, sio wa kihalisi. Kwa ajili ya mji uliokufa ni kwa kukadiria, yaani kwa ajili ya uhai wa mji uliokufa.

Upepo huvuma, jua huyatia mvuke maji ya bahari na pepo hupandisha mvuke huu hadi juu; kisha ardhi huuvuta na kuanguka juu yake matone yenye kufuatana, yote haya na mfano wa hayo huja kwa mujibu wa desturi ya maumbile, Hilo halina shaka.

Lakini ni nani huyo aliyeweka maumbile haya na kuyapa utaratibu unaok- wenda nayo kwa jinsi moja katika mamilioni ya karne bila kugeuka au kubadilika? Je, maumbile yamepatikana kibahati tu. Je, kanuni, na desturi zimesimamiwa na sadfa tangu mwanzo hadi mwisho bila ya sababu yoyote? Vipi kisicho na nidhamu kizalishe nidhamu? Na kisicho na utambuzi kizalishe utambuzi?

Isitoshe je, maswali haya yana majibu ya kuingilika akilini na kukubalika zaidi ya kuwako muumbaji mwenye hekima, Aliyeyaleta maumbile na akayapa utaratibu na kanuni. Na kwake yeye kinaishia kila kitu na kuhitajia kila kitu, wala yeye hahitaji chochote?

Kwa hiyo upepo, mvua na kuhuyishwa mji uliokufa hunasibishwa kwenye desturi ya maumbile moja kwa moja na kupitia kwa muumbaji wa maumbile.

**Kama hivi tutawafufua wafu, ili mpate kukumbuka.**

Wakanushaji husema: Vipi tutaamini ufufuo na hatujaona yeyote aliyerudiwa na uhai baada ya kufa kwake? Wanasema hivi na wao wanaona kwa macho ardhi baada ya kufa inavyopata uhai, lakini wao wamesahau kuwa sababu ni moja na kwamba hakuna tofauti ila katika sura tu, ndipo Mwenyezi Mungu akawakumbusha hilo ili wao wanufaike kwa ukumbusho au iwalazimu hoja.

**Na mji mzuri hutoa mimea yake kwa idhini ya Mola wake. Na ule ulio mbaya hautoi ila kwa taabu tu.**

Kwa idhini ya Mola wake ni fumbo la kutoa kingi kutokana na uchache na kwa wepesi, na kidogo ni fumbo la kutoa kichache kwa uzito na ugumu.

Wafasiri wengi wanafananisha moyo wa mumin na kafiri, na mwema na mwovu na ardhi ambayo wote wameumbwa kutokana nayo. Wajihhi wa kufananisha ni kwamba ardhi yote ingawaje ni jinsi moja, lakini kuna ile iliyo nzuri ambayo ikinywa maji husisimka na kututumka na kumea kila namna ya mimea mizuri.

Na kuna nyingine iliyosusuwaa imefungika inapinga kheri na utengenefu, inapojiwa na kheri yoyote ni kama kwamba inapelekwa kufa.

**Namna hii tunazipambanua ishara kwa watu wanaoshukuru.**

Mwenyezi Mungu hupiga mifano hii na mengineyo kwa wote kwa mwovu na mwema, lakini wema ndio wanufaikao nayo na kumshukuru Mwenyezi Mungu. Ama kwa mnasaba wa waovu. Basi ni hoja juu yao inayokata nyudhuru na sababu zao.



## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

لَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ فَقَالَ يَا قَوْمِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٥٩﴾

59. Hakika tulimtuma Nuh kwa watu wake. Akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, hamna Mungu mwingine zaidi yake. Hakika mimi ninawahofia na adhabu ya siku iliyo kuu.

قَالَ الْمَلَأُ مِنْ قَوْمِهِ إِنَّا لَنَرَاكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٦٠﴾

60. Wakasema wakuu wa watu wake: Hakika sisi tunakuona umo katika upotofu ulio wazi.

قَالَ يَا قَوْمِ لَيْسَ بِي ضَلَالَةٌ وَلَكِنِّي رَسُولٌ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٦١﴾

61. Akasema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika upotevu, lakini mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola wa walimwengu wote.

أَبْلَغُكُمْ رَسُولَاتِ رَبِّي وَأَنْصَحُ لَكُمْ وَأَعْلَمُ مِنَ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦٢﴾

62. Nawafikishia ujumbe wa Mola wangu na nawanasihi; na ninajua kwa Mwenyezi Mungu msiyoyajua.

أَوْعَجِبْتُمْ أَنْ جَاءَكُمْ ذِكْرٌ مِنْ رَبِّكُمْ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنْكُمْ لِيُنذِرَكُمْ وَلِتَتَّقُوا وَلَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٦٣﴾

63. Je, mnastaajabu kuwafikia mawaidha kutoka kwa Mola wenu kupitia mtu anayetokana na nyinyi ili awaonye na ili muwe na takua, na ili mpate kurehemiwa? ”

فَكَذَّبُوهُ فَأَنْجَيْنَاهُ وَالَّذِينَ مَعَهُ فِي الْفُلْكِ وَأَعْرَفْنَا الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا عَمِينَ ﴿٦٤﴾

64. Basi walimkadhibisha. Nasi tukamwokoia yeye na waliokuwa pamoja naye katika jahazi, na tukawazamisha waliozikadhibisha ishara zetu, Hakika wao walikuwa watu vipofu.

NUH

**Aya 59 – 64**

### MAANA

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kusema, katika Aya 35 ya Sura hii: “Enyi Wanadamu! Watakapowafikia Mitume kutoka miongoni mwenu” Anaashiria, katika Aya hii na zinazofuatia, kisa cha Mitume Nuh, Hud, Swaleh, Nabii Lut, na Shuaib <sup>(a.s)</sup>.

Mwenyezi Mungu amekifupisha sana hapa kisa cha Nuh, ambapo ametosheka tu na kutaja majibizano kati yake na jamaa zake na namna walivyoeputa mwito na jinsi walivyostaajabu kuchagua Mwenyezi Mungu Mtume kutokana na wao.

Na kwamba yeye (s.w.t) aliwagharikisha wakadhibishaji na kuwaokoa waumini.

Hakika tulimtuma Nuh kwa watu wake.

Tabrasi anasema katika Majamaul-Bayan: “Yeye ni Nuh bin Mulk bin Matoshalkh bin Ukhnun, Mtume Idris. Na Nuh ni Mtume wa kwanza baada ya Idris.”

Inasemekana kuwa yeye alikuwa ni seremala na kwamba alizaliwa mwaka aliokufia Adam, Ama sisi, hatujui chimbuko la kusemekana huku.

**Akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, hamna Mungu mwingine zaidi yake. Hakika mimi ninawahofia na adhabu ya siku iliyo kuu.**

Aliufupisha Nuh <sup>(a.s)</sup> ujumbe aliouchukua kwa watu wake kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa jumla moja tu: Mwabuduni Mwenyezi Mungu peke yake kwa sababu hakuna Mola mwingine isipokuwa yeye. Na kwam- ba mwito wake huo kwao ni kuwahurumia na adhabu ya siku ya Kiyama.

**Wakasema wakuu wa watu wake: Hakika sisi tunakuona umo katika upotofu ulio wazi.**

Wakamshutumu kwa upotevu na usafihi si kwa jingine ila tu kwa vile amewakataza walioyazoea na kuyarithi ya kuabudu mawe.

Hivi ndiyo alivyo kila safihi na kila mpotevu, humzulia ule ugonjwa wake kila anayekwenda kwenye njia ya uongofu.

**Akasema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika upotevu, lakini mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola wa walimwengu wote. Nawafikishia ujumbe wa Mola wangu na ninawanasihi; na ninajua kwa Mwenyezi Mungu msiyoyajua.**

Aliwajibu kwa kukanusha upotevu yeye mwenyewe na kujisifu kwa sifa tukufu kwamba yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, amempeleka ili awaokoe na upotevu na kuangamia, na kwamba yeye ni mtoaji nasaha mwaminifu, na anajua kutoka kwa Mwenyezi Mungu umoja na uadilifu wake. Na mwenye kuwa na sifa hizi hawezi kuwa mpotevu.

**Je, mnastaajabu kuwafikia mawaidha kutoka kwa Mola wenu kupitia mtu anayetokana na nyinyi ili awaonye na ili muwe na takua na ili mpate kurehemiwa?**

Watu wake walimwaambia wewe ni mtu tu kama sisi, Lau Mwenyezi Mungu angelitaka kutuma mjumbe angelimtuma Malaika. Akawajibu kwamba hakuna ajabu kutuma Mwenyezi Mungu mtu kwa watu wake akiwa hana masilahi yoyote au lengo lolote ila kuwaongoza kwenye lile lililo na kheri yao na utengenefu wao, isipokuwa ajabu ni kupuuzwa na kuachwa bila ya mwongozi.

Razi anasema huu ni utaratibu wa lengo zuri, kwani lengo la kutuma ujumbe ni kuonya, na lengo la kuonya ni takua, na lengo la takua ni kufuzu rehema ya Mwenyezi Mungu katika nyumba ya akhera.

**Basi walimkadhibisha, Nasi tukamwokoia yeye na waliokuwa pamoja naye katika jahazi, na tukawazamisha waliozikadhibisha ishara zetu, Hakika wao walikuwa watu vipofu.**

Milango ya mbinguni ilifunguka ikatoa maji na ardhi ikachimbuka chemchemi. Hapo Mwenyezi Mungu akawaangamiza madhalimu wenye kukadhibisha na akaokoka Nuh <sup>(a.s)</sup> na waumini aliokuwa pamoja nao. Yatakuja maelezo kwa ufafanuzi kuhusu Nuh <sup>(a.s)</sup> na watu wake katika Sura iliyoitwa kwa jina lake (71) inshaallah.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا هُمُ الْكَافِرُونَ ﴿٦٥﴾

65. Na kwa Adi (tulimpeleka) ndugu yao Hud. Akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, nyinyi hamna Mungu mwingine zaidi yake, Basi hamwogopi?

﴿قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَوْمِهِ إِنَّا لَنَرَاكَ فِي سَفَاهَةٍ وَإِنَّا لَنَظُنُّكَ مِنَ الْكَاذِبِينَ﴾ ﴿٦٦﴾

66. Wakasema wakuu waliokufuru katika watu wake: Hakika sisi tunakuona umo katika upumbavu na tunakudhania ni katika waongo.

﴿قَالَ يَا قَوْمِ لَيْسَ بِي سَفَاهَةٌ وَلَكِنِّي رَسُولٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ﴾ ﴿٦٧﴾

67. Akasema: Enyi watu wangu! Mimi sina upumbavu, lakini mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola wa walimwengu.

﴿أُبَلِّغُكُمْ رِسَالَاتِ رَبِّي وَأَنَا لَكُمْ نَاصِحٌ أَمِينٌ﴾ ﴿٦٨﴾

68. Nawafikishia ujumbe wa Mola wangu na mimi kwenu nimtoa nasaha, mwaminifu.

﴿أَوْعَجِبْتُمْ أَن جَاءَكُمْ ذِكْرٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنكُمْ لِيُنذِرَكُمْ وَأَذْكُرُوا إِذْ جَعَلْنَا خُلَفَاءَ مِن بَعْدِ قَوْمِ نُوحٍ وَرَادَكُمْ فِي الْخَلْقِ بَسْطَةً فَادْكُرُوا آلَاءَ اللَّهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾ ﴿٦٩﴾

69. Je, mnastaajabu kuwafikia ukumbusho kutoka kwa Mola wenu kupitia mtu anayetokana na nyinyi ili awaonye. Na kumbukeni alivyowafanya makhalifa baada ya watu wa Nuh, Na akawazidisha nguvu katika umbo. Basi kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu ili mpate kufaulu.

﴿قَالُوا أَجِئْنَا لِنَتَّعِبِدَ اللَّهَ وَحْدَهُ وَنَذَرَ مَا كَانَ يَعْبُدُ آبَاؤُنَا فَأُنَبِّئْنَا بِمَا نَعْبُدُ إِنَّ كُنتَ مِنَ الصَّادِقِينَ﴾ ﴿٧٠﴾

﴿الصَّادِقِينَ﴾ ﴿٧٠﴾

70. Wakasema: Je, umetujia ili tumwabudu Mwenyezi Mungu peke yake na tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu? Basi tulettee unayotuahidi ukiwa ni miongoni mwa wasemaio kweli.

﴿قَالَ قَدْ وَقَعَ عَلَيْكُمْ مِّن رَّبِّكُمْ رَجْسٌ وَعَصَبٌ أُنزِلَ لِيُنذِرَ فِي سَمَاءٍ سَمِيَّتُوهَا أَنْتُمْ

﴿وَأَبَاؤُكُمْ مَا نَزَّلَ اللَّهُ بِهَا مِن سُلْطَانٍ فَانظُرُوا إِلَيَّ مَعَكُمْ مِّنَ الْمُنتَظِرِينَ﴾ ﴿٧١﴾

71. Akasema: Hakika adhabu na ghadhabu zimekwishawaangukia kutoka kwa Mola wenu. Je, mnanijadili katika majina mliyoyaita nyinyi na baba zenu ambayo Mwenyezi Mungu hakuyateremshia dalili yoyote? Basi ngojeni; mimi pia ni pamoja nanyi katika wangojao.

﴿فَأَنجَيْنَاهُ وَالَّذِينَ مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَقَطَعْنَا دَابِرَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَمَا كَانُوا مُؤْمِنِينَ﴾ ﴿٧٢﴾

72. Basi tukamwokoia yeye na waliokuwa pamoja naye kwa rehema zetu na tukakata mizizi ya wale waliokadhibisha ishara zetu, na hawakuwa wenye kuamini.

## HUD

Aya 65 – 72

## MAANA

Imesemwa katika Tafsir Al-Manar kwa kunukuliwa kutoka kwa Is-haq bin Bashar na Ibn Asakir: “Nabii Hud <sup>(a.s)</sup> ndiye wa kwanza kuzungumza Kiarabu, alikuwa na watoto wane: Qahtan, Muq-hit, Qahit na Faligh ambaye

ni baba wa Mudhar. (Abu Mudhar) Na Qahtan ni baba wa Yemen (Abul-Yaman), Ama Qahit na Muqhit hawana kizazi.”

Wafasiri wamesema: Watu wa Hud <sup>(a.s)</sup> walikuwa ni katika kizazi cha Nuh <sup>(a.s)</sup> na walikuwa kwenye dini yake. Baada ya muda kuwa mrefu, shetani aliwachezea, wakaabudu masanamu na wakafanya ufisadi katika ardhi.

Katika Tafsir Tabari imeelezwa kuwa Imam Ali alimwambia mtu mmoja kutoka Yemen: “Je, umeona katika ardhi ya Hadharamauti chungu ya tifu-tifu jekundu iliyochanganyika na madongo mekundu, ina mipilipili na mikunazi mingi sehemu kadha wa kadha?” Akasema: “Ndio Ewe Amirul Muminin, wallah unapasifu sifa ya mtu aliyepaona.” Akasema Amirul-Muminina: “Hapana, nimehadithiwa”. Yule mtu akasema: “Kwani pana nini Ewe Amirul-Muminin?” Akasema: “Pana kaburi ya Nabii Hud <sup>(a.s)</sup>”

Ikiwa ni sahih Riwaya hii, basi itabidi iondolewe sehemu iliyoandikwa kwenye kaburi ya Imam Ali, isemayo: Amani ishuke juu yako na juu ya jirani zako Hud na Swaleh, ila ikiwa ujirani wenyewe ni katika akhera sio hapa duniani, au iwe mwili wa Hud ulihamishwa baada ya kufa Imam.

Aya hizi zilizoshuka kuhusu kisa cha Hud <sup>(a.s)</sup> zinaafikiana na Aya zilizotangulia, ambazo zimeshuka kuhusu kisa cha Nuh <sup>(a.s)</sup> kimaneno na kimaana isipokuwa katika mambo yafuatavyo:-

Nuh <sup>(a.s)</sup> aliwaambia watu wake: “Hakika mimi nawahofia na adhabu ya siku iliyo kuu”. Na Hud <sup>(a.s)</sup> akawaambia watu wake: **Basi hamwogopi?** Hiyo ni kwa sababu kabla ya Nuh <sup>(a.s)</sup> hakukuwahi kutokea mfano wa adhabu hiyo, ambayo ni tufani. Na watu wa Hud <sup>(a.s)</sup> walikuwa wakijua, ndipo akawahadharisha na akawaamrisha kumwogopa Mwenyezi Mungu, kwa kuacha kumshirikisha na kumthibitishia umoja.

Nuh <sup>(a.s)</sup> aliambiwa na watu wake: ‘Hakika sisi tunakuona umo katika upotofu ulio dhahiri.’ Na watu wa Hud <sup>(a.s)</sup> walimwambia:

**Hakika sisi tunakuona umo katika upumbavu, na hakika sisi tunakudhania ni katika waongo.**

Kwa sababu Nuh <sup>(a.s)</sup> alikuwa akitengeneza safina mahali pasipo na bahari wala mito. Na kazi hii ukitazama kwa dhahiri ni ujinga na upotevu.

Ama Hud <sup>(a.s)</sup> hakufanya namna hii, isipokuwa aliwafanya wapumbavu watu wake kwa kuabudu masanamu. Kwa hiyo nao wakamrudishia na kumnasibishia upumbavu.

Nuh <sup>(a.s)</sup> aliwaambia watu wake: ‘Ili mpate kurehemiwa.’ Na Hud <sup>(a.s)</sup> aliwaambia watu wake:

**Ili mpate kufaulu.**

Nuh <sup>(a.s)</sup> alikusudia rehema, na kuondolewa adhabu na Hud <sup>(a.s)</sup> naye akakusudia kufaulu na kuongoka kwenye njia iliyo sawa, Maana zote mbili zinaungana, haziachani.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja katika Aya hizi mambo ambayo watu wa Hud <sup>(a.s)</sup> walimwambia mtume wao, lakini hakutaja kama watu wa Nuh <sup>(a.s)</sup> walimwambia Mtume wao nayo ni:

**Wakasema: Je, Umetujia ili tumwabudu Mwenyezi Mungu peke yake na tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu?**

Ibara inayotumiwa na kila jahili na mwenye kufuata. Basi tulettee unayotuahidi ukiwa ni miongoni mwa wasemao kweli”

Likaja jawabu la mkato na la haraka kutoka kwa Mtume akasema: Hakika adhabu na ghadhabu zimekwishwaangukia kutoka kwa Mola Wenu. Maana ya kuwaangukia hapa ni kuwawajibikia, na makusudio ya adhabu ni sababu yenye kuwajibisha adhabu.

Je, Mnanijadili katika majina mliyoyaita nyinyi na baba zenu ambayo Mwenyezi Mungu hakuyateremshia dalili yoyote?

Waungu mnaowaabudu hawako, na kila kisichokuweco hakina athari wala dalili. Kwa hali hii majina waliyopewa yanakuwa ni maneno matupu yasiyokuwa na maana.

Basi ngojeni, mimi pia ni pamoja nanyi katika wangojao.

Hili ni jibu la kauli yao: “Basi tulettee unayotuahidi ukiwa miongoni mwa wasema kweli.”

Basi tukamwoko na waliokuwa pamoja naye kwa rehema zetu na tukakata mizizi ya wale waliokadhibisha ishara zetu, na hawakuwa wenye kuamini.

Kukatwa mizizi, ni kuangamizwa mpaka wa mwisho wao. Amebainisha Mwenyezi Mungu mahali pengine aina ya adhabu aliyowaangamizia watu wa Hud <sup>(a.s)</sup>, aliposema:

وَأَمَّا عَادٌ فَأُهْلِكُوا بِرِيحٍ صَرْصَرٍ عَاتِيَةٍ ﴿٦﴾ سَخَّرَهَا عَلَيْهِمْ سَبْعَ لَيَالٍ وَتَمَازِيَةَ أَيَّامٍ حُسُومًا فَتَرَى الْقَوْمَ فِيهَا صَرْعَى كَأَنَّهُمْ أُعْجَازٌ نَقْلٍ خَازِيَةٍ ﴿٧﴾ فَهَلْ تَرَى لَهُمْ مِّن بَاقِيَةٍ ﴿٨﴾

“Na ama Adi waliangamizwa kwa upepo mkali usiozulika, Aliwapelekea masiku saba na siku nane mfululizo. Utawaona watu wameanguka kama kwamba ni magogo ya mitende yaliyo wazi, Basi je, unamwona mmoja wao aliyebaki?” (69: 6 – 8).

Inshallah yatakuja maelezo zaidi kuhusu Hud <sup>(a.s)</sup> na watu wake katika Sura (11) iliyoitwa kwa jina lake.

وَأِلَى ثَمُودَ أَخَاهُمْ صَالِحًا قَالَ يَا قَوْمِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِّن إِلَهٍ غَيْرُهُ قَدْ جَاءتْكُمْ بَيِّنَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ هَذِهِ نَاقَةُ اللَّهِ لَكُمْ آيَةٌ فَذَرُوهَا تَأْكُلْ فِي أَرْضِ اللَّهِ وَلَا تَمَسُوهَا بِسُوءٍ فَيَأْخُذَكُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٣﴾

73. Na kwa Thamud (tulimpeleka) ndugu yao Swaleh. Akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, nyinyi hamna Mungu mwingine zaidi yake. Hakika umekwishawafikia ubainifu kutoka kwa Mola wenu. Huyu ni ngamia wa Mwenyezi Mungu aliye ishara kwenu, Basi mwacheni ale katika ardhi ya Mwenyezi Mungu, wala msimtie dhara, isije ikawashika adhabu ya Mwenyezi Mungu iumizayo.

وَأذْكُرُوا إِذْ جَعَلَكُمْ خُلَفَاءَ مِن بَعْدِ عَادٍ وَبَوَّأَكُمْ فِي الْأَرْضِ تَتَّخِذُونَ مِنْهُ سُهُ وِلَهَا قُصُورًا وَتَنْحِتُونَ الْجِبَالَ بُيُوتًا فَاذْكُرُوا آيَةَ اللَّهِ وَلَا تَعْتُوا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٧٤﴾

74. Na kumbukeni alipowafanya makhalifa baada ya Ad na kuwakalisha katika ardhi mkajenga makasri katika nyanda zake na mkachonga majumba katika majabali, Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu, wala msifanye ufisadi katika ardhi.

قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا مِن قَوْمِهِ لِلَّذِينَ اسْتَضَعُّوهُ لِمَن آمَنَ مِنْهُمْ أَتَعْلَمُونَ أَنَّ صَالِحًا مُّرْسَلٌ مِّن رَّبِّهِ قَالُوا إِنَّا بِمَا أُرْسِلَ بِهِ مُؤْمِنُونَ ﴿٧٥﴾

75. Wakasema wakuu wa watu wake waliotakabari kuwaambia walio wanyonge walioamini miongoni mwao: Je, mwajua kuwa Swaleh ametumwa na Mola wake? Wakasema: Hakika tunayaamini yale aliyotumwa.

﴿قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا بِالَّذِي آمَنْتُمْ بِهِ كَافِرُونَ﴾ (٧٦)

76. Wakasema wale waliotakabari: Hakika Sisi tunayakataa yale mnayoyaamini.

﴿فَعَفَرُوا التَّافَةَ وَعَتَوْا عَنْ أَمْرِ رَبِّيهِمْ وَقَالُوا يَا صَالِحُ ائْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِنْ كُنْتَ مِنَ الْمُرْسَلِينَ﴾

﴿٧٧﴾

77. Wakamchinja ngamia na wakaasi amri ya Mola wao na Wakasema: Ee Swaleh! Tuletee unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa Mitume.

﴿فَأَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جَاثِمِينَ﴾ (٧٨)

Ukawanyakua mtetemeko wakawa wameanguka hawajimudu majumbani mwao.

﴿فَتَوَلَّى عَنْهُمْ وَقَالَ يَا قَوْمِ لَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ رَسُولَ رَبِّي وَنَصَحْتُ لَكُمْ وَلَكِنْ لَا تُحِبُّونَ﴾

﴿التَّاصِحِينَ﴾ (٧٩)

79. Basi Swaleh akawaacha na kusema: Enyi watu wangu! Kwa hakika nimewafikishia ujumbe wa Mola wangu na nikawanasihi, lakini hampendi wenye nasaha.

## SWALEH

Aya Ya 73 – 79

### MAANA

Na kwa Thamud (tulimpeleka) ndugu yao Swaleh. Akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, nyinyi hamna Mungu mwingine zaidi yake.

Thamud ni kabila katika Waarabu. Waliitwa kwa jina la babu yao Thamud bin Amir. Makazi yao yalikuwa Hijr, baina ya Hijaz na Sham mpaka Wadil-qura. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَلَقَدْ كَذَّبَ أَصْحَابُ الْحِجْرِ الْمُرْسَلِينَ﴾ (٨٠)

“Na hakika watu wa Hijr walikadhibisha Mitume (15:80).

Huyu ni ngamia wa Mwenyezi Mungu aliye ishara kwenu.

Kikundi cha Wafasiri wamesema kuwa watu wa Nabii Swaleh (a.s) walimwomba awatolee ngamia kutoka kwenye jiwe; na yeye alimwomba Mola wake hilo. Basi jiwe likashikwa na uchungu wa kuzaa kama mwanamke, likazaa ngamia wa kike mchangamfu mwenye manyoya.

Sisi tunaamini kiujumla kwamba ngamia alikuwa ni ubainifu na ishara kutoka kwa Mwenyezi Mungu; na kwamba hakuja kwa njia ya kawaida; na Mwenyezi Mungu alimtegemeza kwake kwa kumwadhimisha. Tunaamini hivi, bila ya kuongeza chochote ambacho hakikuelezwa na Wahyi au Hadith Mutawatir iliyotoka kwa Maasum.

Basi mwacheni ale katika ardhi ya Mwenyezi Mungu, wala msimtie dhara, isije ikawashika adhabu ya Mwenyezi Mungu iumizayo.

Swaleh <sup>(a.s)</sup> aliwaamrisha watu wake wamuache ngamia akae katika ardhi ya Mwenyezi Mungu, na akawahadharisha na mwisho mbaya ikiwa watamtaaradhi kwa udhia. Kisha akawaambia:

**Na kumbukeni alipowafanya makhalifa baada ya Ad.**

Mwenyezi Mungu aliangamiza kabila la Ad kwa dhambi zao, akawakumbusha neema hii ya kuwa makhalifa. Vilevile aliendelea kuwakumbusha kwa kuwaambia:

**Na kuwakalisha katika ardhi mkajenga makasri kati- ka nyanda zake na mkachonga majumba katika majabali.**

Kauli hii inafahamisha kuwa Thamud waliishi katika majengo yaliyoendelea na kwamba walikuwa katika neema na starehe.

**Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu, wala msifanye ufisadi katika ardhi.**

Baada ya kuwakumbusha neema alizowamiminia Mwenyezi Mungu aliwaamrisha wakumbuke na washukuru neema hizo na kuwakataza wasifanye ufisadi. Hilo ni kuwahadharisha na uovu wa Mwenyezi Mungu na adhabu yake.

**Wakasema wakuu wa watu wake waliotakabari kuwaambia wale walio wanyonge walioamini miongoni mwao.**

Wale wapenda anasa katika watu wa Swaleh <sup>(a.s)</sup> waliendelea na utaghuti na kung'ang'ania kuabudu masanamu. Ama wale wanyonge kuna walioamini katika wao na waliobakia kwenye shirki kwa kuwafuata wapenda anasa. Basi hawa wakawaambia wale walioamini katika mafukara na wanyonge:

**Je, mnajua kuwa Swaleh ametumwa na Mola wake?**

Waliwauliza wanyonge swali hili kwa kupinga na kutishia au kwa dharau na stihzai.

**Wakasema – wale wanyonge – Hakika tunayaamini yale aliyotumwa.**

Waliyasema haya bila ya kujali vitisho na stizai. Kwa sababu wao wana yakini na dini yao.

**Wakasema wale waliotakabari kuwaambia wale wanyonge: Sisi tunayakataa yale mliyoyaamini.**

Pamoja na dalili na ubainifu mkataa juu ya utume wa Swaleh. Kwa sababu masilahi yao ni zaidi kuliko dini za Mwenyezi Mungu na dalili ya kiakili. Razi anasema Aya hii ni miongoni mwa hoja kubwa kuwa kiburi kinatokana na wingi wa mali na jaha. Kwa sababu wingi huo ndio uliowafanya waendele kuasi na kukufuru.

**Wakamchinja ngamia na wakaasi amri ya Mola wao.**

Hakika yao inadhihirisha uasi huu, na kwamba wao hawajali isipokuwa masilahi yao tu. Wakamchochea Nabii Swaleh <sup>(a.s)</sup> kuleta adhabu haraka na wakasema:

**Ee Swaleh!: Tuletee unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa Mitume.**

Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakuwachelewesha kuwalipa inadi hii Ukawanyakua mtetemeko wakawa wameanguka hawajimudu majumbani mwao<sup>1</sup>.

---

1 Makusudio ya mtetemeko hapa ni rindimo, na kutojimudu ni kuangamia.

Mwenyezi Mungu anasema katika Aya nyingine:

﴿٤٣﴾ وَفِي نَمُودٍ إِذْ قِيلَ لَهُمْ تَمَتَّعُوا حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٤٣﴾ فَعَتَوْا عَنْ أَمْرِ رَبِّهِمْ فَأَخَذَتْهُمُ الصَّاعِقَةُ وَهُمْ  
يَنْظُرُونَ ﴿٤٤﴾

Na katika Thamud walipoambiwa jifurahisheni kwa muda mdogo tu. Wakaasi amri ya Mola wao ikawanyakua rindimo na huku wanaona.” (51:43-44)

Basi Swaleh akawaacha na akasema: Enyi watu! Kwa hakika nimewafikishia ujumbe wa Mola wangu na nikawanasihi, lakini hampendi wenye nasaha.

Nabii Swaleh <sup>(a.s)</sup> alipoona adhabu iliyowapata watu wake aliachana nao na akijiepusha na mwisho wao huu walioutaka wenyewe kwa uasi na jeuri.

Razi anasema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w): “Ewe Ali! Mwovu zaidi wa kwanza ni mchinja ngamia wa Swaleh, na mwovu zaidi wa mwisho ni muuaji wako”.

Tutarudia habari ya Nabii Swaleh <sup>(a.s)</sup> mara nyingine inshallah.



## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE

﴿٨٠﴾ وَلَوْطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ أَتَأْتُونَ الْفَاحِشَةَ مَا سَبَقَكُمْ بِهَا مِنْ أَحَدٍ مِنَ الْعَالَمِينَ ﴿٨٠﴾

80. Na Lut alipowaambia watu wake: Je, mnafanya uchafu ambao hajawatangulia yeyote kwa hilo katika walimwengu.

﴿٨١﴾ إِنَّكُمْ لَتَأْتُونَ الرِّجَالَ شَهْوَةً مِنْ دُونِ النِّسَاءِ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ مُّسْرِفُونَ ﴿٨١﴾

81. Hakika nyinyi mnawaendea wanaume kwa matamanio badala ya wanawake! Bali nyinyi ni watu warukao mipaka.

﴿٨٢﴾ وَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَخْرِجُوهُمْ مِنْ قَرْيَتِكُمْ إِنَّهُمْ أَنْفُسٌ يَتَطَهَّرُونَ ﴿٨٢﴾

82. Na halikuwa jibu la watu wake isipokuwa kusema: Watoeni mjini mwenu, maana hao ni watu wanaojitakasa.

﴿٨٣﴾ فَأَنْجَيْنَاهُ وَأَهْلَهُ إِلَّا امْرَأَتَهُ كَانَتْ مِنَ الْغَابِرِينَ ﴿٨٣﴾

83. Tukamwokoia yeye na jamaa zake isipokuwa mkewe alikuwa miongoni mwa waliobakia.

﴿٨٤﴾ وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَطَرًا فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُجْرِمِينَ ﴿٨٤﴾

84. Na tukawamiminia mvua, basi tazama jinsi ulivyokuwa mwisho wa waovu.

### LUT

Aya 80 – 84

### MAANA

Na Lut alipowaambia watu wake: Je, mnafanya uchafu.

Amenukuu Mwenye Tafsir Al-Manar kutoka Kitabu Ansabul Arabiya ya kwamba Nabii Lut ni mwana wa ndugu wa Nabii Ibrahim Khalili <sup>(a.s)</sup>. Na kwamba yeye alizaliwa kaldayo (Chaldeans)

Hiyo ni sehemu iliyo upande wa Mashariki ya kati kusini mwa Iraq upande wa Magharibi katika jimbo la Basra, Sehemu hiyo wakati huo ikiitwa nchi ya Babel. Kisha Nabii Lut akasafiri na Nabii Ibrahim <sup>(a.s)</sup> ami yake hadi sehemu iliyo baina ya mito miwili, sehemu inayozungukwa na Dijla, mamlaka ya Ashwar, Kisha Nabii Ibrahim <sup>(a.s)</sup> akamweka mashariki mwa Jordan.

Ambao hajawatangulia yeyote kwa hilo katika walimwengu.

Inafahamisha kuwa watu wa Nabii Lut <sup>(a.s)</sup> ndio wa kwanza kuzusha aina hii ya ufisadi.

Hakika nyinyi mnawaendea wanaume kwa matamanio badala ya wanawake.

Hii ni tafsir ya uchafu; na makusudio yake ni ulawiti ambao kisasa unaitwa kinyume na maumbile au kitendo kibaya.

Bali nyinyi ni watu warukao mipaka.

Mmepetuka mpaka katika kila kitu, mpaka mmefikilia kiasi hiki cha upotofu ambao unakataliwa na maumbile na kuhalifu desturi ya maisha.

Na halikuwa jibu la kaumu yake isipokuwa kusema: Watoeni mjini mwenu, maana hao ni watu wanaojitakasa.

Ndio! Utakatifu na kujistahi ni dhambi kwa mzinzi mchafu; na uaminifu ni kosa kwa mhaini kibaraka. Watoeni, maana hao ni watakatifu. Hivi ndivyo jamii chafu hukataa wasafi na wema, si kwa lolote ila kwamba wao ni wasafi. Usawa ni kinyume cha hivyo.

Tukamwoko ya yeye na jamaa yake isipokuwa mkewe alikuwa miongoni mwa waliobaki.

Makusudio ya jamaa yake ni kila aliyeamini, ni sawa awe ni katika familia yake au la. Kubaki ni kwamba mke wa Nabii Lut alibakia pamoja na walioangamia, na hakufuatana naye wakati alipoondoka usiku kukimbia adhabu, kwa sababu alikuwa mnafiki akila njama pamoja na washirikina dhidi ya mumewe. Inasemekana kuwa jina lake ni Wahila.

Mwenyezi Mungu ametumia dhamir ya wanaume “waliokuwa nyuma” kwa vile waume walikuwa wengi zaidi.

Yalimpata mke wa Nabii Lut yale yaliyowapata washirikina kwa sababu yeye ni katika wao, wala haukumfaa uhusiano wake na Mtume wa Mwenyezi Mungu na kuwa naye. Kuna Hadith isemayo: “Mtu yu pamoja na kipenzi chake.”

**Na tukawamiminia mvua.**

Amebainisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) adhabu aliyowateremshia kuwa ni aina ya mvua, lakini ni ya mawe sio ya maji, kama ilivyoelezwa katika Aya isemayo:

﴿۸۲﴾ وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهَا حِجَارَةً مِّن سِجِّيلٍ

**Tukawateremshia mvua ya changarawe za udongo mkavu. (11:82)**

**Utakuja ufafanuzi huko mbele inshallah.**

Basi tazama jinsi ulivyokuwa mwisho wa waovu.

Ni adhabu iumizayo, na mwenye akili ni yule anayepata funzo kwa wengine.

**Utauliza:** manabii Nuh, Hud na Swaleh <sup>(a.s)</sup> kila mmoja aliwalingania watu wake kwenye ibada ya Mwenyezi Mungu peke yake; kama ilivyoelezwa katika Aya zilizotangulia.

Lakini Nabii Lut aliwalingania watu wake kujizuia na uchafu; kama inavyoelezwa katika Aya hizi. Je, hii inamaanisha kuwa watu wa Nabii Lut walikuwa ni watu wa Tawhid, lakini walikuwa waovu kwa kitendo chao hiki kibaya?

**Jibu:** watu wa Nabii Lut walikuwa makafiri, na aliwalingania kwa Mwenyezi Mungu mmoja, na kuwakataza na shirk na ukafiri, kama alivyowakataza ulawiti; kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu:

﴿۱۶۳﴾ إِيَّا لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ ﴿۱۶۲﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا

**“Hakika mimi kwenu ni Mtume Mwaminifu. Basi mcheni Mwenyezi Mungu na nitiini”**

(26: 162-163).

Isipokuwa alijishughulisha sana na uchafu huu, kwa vile ulikuwa umeenea sana kwao, na kuwafanya kuwa waasi wenye kuipinga haki na kuthubutu kuwakadhibisha Mitume wa Mwenyezi Mungu.

Yamekongamana madhehebu ya Kiislamu kwa kauli moja kuharamisha ulawiti, na kwamba ni katika madhambi makubwa, Wametofautiana katika adhabu yake.

Hanafi anasema ni kuaziriwa kwa aonavyo hakimumu. Na madhehebu mengine yaliyobaki wamesema ni kuuliwa; kwa Hadith isemayo: “Mtakayempata anafanya vitendo vya watu wa Lut, basi muueni mfanyaji na mfanywa.”

Serikali ya Uingereza imehalalisha ulawiti na kupitishwa na bunge la Britania mnamo mwaka 1967. Gazeti la Al-Ahram la 6.9.1974 likinakili gazeti la Times la London linasema kwamba watu wakubwa wa Uingereza walifanya hafla kusherehekea kuhalalishwa huku kwa ulawiti.

Na wakajionyesha mbele ya mamia ya watazamaji, Hakuna mwenye shaka kwamba kuwoko mabibi na wapenzi katika starehe hii kuliongeza shangwe na furaha!

وَالِى مَدِيْنٍ اَخَاهُمْ شُعَيْبًا قَالَ يَا قَوْمِ اعْبُدُوا اللّٰهَ مَا لَكُمْ مِّنْ اِلٰهٍ غَيْرُهُ قَدْ جَاءَتْكُمْ بَيِّنَةٌ مِّنْ رَبِّكُمْ فَاقُوْا الْكَيْلَ وَالْمِيْزَانَ وَلَا تَبْخَسُوْا النَّاسَ اَشْيَاءَهُمْ وَلَا تُفْسِدُوْا فِى الْاَرْضِ بَعْدَ وُضُوْعِهَا ذٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿٨٥﴾

Na kwa wa Madian (tulimpeleka) ndugu yao Shuaib akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu nyinyi hamna Mungu mwingine zaidi yake, Hakika umewajia ubainifu kutoka kwa Mola wenu. Basi kamilisheni kipimo na mizani wala msiwapunje watu vitu vyao, wala msifanye uharibifu katika ardhi baada ya kutengenea kwake, Hayo ndiyo bora kwenu ikiwa nyinyi mmeamini.

وَلَا تَقْعُدُوْا بِكُلِّ صِرَاطٍ تُوعِدُوْنَ وَتَصُدُوْنَ عَنِ سَبِيْلِ اللّٰهِ مِنْ اَمْرٍ نَّ بِهِ وَتَبْغُوْنَهَا عِوَجًا وَاذْكُرُوْا اِذْ كُنْتُمْ قَلِيْلًا فَكَثَّرَكُمْ وَاَنْظُرُوْا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُفْسِدِيْنَ ﴿٨٦﴾

Wala msikalie kila njia kumwogopesha na kumzuilia njia ya Mwenyezi Mungu mwenye kumuamini na kutaka kuipotosha. Na kumbukeni mlipokuwa wachache Akawafanya kuwa wengi, na tazameni jinsi ulivyokuwa mwisho wa wafisadi.

وَإِنْ كَانَ طَآئِفَةٌ مِّنْكُمْ آمَنُوا بِالَّذِيْ أُرْسِلْتُ بِهِ وَطَآئِفَةٌ لَّمْ يُؤْمِنُوْا فَاصْبِرُوْا حَتَّىٰ يَخْرُجَ اللّٰهُ بَيِّنَاتٍ وَهُوَ خَيْرُ الْحَاكِمِيْنَ ﴿٨٧﴾

Na kama liko kundi miongoni mwenu lililoamini yale niliyotumwa kwayo, na kundi (jingine) halikuamini, basi subirini mpaka Mwenyezi Mungu ahukumu baina yetu; naye ndiye mbora wa wenye kuhukumu.

## SHUAIB

Aya 85 – 87

### MAANA

Na kwa Wamadian (tulimpeleka) ndugu yao Shuaib. Akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, hamna Mungu mwingine zaidi yake.

Umepita mfano wake katika Aya 59 ya Sura hii.

Nabii Shuaib ni miongoni mwa Mitume waarabu; kama vile nabii Hud (a.s) na Nabii Swaleh. Watu wa Madian ni waarabu walikuwa wakikaa katika ardhi ya Maa'n viungani mwa mji wa Sham.

Hakika umewafikia ubainifu kutoka kwa Mola wenu.

Ubainifu ni kila linalobainishiwa haki, ni sawa liwe ni dalili ya akili, au muujiza. Hakuna mwenye shaka kwamba Nabii Suhaib aliwaletea muujiza watu wake unaofahamisha utume wake; vinginevyo angelikuwa ni mtabiri sio Mtume, Hakuna nukuu ya Qur'an inayofahamisha aina ya muujiza huu. Kuuelezea ulivyokuwa, kama ilivyo katika baadhi ya Tafsir, ni kusema juu ya Mwenyezi Mungu bila ya ujuzi.

**Basi kamilisheni kipimo na mizani wala msiwapunje watu vitu vyao.**

hii inashiria kwamba wao walikuwa wanafanyiana vibaya katika biashara, na kwamba hilo lilikuwa limeenea kwao. Kwa hivyo aliwaamrisha kukamilisha kipimo cha ujazo na mizani baada ya kuwaamrisha kumpwekesha Mwenyezi Mungu (Tawhid). Kisha akawaamrisha uadilifu na kuacha kupunja katika haki zote za kimaada, kama vile elimu na maadili; wasimsifu mjinga kwa elimu wala kwa mhaini kwa uaminifu.

**Wala msifanye ufisadi katika ardhi baada ya kutengenea kwake.**

Imepita tafsir yake katika Aya 56 ya Sura hii kifungu 'Mwenyezi Mungu aliitengeneza ardhi na mtu akaiharibu'

**Hayo ndiyo bora kwenu ikiwa nyinyi mmeamini.**

Hayo, ni ishara ya hayo matano yaliyotangulia: Kumwabudu Mwenyezi Mungu, kukamilisha vipimo na mizani, na kuacha kupunja na ufisadi.

**Wala msikalie kila njia kumuogopesha na kumzuilia njia ya Mwenyezi Mungu mwenye kumwamini na kutaka kuipotosha.**

Huu ni ubainifu na tafsir ya kauli yake Mwenyezi Mungu: Wala msifanye uharibufu katika ardhi. Kwa sababu maana yake ni: Msiwatie shaka na kuwatisha ikiwa wanataka kumwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala msimzuie Muumin kusimamisha nembo za dini, msije mkamzuia na njia ya Mwenyezi Mungu iliyo sawa na kujaribu kuwapeleka watu kufuata njia ya kombo mnayoifuata nyinyi.

Ufafanuzi zaidi na ufupi wa tafsir ya Aya hii ni yale yaliyopokewa kutoka kwa Ibn Abbas kwamba wao walikuwa wakikaa njiani kuwahofisha watu wasimwende Nabii Shuaib <sup>(a.s)</sup> na kuwaambia kuwa yeye ni mwongo atawafitini na dini yenu.

**Na kumbukeni mlipokuwa wachache akawafanya kuwa wengi.**

Mwenyezi Mungu amewajalia kuwa matajiri baada ya kuwa mafukara, wenye nguvu baada ya kuwa wanyonge, na wengi baada ya kuwa wachache. Na tazameni jinsi ulivyokuwa mwisho wa waharibifu.

Yaani yasije yakawapata yaliyowapata waliofanya uharibifu katika nchi; mfano watu wa Nu, Hud, Swaleh na Lut <sup>(a.s)</sup>.

**Na kama liko kundi miongoni mwenu lililoamini yale niliyotumwa kwayo na kundi (jingine) haliamini, basi subirini mpaka Mwenyezi Mungu ahukumu baina yetu.**

Kundi moja lilimwamini Nabii Shuaib <sup>(a.s)</sup> na jingine likamkanusha. Akayataka makundi yote yaishi kwa amani na kila kundi liachane na jingine bila ya kumtaaradhi yeyote kwa kukumuudhi; ni sawa awe amechagua ukafiri au imani, kisha yote mawili yataongoja mpaka Mwenyezi Mungu awahukumu.

**Naye ndiye mbora wa wenye kuhukumu.**

Wala hakuna wa kupinga mantiki hii. Utampinga na nini anayekuambia: 'Ngoja Mungu atakuhukumu?.'

15

**SHARTI YA KUCHAPA**

Sharti ya kuchapa au kusambaza ni kutaja rejeo hili. haki zote zimehifadhiwa na Taasisi ya Al-Hasanain Taasisi ya Imamu Husein (a.s)

Site ya Al-Imaamaini Al-Hassanaini (a.s) ya usambazaji wa utamaduni wa Kiislamu na mafunzo ya Kidini.

**MWISHO WA JUZUU YA NANE**

## YALIYOMO

<b>1</b> .....	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>	
	IMEANDIKWA NA: SHEIKH MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYA	
		1
1	..... IMETAFSIRIWA NA: SHEIKH HASAN MWALUPA	
1	..... IMEHARIRIWA NA: USTADH ABDALLAH MOHAMED	
1	IMEPANGWA KATIKA KOMPYUTA NA: UKHT PILI RAJABU	
1	..... UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI	
2	..... MAKOSA YA CHAPA	
<b>3</b> .....	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>	
3	.....AINA YA WATU AYA	
3	..... MAANA	
6	.....NIMTAFUTE HAKIMU ASIYEKUWA MWENYEZI MUNGU	
6	..... MAANA	
<b>8</b> .....	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>	
8	..... BISMILLAH KWA KINACHOCHINJWA	
8	..... MAANA	
10	..... KUMHUISHA MAITI	
10	..... MAANA	
11	.....MWENYE KUULIZWA NA MUULIZAJI MKUU	
<b>14</b> .....	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>	
14	..... HUMFUNGULIA KIFUA CHAKE UISLAM	
14	..... MAANA	
16	..... SIKU ATAKAPOWAKUSANYA WOTE	
17	..... MAANA	
<b>19</b> .....	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>	
19	.....NA MOLA WAKO NDIYE MKWASI	
19	..... MAANA	
21	.....HUSEMA: HII NI SEHEMU YA MWENYEZI MUNGU	
21	..... MAANA	
24	.....KULENI MATUNDA YAKE	
24	..... MAANA	
<b>26</b> .....	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>	
26	.....SIONI KATIKA NILIYOPEWA WAHYI	

26	MAANA
28	ANGELITAKA MWENYEZI MUNGU TUSINGELISHIRIKISHA
28	MAANA
<b>31</b>	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>
31	ALIYOWAHARAMISHA MOLA WENU
31	MAANA
32	NASAHA KUMI
34	KISHA TULIMPA MUSA KITAB
35	MAANA
<b>37</b>	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>
37	HAITAMFAA MTU ILA IMANI YAKE
37	MAANA
40	SEMA MOLA WANGU AMENIONGOZA
40	MAANA
41	KILA MTU NA MZIGO WAKE
42	ARDHI NA NYUMBA
43	MWISHO WA SURU YA SITA: AL-AN'AM
<b>44</b>	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>
44	KITABU KIMETEREMSHA KWAKO
44	MAANA
45	NA MIJI MINGAPI TULIANGAMIZA
45	MAANA
46	MIZANI YA MATENDO
48	NA HAKIKA TULIWAUMBA
48	ASILI YA MTU
48	MAANA
<b>53</b>	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>
53	NA WEWE ADAM KAA PEPONI PAMOJA NA MKEO
53	MAANA
55	KISA CHA ADAM KAMA KILIVYO KATIKA QUR'AN
57	KIVAZI CHA KUONEKANA NA KISICHOONEKANA
57	MAANA
<b>59</b>	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>
59	WANAPOFANYA UCHAFU
59	MAANA
61	CHUKUENI MAPAMBO YENU

61	.....	MAANA
<b>65</b>	.....	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>
65	.....	WANAOGOPA NA KUFANYA MEMA
65	.....	MAANA
67	.....	NGAMIA NA TUNDU YA SINDANO
67	.....	MAANA
69	.....	WATU WA PEPONI WATAITA
69	.....	MAANA
<b>70</b>	.....	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>
70	.....	WATU WA A'RAF
70	.....	A'RAF
73	.....	WATU WA PEPONI NA WA MOTONI
73	.....	MAANA
<b>75</b>	.....	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>
75	.....	KATIKA SIKU SITA
75	.....	MAANA
		MWENYEZI MUNGU AMEITENGENEZA VIZURI ARDHI NA
77	.....	BINADAMU AKAIHARIBU
79	.....	APELEKAYE PEPO KUWA BISHARA
79	.....	MAANA
<b>81</b>	.....	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>
81	.....	MAANA
83	.....	HUD
83	.....	MAANA
86	.....	SWALEH
86	.....	MAANA
<b>89</b>	.....	<b>TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA NANE</b>
89	.....	LUT
89	.....	MAANA
91	.....	SHUAIB
91	.....	MAANA
93	.....	SHARTI YA KUCHAPA
93	.....	MWISHO WA JUZUU YA NANE
94	.....	YALIYOMO